ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 10 Julai, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti, (Mahmoud Muhammed Mussa) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 86

Kukosekana Nambari za Nyumba Shehia ya Ole

Mhe. Farida Amour Moh'd – Aliuliza:-

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la mwanzo katika siku ya leo ya Ramadhani. Pili naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia siku hii ya leo ya Ramadhani pia ninamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie tuifunge Ramadhani tukiwa salama na atupokelee funga zetu. *(Makofi)*

Kwa kuwa suala la nambari za nyumba ni muhimu sana na hivyo kila Shehia ni vyema kujua nambari yao ya nyumba, kwani hutumika katika maandiko mbali mbali ya Kitaifa (*Public Registrations*). Vile vile katika Shehia ya Ole nyumba zao hazina nambari zilizotolewa na Sheha (Serikali) badala yake hulazimika kutumia nambari ilizotolewa na miradi ya mashirika mbali mbali mfano (Mradi wa *ZINC*).

(a) Je, kufanya hivyo ni sawa.

(b) Hatua gani zitachukuliwa kuzipatia nambari nyumba hizo.

Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 86 lenye sehemu (a) ,(b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa ziko nyumba ambazo zimewekewa nambari za utambulisho kupitia mapango wa kuzuia Malaria Zanzibar unaosimamiwa na Wizara ya Afya na

mipango mengine ikiwemo mradi wa *ZINC*. Hata hivyo, uwekaji na nambari hizo sio kosa kisheria kwani zinasaidia ufumbuzi wa nyumba hizo kirahisi wakati wa utekelezaji wa mradi husika.

b) Katika kuhakikisha kuwa nyumba zote zinapatiwa nambari sahihi, serikali ina mpango maalum na hatua ya awali imeanza kwa kuwapatia madaftari maalum ya usajili Masheha wote wa Zanzibar kwa lengo la kufanya utambuzi wa nyumba zote ziliomo katika Shehia zao pamoja na wakaazi wake.

Pia, kupitia mradi wa *post code* ambao unatekelezwa kwa pamoja baina ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Wizara ya Miundo mbinu na Mawasiliano na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* ambayo ndio mratibu wa mradi huu. Mhe. Mwenyekiti, mradi ulizinduliwa na Dkt. Ali Mohammed Shein tarehe 18 Januari, 2010 huko Arusha wakati alipokuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, mradi una malengo mawili ni pamoja na;

(i) Kuweka majina ya mitaa, yaani *street* kwa maana ya barabara na

(ii) Kuziwekea nambari nyumba zote katika mitaa hiyo.

Kwa upande wa Zanzibar mradi umeanza kutekelezwa katika shehia nne kwa awamu ya kwanza. Shehia za Mombasa na Chukwani kwa Unguja na shehia za Limbani na Selem kwa Pemba.

Mhe. Farida Amour Moh'd: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri. Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba baadhi ya nyumba zimeekewa nambari za mradi, na si kosa na ninakubaliana naye kwamba si kosa.

Lakini kwa kuwa kuna baadhi ya nyumba zimejengwa baada ya kupita ule mradi wa *ZINC* nazo hazina nambari hizo na wala zile za Sheha kwa maana za Vijiji pia hamna. Kwa kuwa nambari za nyumba ni muhimu kama alivyothibitisha Mhe. Waziri kwamba popote unapokwenda unatakiwa nambari ya nyumba.

Je, katika nyumba ambazo bado hazijapata kupimwa na ule mradi wa *ZINC* pamoja na nambari nyengine utawachukulia hatua gani hawa, ili na wao wasipate tabu wakati wanapokwenda eneo husika na kutakiwa nambari za nyumba.

Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, huu mradi ni endelevu. Kwa hiyo, kama zimejengwa nyumba mpya basi wanachotakiwa kufanya ni kujitambulisha kwa sheha wa shehia ile, lakini bila ya shaka nao wakati wa ujenzi pia bila shaka walipita kwa sheha kuthibitishwa kwamba wamepata kiwanja na wanajenga.

Kwa hivyo, hakuna tatizo kwamba wataachwa na wala hawatoachwa, isipokuwa mradi ni endelevu na kama nilivyosema masheha wamepewa daftari na sasa wanatakiwa waorodheshe watu wote katika shehia zao. Lakini jambo la msingi kama anajenga au anahamia basi ni vyema ajitambulishe kwa Sheha wa Shehia wa eneo lile na bila ya shaka na yeye nyumba yake itapatiwa nambari na wala hakuna tatizo lolote.

Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nataka kumuuliza swali dogo tu la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, mradi wa *post code* unahitaji *Master Plan* katika maeneo ili kuweka wepesi wa mambo mawili; yaani kuweza kuweka nambari za nyumba pamoja na kuweka majina ya mitaa. Kwa bahati nzuri imeanzia katika maeneo yenye *Master Plan* ya Chukwani na Mombasa.

Lakini katika nchi yetu tunayo matatizo ya *Master Plan* katika maeneo ya Kwamtipura, Mboriborini. Mhe. Mwenyekiti, tatizo kubwa la maeneo hayo unaikuta nyumba upande wa mbele uko Kwamtipura na nyuma uko Mwembemakumbi. Je, wizara yako ina mpango gani katika kuweka suala hili kwenye maeneo ambayo hayana *Master Plan*.

Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, suala la *Master Plan* ya Mji wetu tayari limo katika maandalizi na wizara husika, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati hilo wanalishughulikia kikamilifu kupitia Idara yake ya Mipango Miji, na sisi ni wadau wakubwa sana wa hiyo *Master Plan*, kwa sababu katika ukataji wetu wa Shehia, Wadi, Wilaya na hata Mikoa tunaisubiri hiyo *Master Plan*.

Kwa hivyo, kazi tayari imeshaanza na walichelewa kidogo, isipokuwa naomba tuwe na subira tu na hiyo kazi inaendelea. Mhe. Mwenyekiti, nataka

kusisitiza tu kwamba utoaji wa majina ya mitaa tunawategemea wananchi wenyewe wenye mitaa, kwa sababu kumeshatokea migongano na mivutano, kwamba sisi tunataka jina hili na wengine wanataka jina jengine.

Kutokana na hali hiyo, naomba sana tushirikiane na tutoe yale majina halisi na waliokubaliana wao. Kwa mfano, kwa Pemba kidogo tulichelewa kwa sababu ya mivutano ya majina ya mitaa ile. Mhe. Mwenyekiti, nawaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi, kwamba tusaidiane na madiwani wetu, ili tupate majina halisi yaliyokusudiwa katika mitaa ile.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa nambari za nyumba ni muhimu, na kwa kuwa kuna tabia ya masheha kusema hawawaelewi wananchi waliomo katika shehia zao na nyumba wanazotoka. Vile vile Mhe. Rais amezindua mpango huu muda mrefu. Je, Mhe. Waziri wizara yako ina mpango gani wa kuharakisha suala hili, ili usumbufu huu uondoke.

Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema ni kwamba tatizo si kubwa, isipokuwa ni kwamba wale wote wanaohamia kwenye shehia na sasa masheha wamepewa daftari, basi wanaporipoti kwenye shehia ile basi wakaripoti kwa sheha na barua ya walikotoka huko wakajitambulishe kwenye shehia ile watambulikane, na wala tusijifanye tunakwenda kulala tu kwenye nyumba ile, yaani unaingia na kutoka usiku hutambulikani sivyo.

Kwa hivyo, tujiandikishe, tujulikane na nyumba zote kwa utaratibu huu zitapatiwa sasa nambari. Vile vile kama nilivyosema Sheha ameshapatiwa daftari ataorodhesha wananchi wake wote katika eneo lile na hilo ni suala la msingi kabisa.

Nam. 48

Malipo ya Fidia kwa Wakulima wa Bungi

Mhe. Salim Abdalla Hamad – Aliuliza:-

Kabla ya ujenzi wa mtambo wa kurushia matangazo eneo la Bungi. Wizara ya Kilimo na Maliasili ilitumia Afisa wake wa Kilimo wa Wilaya kufanya makisio ya kitaalamu ya waathirika katika ujenzi huo kutokana na vipando vyao walivyokwishalima. Matokeo ni kuwa wizara hii iliwalipa waathirika hao kinyume na makisio ya mtaalamu huyo.

(a) Ni kitu gani kilichosababisha kulipwa waathirika hao kinyume na makisio ya mtaalamu huyo.

(b) Nani aliyehusika na kupanga makisio mapya na kwa nini.

(c) Kwa sababu waathirika wale wengine hawakuridhika, wizara haioni kuwa iko haja ya kuangalia suala hili upya, ili papatikane makubaliano baina ya wizara na waathirika

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 48 lenye kifungu (a), (b), na (c) kama hivi ifuatavyo:-

a) Ni kweli Afisa wa Kilimo wa Wilaya alifanya makisio ya mazao ya wananchi walikuwa waliazimwa eneo la Bungi kwa shughuli za kilimo. Katika makisio ya awali Afisa huyo wa Wilaya alifanya makisio ambayo ni makubwa sana ambayo serikali haikuyakubali.

   Mhe. Mwenyekiti, tulichokiamua ni kumtaka afisa huyo kufanya tathmini nyengine ya kitaalamu pamoja na pia kutoa muda kwa baadhi ya wakulima kuvuna mazao yao yaliyokuwa karibu na kuvunwa. Tathmini ya pili ilifanywa na afisa huyo iliyozingatia uchanga, upevu na wingi wa mazao hayo ilifikia shilingi milioni 15, ambayo ndiyo iliyolipwa. Hivyo malipo yaliyotolewa hayakufanywa kinyume na makisio ya mtaalamu huyo.

b) Aliyehusika na kupanga makisio ya pili ni Afisa huyo huyo wa kilimo Wilaya ya Kati.

c) Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu haihusiki na utayarishaji wa makisio ya mazao ya wakulima, hivyo haioni haja ya kuliangalia upya suala hilo kwa ajili ya kutaka kupatikana makubaliano kati ya Wilaya yangu na waathirika.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa jibu lake na ninakubaliana naye kwamba Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo haihusiki na upangaji wa bei ya wale walioathirika.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu aliyekwenda kule ni Mtaalamu wa Kilimo wa Wilaya na kuweka makisio yake kwa kila mtu kutokana na kipando alichokuwa nacho na akapeleka barua yake au taarifa hiyo Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, kwa ajili ya walipe malipo hayo, na

baadaye Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo fedha zile zilizotajwa mwanzo milioni 70, 205,368.5/= na matokeo yake wakalipwa watu wote 43 shilingi milioni 15, 036,761/= tu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, naomba uende kwenye swali la nyongeza.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, swali ni hili, ili nifahamike naomba unipe muda kidogo. Kutokana na hali hiyo, kama mkulima Msafiri Ezakiel Msafiri alikuwa alipwe shilingi milioni 3, 000,000/=, lakini amelipwa shilingi 900,000/= tu, na mwengine Edward Abiria Masoud alikuwa alipwe shilingi milioni 3, 000,000/=, lakini amelipwa shilingi 800,000/= tu na wengi wengine sitawataja kutoka na wakati hatuna.

Mhe. Mwenyekiti, haoni kuwa kwa sababu hawa wenyewe hawakulipwa na malipo haya na mimi waliniita nikaenda kushuhudia. Kwa hivyo, nadhani ipo haja kwa ajili ya kuondoa matatizo Mhe. Waziri kukubali kukutana tena na Wizara ya Kilimo na Maliasili, ili kuangalia upya malipo haya kwa vile hayalingani kutokana na ilivyokuwa mwanzo na mabadiliko yaliyotokea wakati wa ulipaji.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwenye jibu langu mama nimeeleza vizuri na nimefahamisha vizuri, kwa sababu ya kusema hivyo Mhe. Mwakilishi yeye alikuwa ni Mjumbe wa Kamati na kwa kweli suala hili tuliwapa Wajumbe wa kamati kwa ajili ya kuifuatilia na wala hawakuweza kulifuatilia.

Lakini wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Maliasili makisio ya mwanzo ilikuwa ni shilingi milioni 71. Kwa hivyo, kama nilivyoeleza ni kwamba malipo haya kwa serikali yalikuwa ni makubwa sana, na baadaye tukarudi tena kwa afisa huyo huyo na tukafanya makisio ya mara ya pili na tukapata shilingi milioni 15.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu imelipa na kwa kweli wakulima hao wameridhika. Sasa nimuombe Mhe. Mwakilishi kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba kwa imani yangu nikiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kushirikiana na Mhe. Mwakilishi pamoja na wakulima, basi tukae pamoja kwa ajili ya kulifuatilia suala hili, ili apate usahihi wa malipo haya tuliyafanya. *(Makofi)*

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, mimi kidogo napata mashaka katika hili. Kwa kweli kama Afisa wa kilimo alikwenda kufanya tathmini zikagundulikana ni milioni 72, na wizara ikaona nyingi na wakafanya utafiti wanaona milioni 12. Hali

hii, maana yake lazima kutakuwa na jambo aidha la udanganyifu kama si afisa basi ni wizara.

Je, wizara imefanya mipango au imechukua hatua gani kujua tatizo lililosababisha mwanzo makisio yawe 72, 000,000/= na baadaye yashuke hadi milioni 12, 000,000/=, wizara imegundua kitu gani ambacho kimesababisha suala hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi, kwamba tulipohama kuelekea Bungi kwa kweli kulikuwa na vipando vya wakulima na vyengine ilikuwa ni karibu kuvunwa na vyengine ilikuwa ni uche tu.

Lakini kama nilivyoeleza mwanzo Afisa huyu wa Kilimo alifanya makisio ambayo yalikuwa hayana utaratibu na utaalamu ndipo tukarudi tena mwanzo, ili kumtaka afanye makisio. Mhe. Mwenyekiti, nadhani ni vyema Mhe. Mwakilishi atuamini, kwa sababu sisi pale Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ndio tuliolipa na wenyewe wakulima waliridhika.

Hata hivyo, Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili nimemhakikishia kuwa tukae pamoja, ili afahamu vizuri na aridhike kwenye nafsi yake kujua kwamba makisio yaliyofanywa ni haya na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ndio iliyolipa.

Nam. 125

Malipo Maalum ya Usafiri kwa Wafanyakazi wa Wizara ya Afya – Pemba

Mhe. Rufai Said Rufai – Aliuliza:-

Kwa kuwa Wizara ya Afya ina tatizo kubwa la nyumba za makaazi ya wafanyakazi katika Hospitali zake za Pemba, hivyo kusababisha wafanyakazi wa hospitali kutembea masafa marefu hadi katika vituo vyao vya kazi, ambapo kwenda na kurudi hugharamia zaidi ya shilingi 3,000/= kwa siku ambacho ni sawa na shilingi 90,000/= kwa mwezi. Ukitilia maanani kwamba serikali haitoi "*special bus fare*" nauli maalum kwa Wizara ya Afya.

(a) Je, serikali haioni kwamba huku ni kuwazidishia mzigo mkubwa wa gharama ya maisha kwa watendaji wake

(b) Je, ni lini serikai itatoa malipo maalum ya nauli kwa wafanyakazi wa Wizara ya Afya Kisiwani Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda nitoe mkono wa Ramadhani kwa Waheshimiwa Wawakilishi, wafanyakazi wote wa Baraza pamoja na wale wote wanaofanikisha Baraza hili. Ramadhani Karimu.

Baada ya kusema hayo, Mhe. Mwenyekiti napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 125 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia wizara inajitahidi kwa kupitia wafadhili wa miradi mbali mbali kama vile *DANIDA*, *ADB* na wengine kujenga nyumba za wafanyakazi, kila pale wizara inapobuni miradi mipya basi kipengele cha nyumba za wafanyakazi kinakuwemo. Vile vile pale kituo kipya kinapojengwa na wizara basi inahakikisha inajenga na nyumba, kwa vile vituo vinavyojengwa kwa vile vituo vinavyojenga kwa nguvu za wananchi kila inapopata ufadhili.

Wizara imekuwa ikishauri Wawakilishi, Wabunge na wananchi badala ya kuendelea kujenga vituo ambavyo kwa kiasi fulani tumefikia lengo, na wakajikita kujenga nyumba za wafanyakazi au wakijenga kituo ni vyema ijengwe na nyumba, ili wizara iweke samani, na kuleta wafanyakazi, kwa sababu hilo ndilo jukumu la wizara.

Mhe. Mwenyekiti, wizara bado inasisitiza kwamba ni vizuri kwa wananchi kujenga nyumba za wafanyakazi na sio kwa tatizo la usafiri bali kuwa na mfanyakazi karibu na kituo masaa 24.

Katika mshahara wa wafanyakazi wa afya suala la usafiri limeingizwa, najua hazitoshi lakini ndizo zilizopo. Lakini jengine linalojitokeza hasa kwa Pemba, wafanyakazi hawapendi kukaa kwenye nyumba za wafanyakazi hata kama nyumba ipo na wanapendelea kukaa makwao, ili waweze kujiimarisha au sababu nyengine wanazozijua wao wenyewe.

Kwa hivyo, wale ambao nyumba haziko na hawajakataa kukaa karibu na vituo na pengine wanatumia nauli zaidi ya moja kweli hao tumewafikiria na tunalichukulia hatua, ili tuweze kuona jinsi gani tutawasaidia.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na amekubali kwamba mara hii wameongezewa posho la usafiri ijapo kuwa halitoshi. Kwa kuwa baadhi ya wafanyakazi hawa wana usumbufu wa tatizo la usafiri ukilinganisha na maeneo wanayoishi na

wanakofanya kazi. Vile vile kwa kuwa wizara bado haijakuwa na majengo hasa hospitali za kule Pemba. Je, kwa sasa haoni serikali kuwakopesha angalau vile vyombo vya moto kuweza kwenda na kurudi kazini kwa wakati.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, sisi kama Wizara ya Afya sitaki nilibebe jukumu hilo kwa sababu fedha zetu pamoja na shughuli zake munazijua na serikali imelisikia hilo. Kwa hivyo, tutalipeleka na tutalifanyia kazi na kama itawezekana, lakini ninachokisema ni kwa wale ambao tunajua kwamba tatizo la usafiri lipo kama Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwamba inafanya mahesabu na itawalipa, basi na sisi tutafanya mahesabu tutaweza kujua ni kiasi gani kinachohitajika, ili tuweze kuwaombea kwa ajili ya kulipwa kwa hivi sasa. *(Makofi)*

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa fursa nikaweza kuuliza swali moja dogo la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri. Kwa kuwa serikali imejitahidi kujenga vituo vya afya pamoja na nyumba za madaktari, lakini zipo nyumba za madaktari ambazo hazijahamiwa, hali ambayo inaleta usumbufu kwa wananchi wanapotaka huduma wakati wa usiku. Je, serikali ina mpango gani wa kupeleka madaktari kwenye nyumba hizo, ili lengo lililokusudiwa liweze kufikiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli anayoyasema kuna baadhi ya nyumba zimejengwa ndio kama hizo ninazozisema za Pemba, kwamba wafanyakazi wapo lakini kukaa hawataki na hapa Unguja pia nyumba zipo na wafanyakazi wapo na kukaa hawataki na wanazo sababu nyingi tu wao wenyewe.

Kwa mfano, Ukongoroni iko nyumba na mfanyakazi anakaa Bwejuu, mke wa mtu na mumewe hataki mkewe akae kule na hilo ni suala la msingi. Lakini hata hivyo, nyumba kuwepo pale ni lazima kwa sababu vituo vya afya vina kada nyingi za wafanyakazi. Sasa wale wengie tutakapojaaliwa kuweza kujaliza basi kuna wengine lazima watakaa.

Kwa hivyo, tutaendelea kujenga, na kwa yule ambaye hatuoni sababu ya msingi kwa nini hakai, basi tutamwambia akae na kama hatokaa basi hatutomlipa nauli ya kumpeleka kule na kurudi na tutahakikisha kwamba afike kazini asubuhi saa inayotakiwa na wala asiwe na kisingizio kwamba nilikosa gari au nimechelewa, ili tuweze kuhakikisha kwamba tunafikisha huduma kwa wananchi kama vile tulivyojipangia.

Nam. 120

Ukosefu wa Maji Safi na Umeme Shehia ya Kijini – Matemwe

Mhe. Kazija Khamis Kona – Aliuliza:-

Shehia ya Kijini iliopo Jimbo la Matemwe hadi hivi sasa haijapatiwa huduma muhimu ya maji safi na salama, jambo ambalo linaathiri maendeleo yao na ni hatari sana kwa afya zao. Zaidi ya hayo, Shehia ya Kijini pia inakosa huduma adhimu ya umeme ambayo ni kiungo muhimu, kwa ajili ya maendeleo yao ya kiuchumi.

Je, ni lini hasa wizara yako itawapelekea wananchi hawa huduma hizi muhimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nam. 120 kama ifutavyo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba kukubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa Shehia ya Kijini iliopo Jimbo la Matemwe hadi hivi sasa haijapatiwa huduma muhimu ya maji safi na salama, jambo ambalo linaathiri maendeleo ya wananchi wa Jimbo hilo.

Serikali kupitia wizara yangu imechukua juhudi kwa kiasi kikubwa kwa kuwapatia wananchi wa mijini na vijijini huduma ya maji safi na salama, na kwa sasa huduma ya maji mijini na vijijini imeimarika kiasi. Maeneo machache yaliyobakia wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar (*ZAWA*) bado inaendelea na mipango ya kuwaondoshea tatizo la upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kupitia washirika wa maendeleo (*Development Partners*) pamoja na nguvu za ndani.

Aidha baadhi ya vijiji vinavyotegemewa kunufaika na huduma hiyo kupitia ujenzi wa mradi mkubwa wa maji unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) ni kijiji cha Kijini.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu umeme katika eneo la Kijini ahadi yangu iliyotolewa siku ya ufunguzi wa Skuli ya Mbuyu Tende iko pale pale na *ZECO* wataitekeleza kwa mwaka huu wa fedha.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza.

a) Mhe. Naibu Waziri alivyojibu swali lake amesema kwamba serikali imechukua juhudi mbali mbali. Nataka kujua juhudi hizo ni zipi.

b) Mhe. Waziri alisema kwamba Wizara yake inaendelea na kuchukua juhudi kuhakikisha kwamba wananchi wale wanaondokana na tatizo hilo. Je ni lini wananchi wale wataondokana na tatizo hilo.

c) Mhe. Naibu Waziri alijibu kwamba ahadi yake ipo pale pale. Ahadi hiyo itatekelezwa mwaka gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, ahadi zinazotekelezwa au ahadi anazotaka kujua kama nilivyoeleza tuna miradi imeshaanza shughuli zake, hususan katika maeneo ya Kaskazini kupitia jimbo la Matemwe, Mradi wa AfDB ambao kwa sasa hivi wameshaanza kutandika mabomba na tayari tumeshaanza kuchukua juhudi za kujenga matangi, tumeshaweka nondo kwenye matangi na tayari sasa hivi tuko katika hatua za kuweka sakafu kwenye matangi hayo.

Maeneo ya Kijini tumeshachimba mitaro na wakati wowote tutaanza kutandika mabomba yetu. Hizo ni juhudi ambazo tayari zinachukuliwa na wizara yangu. Kama nilivyomueleza kwamba mradi huu au ahadi hiyo itakamilika pale tu miradi hii itakapomaliza shughuli zake.

Kuhusu suala la umeme kama nilivyoeleza kwamba katika mwaka huu wa fedha basi watu wetu wa ZECO wataelekea huko na kwenda kuwawekea huduma hiyo ya umeme wananchi wa Kijini. Kwa sababu huduma hiyo haiko mbali, *line* zetu za XT ziko pale isipokuwa *line* za LV ndio bado hatujazipeleka katika kijiji hicho. Kwa hiyo watu wangu wa ZECO wakati wowote ndani ya mwaka huu wa fedha watakuwepo hapo kwa ajili ya kulishughulikia suala hilo na wananchi hao wa Kijini watanufaika na huduma hiyo ndani ya mwaka huu wa fedha.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuwa maji ni uhai na bila ya maji hakuna maisha, na kwa kuwa tatizo la maji si tu kijiji alichokitaja Mhe. Kazija, nchi hii tatizo la maji ni nchi nzima. Tukitilia maanani kuwa huu ni Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, sasa hivi kuna vijiji kadhaa maji hayafiki kikiwemo Kijiji changu cha Sikwese. Je, wizara yako ina mpango gani kuhakikisha angalau kwa mwezi Mtukufu wa Ramadhani watu wanapata maji.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu inaelewa kwamba tatizo la maji ni kubwa na maji ni uhai, hilo tunalielewa. Nitakavyosoma bajeti yangu kesho ataona kwamba asilimia 70

ya matumizi ya bajeti yangu mwaka huu yamekwenda kwenye maji, kwa sababu nataka tulishughulikie kweli kweli suala hili la tatizo la maji.

Miradi imeshaanzishwa; kuna miradi ya maji vijijini na kuna miradi ya maji mijini ambayo hivi sasa inaendelea kutekelezwa. Kwa hivyo tuvute subra kidogo *Inshallah* Mwenyezi Mungu akipenda matatizo ya maji yatapungua sana. Mwezi huu wa Ramadhani nimetoa jana tangazo kwamba kwa yale maeneo ambayo yana matatizo ya maji wawasiliane na ZAWA tutawapelekea maji kwa zamu kwa kutumia magari tuliyonayo kwa ajili ya kufanya shughuli hiyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kwanza nataka nimpongeze kwa dhati kabisa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji kwa juhudi anazozichukua pamoja na watendaji wake. Lakini bila ya kuwa na nyenzo hawa watu tutawalaumu na tutaendelea kulaumu. Hawa ni watu ambao wanafanya kazi lakini vitendea kazi hawana na bajeti yao imekuwa ndogo.

a) Katika swali la msingi lililoulizwa hapa kuna Shehia kama hii Muyuni inahusu Bwejuu na Kitogani kwa muda mrefu sasa shehia hiyo inakosa maji pamoja na jitihada zinazochukuliwa na viongozi wao. Je, serikali inatoa kauli gani kuhusu suala hili

b) Kwa vile leo pengine mchana tutasoma Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, je wizara imetenga kiasi gani kuipa nguvu sekta hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, amesema kwamba suala hili la msingi linafanana na tatizo alilonalo yeye katika Jimbo lake. Napenda kujibu tena kwamba Wizara, ZAWA, na Serikali kwa jumla inajua kwamba tatizo la maji ni lazima kipindi hichi lishughulikiwe kwa nguvu zote.

Kipindi kilichopita tulikuwa tunashughulikia masuala ya umeme, *Alhamdulillah* tumefika pazuri. Mwaka huu tunashughulikia tatizo la maji na hivi sasa tuna miradi ambao mmoja umeshaanza. Ras el Khaima tayari wako kwenye maeneo huko wanaanza kuchimba visima kutafuta maji. Wachina na wao wana ahadi vile vile ya kuja kuendelea na mradi huu kwenye bajeti hii tunayoendelea nayo.

Kwa hivyo napenda kumjulisha kwamba pamoja anahisi kwamba kuna matatizo ya zana na wakati fulani aliwahi kusema Mhe. Jaku kwamba kuna tatizo la mashine ya kuchimbia kisima. Tumeshanunua mpya na imeshafika hapa Unguja na Ras el Khaima na wao wamekuja na mashine zao na

wameshaanza kazi hii ya kuchimba visima. Kwa hivyo tuvute subra tu Mwenyezi Mungu atatujaalia tutaondokana nalo suala hilo.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe wakati majadiliano yakiwa yanaendelea napenda kuchukua fursa hii kuwatangazia kwamba kwa siku ya leo kuna wageni, na wageni wetu wa leo ni wanamichezo ya timu ya Kijangwani, Jimbo la Kwahani ambao ni mabingwa wa daraja la tatu Wilaya ya Mjini mwaka 2013. Naomba wasimame. *(Makofi)*

Wanamichezo hawa wanatokea jimbo la Kwahani, jimbo ambalo linasimamiwa na Mhe. Ali Salum Haji, tunawapa hongera kwa ushindi huo. Lakini pia Mhe. Ali Salum Haji baada ya kuwa vijana hawa wamepata ushindi huo anawatunukia zawadi ya shilingi laki tano. (*Makofi*)

Baada ya maelezo hayo Waheshimiwa Wajumbe sasa tunaelekea katika harakazi zetu za kuchangia. Napenda niwafahamishe Waheshimiwa Wajumbe kwa sasa nina orodha ya watu wanane na tunatarajia michango ya wachangiaji kutokana kwamba muda wetu umetuacha mkono tumalize saa 6:00 baada ya saa 6:00 tumkaribishe Mhe. Waziri ili aje kufanya majumuisho. Ningeliwaomba sana wale Wajumbe ambao wanaokuja kuchangia wajitahidi waende katika *points* zile ambazo zitakuwa hazina marudio. Ahsante.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya mwanzo ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujaalia kutufikisha siku ya leo tukiwa wazima na afya njema. Pia nimuombe Mwenyezi Mungu atujaalie tuifunge Ramadhani kwa salama, atujaalie tupate fadhila ya Ramadhani hii na ya mwakani.

Mhe. Mwenyekiti, ingawaje umeshaweka misingi ya kuchangia kwa muda mfupi, lakini tutaendelea hivyo hivyo. Hii wizara unavyoiona ni wizara ndogo lakini ni wizara kubwa, ni wizara mama, inayosimamia mambo ya jamii, sasa kuipa muda mfupi huo uliofikiriwa naona si sahihi.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri pongezi za dhati kabisa pamoja na watendaji wake jinsi walivyotuletea hotuba yao hii adhimu. Nataka nianze mchango wangu kwenye sehemu ya udhalilishaji wa wanawake kijinsia. Katika dunia kuna mambo yanakera sana na katika jambo linalokera kupindukia ni suala la udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme tunaiona sana na tunaithamini jitihada ya Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Vijana wanayoichukua katika kuhakikisha suala hili linaondoka lakini kwa bahati mbaya sana, juu ya jitihada zao zote wanazozichukua kufungua *One Stop Center*, kuandaa semina, mafundisho haya na yale, lakini bado tatizo hili ni kubwa na linatisha katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo la udhalilishaji sijui tulizungumzie kinamna gani mpaka lionekane kama hili ni tatizo. Naomba nipeleke kilio changu kikubwa kwa Mhe. Rais kwa sababu Mhe. Waziri na wizara yake kila wanavyojitahidi suala hili bado halijapatikana ufumbuzi. Naomba nimwambie Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kama hajalisimamia mwenyewe suala hili kwa umakini sana basi hatimaye kesho na keshokutwa tutaambukia taifa lenye watu waliokuwa hawana uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu kuna kesi nyingi za udhalilishaji. Kuna udhalilishaji wa aina nyingi. Kuna udhalilishaji wa watoto wetu chini ya umri wa miaka mitano, na wanaowadhalilisha watoto hawa ni watu wazima na akili zao. Baadhi yao huchukuliwa wakapelekwa vituoni na watoto wengine walemavu na huthibitisha kwamba huyu ndiye aliyenifanyia tendo hili lakini bado serikali imekaa, hatujui ushahidi gani tena wanaoutaka.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili linatutisha, watoto wetu hawana uhakika wa kutembea, hawana uhakika wa kucheza, hawana uhakika wa uhuru wao wa kupita popote pale ilimradi hili ni balaa limetuingilia. Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Rais wa nchi hii kama anatupenda wananchi wake, kama anapenda kurudisha hadhi ya nchi hii basi suala hili alisimamie mwenyewe kwa sababu vyombo vya maamuzi inaonekana bado havijaamua.

Mhe. Mwenyekiti, vyombo vya maamuzi hasa hapa tunapopeleka kelele zetu ni Mahkama na Polisi lakini hawajataka kulichukulia uzito hili suala, sasa sijui ni kwa tatizo gani. Ukizungumza unaambiwa ushahidi, ushahidi, ushahidi, jamani hivi ushahidi gani. Mtu anakamatwa na motto wa watu tayari keshamkalia katika hali isiyojulikana halafu yeye bado mnataka ushahidi, ushahidi upi tena unaotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimwambie Mhe. Waziri ashirikiane na Wizara ya Afya na kutafuta wafadhili wa sehemu mbali mbali kama tatizo pengine ni hicho chombo cha kutafutia ushahidi, basi kwa vyovyote itakavyokuwa kama lilivyokuwa suala la meli iliweza kupatikana basi na suala la DNA nalo tujitahidi liweze kutafutiwa wafadhili. Tunajua kwamba serikali yetu haina uwezo wa kufanya mambo yote hayo lakini itafute yale mambo ya kipaumbele.

Athari za kudhalilishwa watoto wetu ni kubwa zaidi kuliko kitu chengine chochote. Watoto wetu ndio taifa la kesho na ndio tunaowategemea lakini leo watoto wote wanaharibiwa si wa kike si wa kiume. Kwa sababu mtoto ukimzoesha tendo baya utotoni katika umri mdogo na hukumu haichukuliwi sasa pale kila mmoja ataona ni mambo ya kawaida, matokeo yake watoto wote wataharibiwa, tutajikuta tunaishi na watu waliokuwa hawaeleweki.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba niingie katika tatizo jengine ambalo pia ni kero nalo ni tatizo la omba omba. Nina masikitiko makubwa mno ya suala hili la omba omba lilivyoingia ndani ya nchi yetu. Katika silka zetu za Kizanzibari ilikuwa hamna mambo haya. Ni ajabu kwa sababu kuwa Wazanzibari tunaongoza kwa omba omba. Omba omba hao ukitizama asilimia kubwa ni wanawake, inasikitisha na inatisha.

Kuna watu wengine kuomba ni tabia yao, suala linalotusikitisha kuna watoto wa kike wenye umri mdogo wana nguvu za kufanya kazi, wazuri wa sura ukiwaona huamini, lakini wanapita mitaani na kuomba omba. Hili ni tatizo na inatakiwa wizara ijitahidi kutafuta ufumbuzi wa kina. Ingawaje wizara ina mipango mingi ya kuandaa sera za hifadhi ya jamii pengine kwa imani yangu naona hiyo itatusaidia. Kabla ya Sera kufanya kazi naomba wizara kupitia serikali kwa jumla ichukue jitihada za makusudi. Itoe adhabu za kutisha na kila aina ya mambo ilimradi hawa wanaopita wakiomba omba wakijulikana hasa kama ni vijana wenye umri mdogo na uwezo wa kufanya kazi wanao, wahifadhiwe Mhe. Mwenyekiti, wanatutia aibu na wanalitia aibu taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niipongeze wizara kwa kuchukua juhudi za makusudi kuandaa mabaraza ya watoto ili kuwafahamisha watoto kujua haki zao za msingi ikiwemo, elimu, afya na mambo mengine. Mabaraza haya ya watoto yatasaidia kujenga taswira nzuri ndani ya nchi yetu. Lakini katika mabaraza haya ya watoto katika Kamati yangu tulipotembelea mabaraza haya ya watoto tumeona kuna changamoto nyingi. Changamoto ya kwanza haya mabaraza wametakiwa wale watoto wapate pahala pazuri pa kukaa na kujadili shughuli zao. Lakini kwa bahati mabaraza yote tuliyoyatembelea hayana maeneo mahsusi ya kukaa hasa na kufanya shughuli zao.

Pili tuliona hawa watoto kwa nia zao safi na ni watoto wadogo wadogo, wameamua kutaka kuwasaidia wenzao wale wanaoishi katika mazingira magumu, na wengine walioacha kwenda skuli kwa sababu moja au nyengine, pengine hawana *uniform*, maradhi na sababu nyenginezo. Sasa hawa watoto wenyewe wanajipigisha mchango shilingi mia mbili kila siku kwa ajili ya kuwasaidia wenzao wale.

Namuomba Mhe. Waziri kwa sababu hawa ni watoto wadogo, ile pesa wanayopewa pengine kwa matumizi ya nyumbani wanajihini kwa ajili ya kuwasaidia wenzao. Naiomba wizara iandae mfuko maalum wa kuwasaidia watoto hawa. Pia wawaandalie mafunzo maalum wale watoto, wawaandalie angalau safari na mipango ili kubadilishana mawazo na watoto katika maeneo mengine kwa sababu haya mabaraza ya watoto hapo si Zanzibar tu, haya yapo kitaifa na nchi zote yamo na tunaona na shughuli zao na yanakwenda vizuri. Watoto wale ndio wanaojifunza baadaye ndio watakaokuja kuwa mawaziri na maspika.

Mhe. Mwenyekiti, wale watoto katika kuwaandaa vizuri naomba Mhe. Waziri ulichukulie uzito wa aina yake. Hawa watoto kwa sababu wamejitolea wenyewe kufanya shughuli zao kuwasaidia wenzao wanaoishi katika mazingira magumu. Wameshaanza kuwarudisha vijana wengi, wanawasaidia madaktari, wanawasaidia *uniform* za skuli, kwa hivyo hawa lazima muwaangalie vizuri, mkiwaandalia visafari angalau kwenda kusoma katika maeneo mengine na wao wenzao wanafanya nini na wao watafanya mambo makubwa ndani ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba nizungumzie suala moja, kwa sababu suala la Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Vijana katika kisiwa cha Pemba ina tatizo kubwa na Ofisi. Bila ya kuwa na Ofisi ya kujulikana ya kutulia mnashindwa kufanya shughuli zetu kwa umakini, hili ni tatizo. Mheshimiwa kwa taarifa tulizozipata wanakodi nyumba hawa kwa mwaka shilingi milioni 18. Pesa hizi nyingi zinazotoka kwa ajili ya kukodi nyumba na katika ufuatiliaji wake tulisikia kwamba kuna azma ya kushirikiana wizara tatu. Wizara ya Uwezeshaji, Wizara ya Fedha na Wizara ya Vijana, Wanawake na Watoto, ili kujenga jengo la pamoja, kiwanja tayari kipo. Nimuulize Mhe. Waziri ni lini azma hii ya kujenga ofisi hii au nyumba hii itatekelezwa ili kupunguza hii idadi ya pesa nyingi zinazotumika kwa kukodi nyumba kwa milioni 18 kwa mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri amezungumza katika hotuba yake kaunda timu maalum za kupita katika maeneo, kusimamia shughuli za udhalilishaji usifanyike. Hapa kidogo nimepata mshtuko, kwa sababu timu zote hizi zinaonekana zipo mkoa mmoja tu wa Kusini Pemba na hili suala la

udhalilishaji lipo katika Zanzibar nzima. Sasa je, katika hizi Wilaya nyengine au Mikoa mengine utafanya lini timu hizi nazo kusikusanya ili na wao hili suala waanze kulifuatilia mapema ili tupate kuliondoa tatizo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye kiambatanisho kuna SACCOS kuna vikundi vya Wanawake je, vilitembelewa kuanzia mwaka gani na mwaka maana kuna vikundi vingi. Hebu naomba kidogo Mhe. Waziri hapa anifafanulie. Sina tatizo na hili, lakini naomba anifafanulie katika viambatanisho hivi kuhusu hizi SACCOS zilizotembelewa. Kwa sababu hii ni Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana na Wanawake. Lakini SACCOS hizi nyingi zipo kwa upande wa Wanawake na Vijana kuna kuchonga na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, hawa wazee wetu nao kwa sababu hii wizara yako inasimamia watu wote na hawa nao wamefikiriwa nini angalau kuwatembelea ukawasaidia, mbali na wale wazee waliokuwepo Sebleni na waliokuwepo Limbani na wazee waliokuwepo Welezo. Kuna wazee wengine wana hali ngumu za maisha nao ni wazee wetu. Ni lini nao hawa utawafanyia tathmini na kuwajua kama ni wangapi na kuwasaidia katika maisha yao.

Kwa kumalizia Mhe. Mwenyekiti, naomba niiunge mkono bajeti hii asilimia mia moja.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunitanabahisha na pia nikushukuru kwa kunipa fursa hii. Pia nimshukuru Mhe. Waziri wa Wizara ya Ustawi wa Jamii Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto. Kwa kweli hotuba hii ina mambo mengi kama unavyojua Mhe. Mwenyekiti, Wizara hii ni nzito na ina majukumu mazito kabisa. Wizara hii imebeba vijana, wanawake, wazee, pamoja na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, kama nitazipanga kwa foleni basi baada ya Wizara ya Elimu mngeipanga Wizara ya Wanawake na Watoto na baadaye ikafuatia Wizara nyengine. Wizara hii muhimu lakini kwenye jambo lolote ni lazima changamoto ziwepo. Tumeona wizara hii kwa sababu inabeba watoto, wanawake, wazee na vijana. lazima changamoto ziwepo.

Nikienda kwenye wezee, tunashukuru Mhe. Waziri ametuonesha katika sehemu mbali mbali namna gani anavyowatunza wazee na sisi tunaona. Kwa sababu sio kama anasema tu lakini na mambo mengi tunayaona ambayo anayatekeleza. Juzi tu tulikuwa kwenye semina nashukuru kwamba katuandalia semina ya sera ambayo itakuja baadae kuja kwetu sisi na kuipitisha.

Nawaomba Waheshimiwa wenzangu itakapokuja basi tuipitishe kwa nguvu zote ikija sheria hiyo ya kuanzisha pencheni jamii. Kwa sababu inaonekana kwamba kuna umuhimu wa kuanzisha pencheni jamii ambayo sasa itamuhusu kila mtu anayefikia umri wa miaka 60 aweze kupata pencheni hiyo. Haijulishi kwamba alikuwa mfanyakazi au ni nani inajumuisha kwamba wazee wote watakaofikia umri wa miaka 60 basi anastahiki kupewa pencheni jamii na kutokana na sababu hata kama hakuwa na sekta maalum basi atakuwa analipa kodi mbali mbali.

Hili ni jambo la faraja na jambo ambalo kwa upande wetu sisi Zanzibar niseme ni jambo la kujivunia. Mambo mengi tunaanzisha na katika nchi za Afrika basi Zanzibar ni ya mwanzo ambayo imeanza kuwahifadhi wazee. Kwa hivyo hili namshukuru sana Mhe. Waziri kuliendeleza. Limeanza tokea kwa Mheshimiwa wetu muasisi wa Serikali ya Mapinduzi, Mheshimiwa Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema kwa yale mengi ambayo ametufanyia katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda na hotuba hii Waziri amesema kwamba utafiti umefanywa na kuonekana kwamba omba omba wamezidi. Kati ya miaka 40 - 60 na wengi ni wanawake. Mimi nakubaliana na Mhe. Waziri kuhusu hili kwamba wanawake ni wengi omba omba kwa sababu tuna majukumu mengi na hasa pale tunapoachika wenzetu wanatuachia ulezi. Kwa kuwa tunataka kuishi na watoto wetu basi kadhia hii hutukuta sisi wanawake ambao tunakuwa omba omba wengi.

Mimi nimuombe tu Mhe. Waziri kwamba sasa umefika wakati wa kujipiga vifua ili kuwasaidia wanawake hawa kwenye vikundi vya Ujasiri Amali ili waweze kujikomboa katika matatizo mengi.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile katika hotuba yake sehemu mbali mbali alielezea kuhusu unyanyaswaji wa kijinsia kwa watoto na wanawake. Kwa kweli suala hili limekuwa likiendelea kwa muda mrefu na linapigiwa kelele sana lakini bado hatujaona yale mafanikio hasa ya kuondoa matatizo haya. Kwa sababu kesi tunazijua ni nyingi ambazo ziko zina mrundikano na wala hatuoni hatua zinazochukuliwa kwenye matatizo haya na bado yanaongezeka siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, niseme hasa katika kudhalilisha watoto kama wanaume ikiwa ni wanawake mtu kumfanyisha jambo kama alivyosema mwenzangu kabla ya umri wake kwa kweli unamsababishia maumivu na matatizo. Mimi niseme sasa serikali ichukue juhudi ya kutafuta jambo litakalowafanya watu wakome na jambo hili. Kwa sababu tunaona bado hawajadhibitiwa hawa watu, serikali bado haijachukua mkondo wake hasa. Sioni sababu kwamba mtoto mdogo watu wenye kazi zao wapo, si mfuate tu uliyekuwa unamuona

kwamba huyu mimi wala sitofedheheka, kumchukua mtoto mdogo kwa kweli ukamfanyia vitendo ambavyo havieleweki na hasa watoto wanaume. Kama wewe ni mtu unayependa liwati basi kwa nini usimtafute yule atakayekubali mwenyewe laana na Mwenyezi Mungu atakwenda kumuhukumu huko.

Lakini kumchukua mtoto wa mwenzio mdogo ukamfanyia suala lile kweli wewe unamtendea haki mtoto yule? Au wewe kweli ni mzazi? Kama ni mzazi kweli huoni kwamba hili ni suala zito na gumu kumfanyia mtoto wa mwenzio? Kwa hivyo haya naomba Mhe. Waziri utakapokuja utupe hasa ni adhabu gani ambayo mpaka sasa hivi itachukuliwa kuhusu watu hawa.

Mhe. Mwenyekiti vile vile niende kwenye suala la Mhe. Waziri ametwambia kwamba anafuatilia kuhusu habari hii ya wanaoumia kazini kwa kushirikiana pamoja na Ofisi ya Rais Fedha na Uchumi. Mimi nimshukuru sana kwa kuwa ninajua kwamba yeye ni mama na ana uchungu sana na mwanamke siku zote ukitaka mambo yaende vizuri basi ni lazima umpe jukumu mwanamke analichukua kwa kilillahi, kwamba anajua kuwa na yeye ni mzazi kama ni yeye analenga kote kwamba anajua kuwa siku moja na yeye yatamkuta kama yale. Na ni lazima kila binaadamu ajue kwamba kila linalomkuta mwenziwe basi ujue na wewe kuna siku litakukuta na lazima ujihadhari nalo na vile vile uliwekee mikakati.

Kwa hivyo hapa mimi ninamshukuru Mhe. Waziri kwa kuchukua juhudi hiyo na ni lazima zile Wizara basi ziwe na *coordination* ili kusaidiana kufanikisha, kwa sababu watu wamesema *kidole kimoja hakivunji chawa*. Kwa hivyo ni lazima wizara na wizara zikae pamoja ili kuona kwamba yale malengo ambayo wameyakusudia basi yawepo kwa pamoja.

Vile vile Mhe. Waziri nina dukuduku langu kwa siku nyingi. Kama tukiwa wanasiasa tuna mambo chungunzima ambayo tumeji-*commit* kwa watu na ni lazima tuyatekeleze. Katika eneo langu kuna tatizo la maji kusema kweli kwa muda mrefu na tuna eneo ambalo tumekaa na wenzetu Mamlaka ya Maji na wametwambia tukichimba kisima hapo tutapata maji ambayo yatatosheleza kwa maeneo yetu. Maeneo hayo ni matatu likiwemo Jimbo la jirani yangu Mhe. Salmin Awadh vile vile Jimbo la Mhe. Ali Salum pamoja na Jimbo langu la Amani katika shehia ya Sebleni, kuna mradi ambao unaitwa SEMUSO, kwa hivyo hapa kusema kweli kuna kitu labda utasema ushindani siwezi kusema ni ushindani, na sisi kama serikali pamoja na sisi wanasiasa ni lazima tuwe tunashirikiana pamoja ili kuondosha haya matatizo.

Kwa kweli kumetokezea mambo kidogo ya kwamba hapafahamiki, na kwa sababu hii ni miradi ya wananchi na wewe Waziri nakuona kwamba ni mtu ambaye ni muwajibikaji ingawaje hili suala nimekuletea na

tumeshalizungumza na umenambia nikungojee kidogo, nina hakika kwamba suala hili utalichukulia kwa uzito mkubwa na unaweza ukanisaidia.

Ukija kunielezea suala hilo nitafurahi sana baada ya hayo niseme kwamba bajeti sina matatizo nayo, na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani naunga mkono mia kwa mia.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto. Napenda kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Waziri bi Zainab na watendaji wake wote kwa kuandaa hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti pia niipongeze serikali kwa dhati kabisa kwa jitihada mbali mbali ambazo wanazichukua kuwaletea maendeleo wananchi wake. Mimi nitachangia katika maeneo ya mabaraza ya watoto, mapitio ya sera, utoaji wa mikopo kwa vijana, vituo vya mkono kwa mkono na suala zima la omba omba.

Mhe. Mwenyekiti kitabu cha hotuba ukurasa wa 8 kifungu cha 15 kimeelezea suala zima la ombaomba. Suala la ombaomba hapa Zanzibar Mhe. Mwenyekiti linaongezeka siku hadi siku na niipongeze Wizara kwa kufanya utafiti ili kuona kwamba ni sababu gani ambazo zinapelekea kuongezeka suala la ombaomba hapa Zanzibar. Na matokeo ya utafiti yameonesha katika kitabu cha hotuba hii asilimia 65 ni wanawake na asilimia 35 ni wanaume. Na changamoto ambazo zinapelekea kutokea tatizo hilo la ombaomba ni suala la mazingira magumu, ukosefu wa elimu pamoja na ukosefu wa ajira.

Hapa Mhe. Mwenyekiti mimi nilikuwa na ushauri tu kwa wizara kwa kushirikiana na wizara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ipange mipango madhubuti ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu hawa. Kwa sababu hawa ni wazee wetu, ni dada zetu ni watoto wetu hawafanyi hivyo kwa kutaka, bali ni changamoto za maisha. Kuna wengine ni kama tabia kuomba lakini kuna wengine kwa kweli wana hali ngumu pengine elimu yao ni ndogo, lakini serikali ikishirikiana na Wizara ya Uwezeshaji Kiuchumi iweze kuwasaidia watu hao kwa sababu ni miongoni mwa jamii yetu.

Nitakwenda kwenye mabaraza ya watoto hii ipo katika ukurasa wa 47 kifungu 103. Mabaraza yameundwa ili kuona kwamba watoto wanapata fursa kujadili haki zao za kimsingi ikiwa ni pamoja na kupata mazungumzo ya kubadilishana mawazo mbali mbali kujadili changamoto ambazo wanazipata zikiwemo unyanyasaji pamoja na udhalilishaji. Hapa pia nilikuwa nina ushauri.

Mhe. Mwenyekiti, mabaraza 55 ya shehia za Unguja na mabaraza 4 kwa shehia za Pemba yameundwa kwa shehia ambazo zimepatiwa mafunzo kama shehia sita. Hapa nilikuwa namshauri Mhe. Waziri shehia sita walizopata mafunzo hazitoshi, kwa sababu mabaraza ni mengi na hawa wanajengewa uwezo vijana wetu, watoto wetu kuwa wajasiri kupambana na mambo ambayo ni magumu yanayoweza kuwakabili. Kwa hivyo nilikuwa nashauri katika sheria nyengine kupatiwa mafunzo hayo na kuwajengea uwezo zaidi.

Mhe. Mwenyekiti nakwenda katika mapitio ya sera ya uhai, hifadhi, na maendeleo ya mama na motto. Kwanza hapa pia naipongeza wizara kwa hatua ya kutayarisha sera hii, sera hii maalum itasaidia kuwahudumia makundi mbali yakiwemo walemavu, watoto wenye mazingira magumu, watoto mayatima. Hapa Mhe. Mwenyekiti nilikuwa na msisitizo tu, sera hii ilenge hasa kwa wale wahusika ambao ni makundi maalum na si vyenginevyo.

Nakwenda katika utoaji wa mikopo kwa vijana ipo katika ukurasa 34 kifungu cha 76. Hapa pia napenda kuipongeza serikali kwa dhati kabisa kwa hatua hii ya kuwajali vijana wetu, vijana ambao baadhi yao walikuwa wameshakata tamaa na maisha, mikopo hiyo itawasaidia hasa vijana kujiepusha kujiingiza katika mambo ambayo hayatoweza kuwapeleka mbele katika maisha yao. Na takwimu zimeonesha jumla ya milioni 308 zimetolewa kwa wanachama 540 ambapo wanawake 338 wanaume 202 na vikundi 31 ambavyo vimekabidhiwa shilingi milioni 117700 kwa Pemba. Ni hatua nzuri inastahili sifa.

Hapa ninatoa indhari tu Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kulikuwa na mfuko wa AK na JK, na mfuko huu ulikuwa na nia nzuri tu kuwasaidia wananchi wetu SACCOS ili wajiendeleze kimaisha. Lakini kwa bahati mbaya wananchi wengi walichukulia ule mfuko pesa zile kama ni zawadi au kama wamepewa tu, na matokeo yake wananchi wengi hawajarudisha mikopo ile, mikopo ambayo ingerudishwa ingeweza kusaidia hata wananchi wengine kupata ili kujiendeleza katika miradi midogo midogo. Sasa hapa nilikuwa na swali nimuulize Mhe. Waziri ni mikakati gani ambayo ameweka ili fedha hizi zirudishwe na wengine waweze kufaidika.

Nakwenda katika kituo cha mkono kwa mkono hiki kipo katika ukurasa wa 25 na hapa pia naipongeza wizara. Wizara imefanya kazi nzuri kwa kweli, naipongeza wizara kwa kuweza kuvihudumia vituo hivi na imesema hadi mwezi Aprili 2013 jumla ya kesi 1500 za udhalilishaji za watoto ziliripotiwa na kushughulikiwa katika vituo vya mkono kwa mkono Unguja na Pemba. Kwa mujibu wa takwimu inaonesha kwamba kesi za kubakwa ni nyingi zaidi kwa wanawake ambapo imeonesha wanawake 480 wamebakwa. Kesi za mimba 176, kulawitiwi 53; hili ni tatizo tena ni tatizo kubwa, kesi hizi ndio

zimeripotiwa pengine kuna nyengine zaidi ya hizi ambazo hazijaripotiwa, kwa sababu kuna kama tunavyojua jamii ndio sisi sisi. Kuna wengine wanafanyiwa vitendo hivi lakini hawaripoti wanaona wakiripoti pengine watapata aibu, fedheha. Lakini hapa nilikuwa nasisitiza wizara izidi kutoa elimu kwa wananchi, kwa vijana kupitia mabaraza hayo ya watoto, na pia serikali kupitia taasisi husika isiwavumilie wale wote ambao wanafanya vitendo hivi viovu wachukuliwe hatua ili iwe kama funzo kwa wengine.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti naunga mkono hoja. Ahsante.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kabla ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kufika hapa katika hali ya uzima. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti naomba uniruhusu niseme mawili nimuombe Mwenyezi Mungu atujaalie tufunge Ramadhani hii kwa kheri, baraka, atuondolee maradhi, atuondolee uadui ili kuweza kuhitimisha Ramadhan tukufu.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti na mimi kwanza nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote ambao kwa kweli kwa namna moja au nyengine wamemsaidia, na yeye mwenyewe akiwa ni mzoefu katika mambo haya si mgeni wa mambo haya ya wanawake, lakini kwa kweli nitoe pongezi za dhati kwa kitabu hiki ambacho kimejipanga na kimepangwa na kimepangika.

Lakini pia nichukue nafasi hii Mhe. Mwenyekiti nimpongeze Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuona umuhimu wa Wizara hii, kwa kweli ametupa matumaini makubwa na niwaombe wanawake wenzangu tupokee matumaini haya ya Mhe. Rais kwa kuweza kutuona kwamba mwanamke ni muhimili mkuu katika taifa na katika jamii. Kwa hivyo niseme tu tunamshukuru na tumuombe Mhe. Waziri atupelekee salamu zetu kwa Mheshimiwa Rais kwamba tunamshukuru sana kwa kutujali.

Lakini Mhe. Mwenyekiti na mimi nipitie mule mule ambamo wenzangu wamepitia. Kwanza suala la ombaomba Mhe. Mwenyekiti. Suala la ombaomba kwa kweli katika nchi yetu halileti taswira nzuri na sijui linatokea wapi suala hili, kwa sababu suala hili hatukuwa nalo hapa Zanzibar la ombaomba si kwa watoto wala si kwa wanawake, ninamuomba Mhe. Waziri kwa kweli tulifuatilie suala hili na wala tusilipe mwanya kwa sababu litatuletea sura mbaya katika nchi yetu ya Zanzibar.

Kwa nini nikasema hivyo Mhe. Mwenyekiti, siku hizi limeshamiri basi ngojea huu mwezi wa Ramadhan kweli watu wanakwenda futari lakini si vizuri kufanya mambo ambayo kwa kweli yanatufedhehesha hasa sisi wanawake.

Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri kwamba hii ombaomba tuifuatilie na sisi tutajitahidi kushirikiana na wewe kuhakikisha kwamba ombaomba hapa haipo.

Lakini kubwa niseme pia kwamba nije katika udhalilishaji wa watoto. Mhe. Mwenyekiti suala hilo tunalipigia kelele sana tena sana, lakini sasa mtindo mwengine mkubwa zaidi ukiacha watoto wa kike sasa mtindo mkubwa wanabakwa watoto wa kiume, ninasikitika sana na wanaofanya ni watu wenye akili zao. Mtu anajisahau kama na yeye anazaa, watu wanasema *mla kuku wa mwenziwe miguu humuelekea*. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti mimi hili namomba Mhe. Waziri kama kuna tatizo la sheria, kama kuna tatizo la aina yoyote basi tufanye siku hasa tukutane akina mama tulizungumze suala hili jinsi wanavyotudhalilishia vijana wetu na jinsi wanavyodhalilisha watoto wa kiume hakuna sumile mtoto wa miaka 4, mtoto wa miaka 3, mtoto wa miaka 6 na mtoto wa miaka 18 au 15.

Kwa hivyo mimi ninamuomba sana Mhe. Waziri tuko pamoja na wewe kwa suala hili, hatutokubali kabisa taifa la leo kudhalilishwa kwa sababu kwanza Mhe. Mwenyekiti Wizara hii ni wizara nyeti. Wizara hii Mhe. Mwenyekiti ndio iliyozaa ulimwengu. Wizara hii Mhe. Mwenyekiti ndio iliozaa Marais wa ulimwengu wote, Wizara hii ndio iliozaa Mawaziri wa ulimwengu wote. Sasa mimi nashagaa kwamba wizara hii kwa kweli kwanza nimeshtushwa mimi kuambiwa saa sita tumpe Mhe. Waziri atujibu kwa kweli ninasikitika. Kwa sababu wizara hii ni wizara nyeti tungeipa kipaumbele cha hali ya juu wizara hii Mhe. Mwenyekiti naomba sana, yale yote ambayo tunahisi tumsaidie Mhe. Waziri mwenzetu wa kike ambaye ataweza kuhakikisha kwamba tuko pamoja naye tumsaidie kwa hali na mali kuhakikisha mambo mengine ambayo yanadhalilisha nchi yetu tusiyaachie na wala tusiyakubali.

Mhe. Mwenyekiti kuna baadhi ya mambo ambayo yanatendeka na mimi siridhiki nayo, utaona watu wanapita vijumbani madukani, mtoto kijana kama alivyosema Mhe. Farida mtoto mzuri, mtoto ukimuona hana safura, mtoto ukimuona unajua huyu anaweza akaingia kondeni akalima, lakini sasa linalonisikitisha ni kwamba sijui ni sababu zipi ambazo zinamfanya yeye apite majumbani kuombaomba.

Si hilo tu ombaomba yake utamkuta ana mtoto mmoja kabeba mgongoni na mwengine ana mimba, sasa wewe kama kweli unataka kujihakikishia maisha yako kwa nini tena wajane mimi samahani nitasema kidogo wajane hao. Sasa kwa nini umetoka nyumbani Kijijini unasema unakwenda kutafuta maisha mjini, mjini kuna maisha kuna tabu? Kwa sababu kijijini kule unapata sehemu unalima, unajenga kibanda chako unakaa unakula na wanao huku mjini hapana pa kulima na ndio maana ikazuka hii ombaomba Mhe. Mwenyekiti.

Mimi kwa kweli nitakusaidia Mhe. Waziri nitakusaidia sana maana ninawaona mimi watu wanaomba hasa sokoni, marikiti huko aibu. Kwa hivyo mimi nadhani japo kijikanuni kidogo kidogo hivi cha ombaomba uwezo huo Waziri unao, au tufanye sheria hasa ya ombaomba kwa sababu kanuni tutakuwa tunachezacheza lakini tufanye sheria hasa ya ombaomba iondoke.

Niseme Mhe. Mwenyekiti nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na Wizara yake na watendaji wake kwa jinsi anavyowanufaisha kinamama katika vikundi mbali mbali lakini pia hata vijana ambao kwa kweli wananufaika, na ndio maana nikasema tupelekee salamu zetu kwa Mhe. Rais kwa mambo ambayo anatusaidia sana katika Wizara hii.

Kwa sababu umesema Mhe. Mwenyekiti tutumie wakati mdogo niseme tu kwamba ninaiunga mkono hoja ya Wizara hii mia kwa mia.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kunijaalia kuweza kuchangia hotuba hii. Kabla sijachangia Mhe. Mwenyekiti mimi naomba kuunga mkono hotuba hii mia kwa mia. Pili nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa hotuba hii ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto kwa mwaka wa fedha 2013/2014 hotuba hii nzuri itakayotuletea mafanikio.

Mhe. Mwenyekiti na mimi nianze kwenye kundi la ombaomba, tatizo hili ni kubwa ikiwa mimi ni Mjumbe wa kamati hii kusema kweli linatusikitisha sana hasa kwa upande wa wanawake. Mhe. Mwenyekiti mimi ninaipongeza Wizara kwa kufanya kazi hii kwa makusudi ya kuona kwamba tatizo hizi limelenga sana kuhusu talaka. Mhe. Mwenyekiti ni kweli talaka zimekuwa nyingi ndio maana wanawake tumekuwa wengi kutokana na matatizo yetu.

Mhe. Mwenyekiti nije katika ukurasa wa 25 kuhusu kituo cha mkono kwa mkono. Mhe. Mwenyekiti niipongeze Wizara pamoja na *Save the Children* kwa kusimamia vizuri vituo hivi pamoja na mafunzo wanaowapa watendaji wao. Mhe. Mwenyekiti ni kweli Wizara hii vituo hivi inasimamia vizuri na tulipoenda katika vituo hivi tumekuta ni kweli kazi wanafanya Wizara ya Ustawi wa Jamii kupitia watendaji wake. Lakini tatizo lililokuwepo askari na mahkama naona bado hawajakuwa tayari, kwa sababu kama Wizara imejitahidi kusema kweli kuchukua hatua ya kuweka vituo hivi na kuhamasisha wanawake au jamii kwenda katika vituo hivi na kazi hii inafanywa vizuri sana. Lakini inafika wakati baada ya kupelekewa kesi kwenda katika vituo vyengine mfano polisi au mahkama hii wizara inakuwa imefikia mwisho wake haiwezi kuingilia katika mamlaka hii nyengine.

Lakini tukiangalia hivi vitengo viwili vilivyokuwa vimebakia vya polisi na mahkama havijakuwa tayari kufanya hii kazi, kwa sababu tuseme hii wizara baada ya kuona iweke vituo hivi na watu kuhamasika kwenda katika hivi vituo, lakini wananchi baada ya kuona kesi zao haziendi inaonesha hii itarejesha nyuma wanawake, baada ya kwenda kule katika vile vituo itakuwa haiendi kwa sababu ndio kesi haiendi. Sasa ninaiomba serikali kuu ilisimamie kushirikiana na wizara. Wizara imejitahidi lakini tuseme serikali kuu nayo itie mkono wake kesi haziendi, watoto wanazidi kubakwa. Kila asubuhi tukiamka kwenye mawio mtoto wa miaka 3 yaani maana yake inatia uchungu kusema kweli haipendezi. Kwa hivyo serikali kwa makusudi mihimili hii miwili polisi na mahkama kama Wizara kwenye vituo vya mkono kwa mkono imejitahidi na inajitahidi.

Mhe. Mwenyekiti nije kwenye mabaraza ya watoto, mabaraza haya mimi mwenyewe nimeyaona na watoto hawa nimewaona, kusema kweli kama wizara mimi naipongeza pamoja na masheha wamefanya kazi nzuri kwa sababu mpaka ukawakusanya wakawa kitu kimoja wakawa wanapendana, naamini Wizara imefanya kazi kubwa, lakini ina matatizo watoto hawa hawana sehemu za kukutana. Kusema kweli kule tulipokuwa tumeenda kutembelea tunakuta wanaazima kwenye madrasa watoto hawaendi chuoni ndio wao waazimwe.

Kwa hivyo ninaiomba wizara isimamie vizuri hawa watoto wakutane katika maeneo yaliyokuwa ya uhakika kwa sababu hawa watoto wanafanya kazi nzuri na tunategemea kuwa hawa watoto watakuwa taifa la kesho.

Mhe. Mwenyekiti niende kwenye utoaji wa mikopo kwa vijana. Mheshimiwa niipongeze Wizara kwa kusimamia vizuri vijana kujiunga na vikundi vya ujasiri amali kwa lengo la kujishughulisha na kazi mbali mbali ambazo zitaiingizia kipato, na pia kujipatia mikopo ya kuendelea na shughuli zao. Mheshimiwa hapa Wizara pia ilijitahidi mimi mwenyewe nimeona tumekwenda kwenye vikundi, tumeona wanapewa mikopo na baadhi ya vikundi wanarejesha vizuri.

Pia Mhe. Mwenyekiti niende kwenye uanzishwaji wa benki ya wanawake. Mhe. Mwenyekiti suala hili sijui nimesimama mara ya pili au mara ya tatu kuliulizia kusema kweli kama Wizara imejitahidi lakini sasa ninaiomba Wizara ya Fedha hili suala hili walisimamie kwa sababu wenzetu Tanzania Bara wanafaidika lakini sisi wanawake wa Zanzibar bado hatujafaidika na hii benki. Kwa hivyo ninaiomba tena Wizara ya Fedha ilichukue hili suala ilifanyie kazi ili na sisi wanawake wa Zanzibar tufaidike na benki hizi.

Mhe. Mwenyekiti nije kwenye fidia. Mhe. Mwenyekiti tatizo hili la fidia la wafanyakazi ni kubwa kila siku linaongezeka. Kusema kweli kama Wizara ya Wanawake na Watoto hili suala sasa hawaliwezi tena, sasa naiomba pia Wizara ya Fedha suala hili walichukue walifanyie kazi haraka kwa sababu linazidi, kila siku tukiendelea linazidi. Na mimi nilipata taarifa kuwa Wizara ya Fedha wameshaanza kulifanyia kazi lakini wazidishe jitihada kwa sababu hili suala ni kubwa na kila tukikaa madeni yanaongezeka.

Mhe. Mwenyekiti kwa vile umesema muda na tuko wengi wa kuchangia, basi mwisho kwa niaba ya wanawake wa mkoa wa Mjini Magharibi naunga mkono tena mia juu ya mia.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, *Bismillahi Rahmani Rahiim*. Awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu si tu kwa kutuamsha tukiwa hai na wazima tukaendelea na shughuli zetu hapa, lakini pia kwa kutujaalia kuudiriki Mwezi Mtukufu wa Ramadhan kwa mara nyengine tena. Nichukue nafasi hii kuwaombe hususan raia wenzetu wa Zanzibar *inshallah* tuufunge vyema mwezi mtukufu wa Ramadhan na Mwenyezi Mungu ajaalie alete baraka na neema kwetu sote na aujaalie uzidishe mapenzi na umoja miongoni mwetu katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia machache sana katika Wizara hii ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo na Vijana, Wanawake na Watoto. Mhe. Mwenyekiti, nampongeza Mhe. Waziri, mama yangu mpenzi Mhe. Zainab Omar Mohammed, ambaye kwa jinsi alivyo na huruma zake ni mtu sahihi kabisa kupewa kuiongoza Wizara hii. Mimi nilibahatika kuwa na Mhe. Zainab katika Kamati ya Kutafuta Muafaka wa Tatu uliokwama kule Bagamoyo, lakini tulipata muda mrefu wa kuwa pamoja, najua jinsi alivyokuwa mama mwenye huruma.

Mhe. Wenyekiti, sasa nikiingia katika hotuba ya bajeti hii naomba kwanza nianze na ukurasa wa 37 kuhusiana na suala la Baraza la Vijana Zanzibar. Suala hili limekuwa linazungumzwa kwa muda mrefu sana, sijui kama haitimii miaka kumi. Kwa sababu ninavyokumbuka mimi tangu mwanzo mwanzo ulipokuja mfumo wa vyama vingi ilipozungumzwa kwamba Jumuiya za Vijana zilikuwepo za vyama vya siasa vitawagawa vijana katika makundi ya kiitikadi pakaonekana kuwe na haja ya kuwa na chombo cha pamoja ambacho kinawaunganisha vijana wote, ili kusimamia maslahi yao ya pamoja, limezungumzwa muda mrefu. Lakini tangu Baraza hili lichaguliwe katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 lilikuwa likihimizwa sana na Baraza hili na mmoja ninataka nimpongeze sana mimi ambaye ni msemaji mkubwa wa suala hili ni Mhe. Wanu Hafidh Ameir.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ninasikitika kidogo kwamba bado nikisoma katika ukurasa wa 37 maelezo yaliyomo ni kwamba bado utaratibu unaendelea tu kwamba wameshirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuandaa waraka, na mswaada wa Baraza la Vijana umepelekwa katika Kamati ya Makatibu Wakuu na baada ya hapo inafanyiwa, sasa unaandaliwa mswada mwengine. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nadhani naomba Wizara ikija itusaidie hapa, suala hili litamalizimika lini na mswada huu wa Baraza la Vijana lini utaletwa na linakuwa kila siku uko katika hatua za kiutawala tu huko ambazo hazimaliziki.

La pili Mhe. Mwenyekiti, ni nasaha ndogo tu. Katika ukurasa wa 40, pamezungumziwa suala la watoto na hususan imesema Wizara inaendelea na kuratibu utekelezaji wa sera na sheria ya mtoto, ambapo tathmini ya utendaji kazi wa mfumo wa kisheria zinazohusu watoto Zanzibar imefanyika na taarifa yake imejadiliwa na wahusika wa sekta ya sheria. Lakini halafu katika ukurasa wa 41 pakatajwa kanuni mbali mbali ambazo zinaandaliwa wamesema ni saba katika kutekeleza sheria ya mtoto, sitaki kuzikariri lakini ninataka nimkumbushe tu kidogo Mhe. Zainab kwamba tulipokuwa tukijadili sheria ya mtoto tulizungumza sana suala la kutofautisha kati ya kuwasili na ule utaratibu uliozoeleka katika nchi yetu kutokana na utamaduni wa kiislamu wa namna gani ya kulea watoto kwa dhamana aliyopewa.

Mhe. Mwenyekiti, haidhuru katika sheria za kiislamu utaratibu ule umewekwa vizuri, lakini ilikuwa nadhani katika hizi kanuni zake ingelikuwa vizuri mwenyewe kukaa na nakumbuka sheria ya mtoto ilikuwa kuna sehemu inayohusu utaratibu ule, sasa nadhani ingekuwa vizuri ule utaratibu wa kiislamu unaoeleweka ule ukawekewa kanuni vile vile nao wangekaa na Mashekh na Wataalamu wa fani ya sheria ya kiislamu ikaandikwa vizuri ili ikawa badala ya kila mtu kuwa na tafsiri yake kukawa kuna kanuni ambayo imekubaliwa kwa pamoja na maulamaa wetu hapa likaongozwa suala lile kama vile ambavyo wametengeneza kanuni kama wanavyotueleza hapa kuhusu kuwasili, nilikuwa naomba hili litazamwe.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nilikuwa nataka kusisitiza tena hapa, na nilisisitiza sana siku ile nilipokuwa nikijadili mswada wa sheria ile kabla ya haijawa sheria ya haki za mtoto. Suala la kutokuwa tayari kukubali kufuata tu masharti tu na matakwa ya mashirika ya maendeleo katika masuala yanayohusu haki mbali mbali za kijamii katika nchi zetu. Mara nyengine kumekuwa na utamaduni wa kutaka kutulazimisha kunakili yale yaliyokuwa yao ambayo hayaendani na maadili yetu, mila zetu, silka zetu. Kwa hiyo nilikuwa naomba hata katika utekelezaji wa sheria ya mtoto bado hili lizingatiwe.

Mhe. Mwenyekiti, atakumbuka Mhe. Waziri, tulisema katika mila zetu hapa suala la kwamba huwezi kumrudi mtoto halikubaliki katika jamii zetu, sote tumeleleka na tunafuata maadili haya kwa sababu wazee wetu, walimu wetu na wengine wote walikuwa na haki ya kuturudi na kutuweka sawa na wengine tulichangia na tukasema kwamba hili muhimu kulitizama kwa sababu hata huko nchi za wenzetu hasa nchi za Magharibi, sasa hivi wenyewe wanapojitathmini wanasema kuna baadhi ya mambo waliyaruhusu yamewaathiri katika malezi ya jamii na familia zao.

Kwa hivyo nilikuwa nasema hili tulitizame tena, isiwe tumejadili siku ile kwa ukali sana hapa lakini katika utekelezaji wa sheria za mtoto tukasahau kwa sababu tu ya ushawishi na nguvu hawa wanaotusaidia mbali tutizame namna gani tunaweza tukalea watoto wetu kwa mila zetu ambapo itatujengea jamii yenye maadili mazuri na jamii njema kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, hapa hapa katika suala ambalo limetajwa hapa katika masuala ya watoto, mimi ninataka kuzungumzia suala la ajira kwa watoto. Inaonekana sasa hivi hasa katika yale maeneo ambayo ukitizama takwimu inaonesha kwamba umasikini umejikita, basi suala la utumikishwaji wa watoto limekuwa linaongezeka sana, baadhi ya maeneo tukipita yanatia huzuni tu utaona watoto wamepewa nyundo wanabanja kokoto.

Katika baadhi ya nchi Mhe. Mwenyekiti, kulitokezea mgogoro mkubwa sana juu ya watoto wanaofanyishwa kazi bidhaa zake zikapelekwa katika nchi za Ulaya, wakaulizwa wale nyinyi mnakuwa hodari wa kupiga kelele katika kutetea haki za watoto, mbona viwanda vyenu vinakwenda kwa mfano ukienda katika nchi kama za India, Bangladesh, Pakistan unakuta watoto wanafumishwa mipira, watoto wanafanyishwa kazi katika mashamba na vitu vingine kama hivi kwamba kwa nini mnafanya hivyo.

Sasa na hapa kwetu haijafika pahala pa kuja nchi za nje, lakini sisi wenyewe kwa sababu ya umasikini familia nyengine zinalazimika kuwafanyisha kazi watoto.Sasa nadhani hili katika zile tafiti wanazozifanya basi walikuwa watusaidie tuone kama Serikali, maana yake ni jukumu lile linaonekana mwisho litakuja kwetu sisi kama wenye dhamana ya uongozi kwamba tunafeli wapi katika kusaidia familia kujikomboa katika umasikini mpaka kulazimisha kutumia watoto wao, kwa sababu sidhani kama kuna mzazi ambaye anapenda kuona watoto wake wanafanya kazi badala ya kwenda skuli akasoma, kama mwengine anakwenda madrasa kama alivyokuwa mwengine. Kwa hiyo mimi nilikuwa nataka alitazame kwa ukaribu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kwa ufupi kabisa nilitaka nizungumzie suala la Ustawi wa Jamii masuala yanayohusu haki za wanawake, wamechangia hapa

na inatia moyo kwamba waliochangia wanaoongoza ni wanawake wenyewe katika mjadala huu, na hii ni Wizara yao kimsingi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka kumuomba Mhe. Waziri na watendaji wake waangalie sana suala linaloendelea hivi sasa, wao katika kuchangia wanawake wengi hapa wamezungumzia suala la kuongezeka kwa talaka, lakini kiasi gani tunalioanisha hili na suala tulilolizungumza sana katika Wizara ya Katiba na Sheria suala la Mahakama zetu hasa za Kadhi kuchangia katika hili, na hapa panakuja vile vile suala la haki ya kuwalea watoto na kuwalinda watoto wale, sijui Wizara inafanya kazi gani kushirikiana na Mahakama za Kadhi katika kufanya utafiti wa pamoja na kuwanasihi katika hili.

Leo tunagundua kuna kesi kwa sababu tu upande fulani una uwezo wa kifedha unapindisha sheria anachukuliwa mtoto anaondolewa kwa mama ambapo sheria zetu zinataka awepo kwa mama, anapelekwa kwa baba, wanaliangalia kiasi gani masuala hayo katika Wizara. Nilikuwa naomba hilo watusaidie vile vile wamejipanga vipi?

La mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, ni suala ambalo kila mtu kalizungumza ni suala la kuongezeka kwa omba omba. Katika ukurasa wa 8 wa hotuba ya Mhe. Waziri, wametaja kwanza takwimu kwamba wengi ni kati ya miaka 40 na 60, halafu katika hawa asilimia 65 ni wanawake na asilimia 35 ni wanaume. Halafu akaelezea miongoni mwa sababu zinazojitokeza katika ufatiti walioufanya ni pamoja na mazingira magumu, kiwango duni cha elimu, ukosefu wa ajira na tabia ya uombaji kwa baadhi yao.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kabla sijachangia nimeletewa *message* katika simu hivi punde tu, wanaotusikiliza katika mjadala huu, wamewasikiliza wale wote humu ndani waliokuwa wanalalamika kwamba omba omba si tabia nzuri, kuna mmoja mwanamke kaniandikia hapa, ananiambia:- "Ikiwa nyinyi kama tuliokupeni dhamana ya kusimamia sera za nchi yetu, mmeshindwa kutuletea sera za kukuza uchumi tukapata ajira na sisi wengine hatuna ajira, hatukusoma, kaandika hatuna waume, kama hatukuomba tufanye nini, mnataka tukazini?" Ninayo *message* Mhe. Mwenyekiti, sitaki kuisoma tu, lakini ujumbe wake ulikuwa ni huu. Sasa kuna mambo inapaswa tuyatazame kwa ujumla wake kabisa katika mambo kama haya.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala moja nilikuwa nataka tuliangalie hapa, wala nikisema hivi isitafsirike vingine, lakini kuna kitu kimoja hatujakiona hapa. Mhe. Mwenyekiti, pametajwa hapa katika moja ya sababu ni tabia ya uombaji, kwamba kuna watu wengine kwa tabia tu ni waombaji, lakini Mhe.

Mwenyekiti, kwa ujumla mimi nasema katika Zanzibar hatukuwa na watu ambao kwa tabia tu ni waombaji, hatukuwa na utamaduni kama huo.

Sasa kuna kitu katika mabadiliko ya tabia kwa watu yanasababishwa na mambo mengi moja ikiwepo ni athari ya ushawishi kwa watu waliokuzunguka, sasa kama kutakuwa na tabia pengine tunaionea haya kuisema kwa sababu ya zile tabia zetu, miye kama kawaida yangu sina linalolionea haya kulizungumza hata moja.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi kama cha mwaka mmoja uliopita na palikuwa na kipindi fulani hasa palikuwa na ongezeko kubwa sana la watu waliokuwa wanatoka Tanzania Bara kuhamia hapa, hawaji kutafuta ajira, hawaji kwa chochote ni wale watu ambao tumewazoea kuwaona katika miji ya Dar es Salaam kwa mfano waombaji wakiwa sasa wanapiga kambi katika maeneo ya Mji Mkongwe, Darajani na katika harakati zote utawakuta, unamuona kaja na kigari chake, wengine unawaona hata yale mambo ya kufanya maigizo kwamba yeye ni mgonjwa wakati si mgonjwa ambapo kwa Dar es Salaam imekuwa ikiripotiwa sana katika vyombo vya habari, na kwetu yamekuwa yanaingia.

Sasa pengine liongezeke tena wimbi la hawa watu, na tunawajua tu wengine hasa vile wakizungumza lafdhi yao unajua kwamba huyu si Mzanzibari. Sasa hilo ninalisema kwa sababu hatuna tabia kama vile nilivyosema mwanzo ya kudhibiti, tunaambiwa kwamba una uhuru wa kwenda unapotaka, sasa hiki ni kisiwa lakini pia kinaathiri maadili yetu kwa sababu wakija hawa na baada ya muda wakiwa wengi wanaathiri na wengine na kutiwa ushawishi katika tabia na maumbile yetu. Sasa nasema hili tulitizame.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nikishasema hivyo, hiyo haiondoshi dhana kwamba Wazanzibari ni malaika hapana, haya yaliyotajwa hapa nayakubali yote, nayakubali yote na mimi nilikuwa nataka kupendekeza Mhe. Mwenyekiti, kwamba tujiulize kwamba kwa nini katika utafiti wanaonekane omba omba badala ya kuwa wale wa zaidi ya miaka 60 wamekuwa ni baina ya 40 na 60, maana yake kimaumbile wale waliofika miaka 60 na kwenda juu ndio wawe waombaji kwa sababu wameshafika umri wa kustaafu hawana kazi pengine na hali yetu ya uhifadhi wa jamii ndio hivyo hivyo, lakini kwa nini tujiulize kuna miaka 40 mpaka 60.

Mhe. Mwenyekiti, wametuambia wanafanya utafiti, mimi ninataka kuwaomba hebu tufanye utafiti sio kwa miaka 40 na 60 hawa tumeona sababu hizo, tuone wale ambao wanastahiki hasa hifadhi ya jamii ambao mimi ninavyotafsiri ni zaidi ya miaka 60 kwenda mbele, sasa tujue ni asilimia ngapi ya wananchi wetu. Mhe. Mwenyekiti, nilikua naangalia hichi kitabu cha sensa tulichopewa,

lakini bahati mbaya hichi hakina mnyambuliko wa umri, kina mnyambuliko wa jinsia lakini bahati mbaya humu ndani hamna na ile nimeona mapungufu makubwa sana, kwa sababu nilitegemea katika jambo la kwanza ni kutizama mjumuiko au mnyambuliko pia wa umri, lakini najua tu kwamba katika nchi zetu Tanganyika na Zanzibar wananchi wenye umri wa miaka 35 kuja chini ni takriban asilimia 70 ya wananchi wote wa Zanzibar, ninavyoambiwa lakini sijathibitisha, kwamba wazee wenye umri wa miaka 60 kwenda juu ni kama asilimia 4 ya wananchi wetu, ningeomba Waziri sijui kama anayo takwimu akaja akatusaidia pengine wanashughulika na Ustawi wa Jamii.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nasema tu kwamba hivyo hatuwezi kuwa na Sera ya hifadhi ya jamii ambayo badala ya kushughulikia wale wazee wachache waliokuwepo katika makaazi kama ya Sebleni au Limbani kule Pemba, ikawa badala yake tunawahudumia wazee wote ambao tumekuwa tumewasajili waliofika miaka 60 kwenda juu hata kama ni posho ndogo lakini akajihakikishia kwamba kila mwezi Serikali aliyoitumikia inamtunza.

Nilikuwa nasema hebu atufanyie utafiti, sipendekezi wakati mwengine katika mwaka huu, lakini katika huu utafiti wao na katika miradi yao ya maendeleo wanayo suala la hifadhi ya wazee nilikuwa naomba hili walifanyie kazi mwakani Mhe. Waziri akija aje atusaidie hapa kwamba hivi hatuwezi kama nchi kuja na sera ya kuhakikisha tunatoa hifadhi ya jamii kwa wazee wenye miaka 60 kwenda mbele kwa wote hata ni kwa mfano kama ni posho 30,000/= au 40,000/= lakini akajua kwamba mwisho wa mwezi ana pahala pa kupata, hii itatupa sasa nguvu za kukabiliana na wale omba omba mitaani, hivyo tutajua Serikali imewalinda na atakayekuwa anaomba aliyekuwa chini ya umri ule tutatizama kwamba huyu anaingia katika kundi gani sasa hivi katika ile hoja nyengine na mambo mengine, nafikiri tukifika hapo tutakuwa na mipango mizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninataka niseme kwamba mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe naiunga mkono hotuba hii ya bajeti na namwambia Mhe. bi Zainab atulie hakuna buti hata moja kutoka kwa Mhe. Jussa.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutukutanisha hapa leo siku hii kujadili hotuba ya Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Pili nikushukuru wewe kwa nafasi ambayo umenipa kusema machache katika hotuba hii. Tatu nimpongeze Waziri, kwa kazi nzuri ya uwasilishaji wa hotuba hii, lakini kama hotuba ya Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilivyosema kwamba tunapowapa hongera Mawaziri

tusisahau kuwapa pole watendaji wanaofanya kazi katika mazingira magumu na kufanikisha uwasilishaji huu wa bajeti katika Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaanza na Idara ya Maendeleo ya Vijana, na Idara hii ina jukumu la kujenga mazingira endelevu ya kuwawezesha vijana kujiimarisha kiuchumi, kiutamaduni na kijamii. Na kati ya malengo waliyojiwekea katika mwaka 2012/13 wameangalia utekelezaji wa mkataba wa kikanda wa maendeleo ya vijana ulioridhiwa Tanzania Januari 2012 kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa mkataba huu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nafahamu kuwa moja ya masharti ya mkataba huu ni nchi ambazo zilizoridhia mkataba huu zinatakiwa kuwa na mabaraza ya vijana. Mhe. Mwenyekiti, hapa ninachotaka kusema ni kwamba tangu Mhe. Rais, na Mhe. Jussa, hili amelisema kwamba tangu Mhe. Rais, ametangaza azma yake ya kuunda hili Baraza la Vijana, limekuwa kila siku linaratibiwa, linaratibiwa, haliishi. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa namtaka Mhe. Waziri, akija atuambie hasa ni lini Baraza la Vijana litaletwa. Bejati ya mwaka jana wamesema kwamba mswada umeshapelekwa kwa Makatibu Wakuu, ukarudishwa tena kwa Mwanasheria Mkuu, ukarudishwa tena kwa Makatibu Wakuu, sasa Mhe. Mwenyekiti, hii dana dana inayopigwa ya mswaada huu na mkataba huu unasema kwamba Mabaraza ya Vijana yaundwe ili vijana wafaidike na fursa na kazi ambazo zinapatikana na faida ambazo zinapatikana katika uridhiaji wa mkataba huu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka kumwambia Waziri kwamba afanye haraka na leo atuambie ni lini baraza la vijana litaundwa kwa sababu fursa kule hazitusubiri sisi tupige dana dana halafu tukazikute kule wakati nchi nyengine nyingi zimeridhia.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naingia katika ajira kwa vijana. Ajira kwa vijana zinaelekea kuwa janga la taifa sasa, kama taarifa zinavyosema kwamba wastani wa vijana laki moja mimi nasema na zaidi hawana ajira sasa limekuwa tatizo. Na Mhe. Mwenyekiti, katika bajeti ya Serikali ile ya ujumla Mhe. Waziri wa Fedha alisema kwamba wameona kwamba hili ni tatizo, na mara hii katika maeneo ambayo yamepewa kipaumbele moja ni ajira kwa vijana, lakini Mhe. Mwenyekiti, tatizo hili kubwa na Serikali imetenga 1.1 bilioni tu kwa ajili ya tatizo hili, na ukiangalia mchanganuo wa ile miradi na programmu za ajira ambazo vijana watanufaika katika wale laki moja ambao tunasema hawana ajira lakini mimi naamini na zaidi vijana elfu moja mia moja na kitu ndio watafaidika na hii *priority* ambayo Serikali imeweka.

Mhe. Mwenyekiti, hapa mimi najiuliza vijana hawana kazi laki moja na *priority* waliyopewa fedha zilizopelekwa katika miradi ni vijana elfu moja

mia moja tu ambao watafaidika je Mhe. Mheshimiwa hatuoni kwamba hili tatizo hata kama limepewa *priority* hatutoona ile *outcome* yake kwa sababu tatizo ni kubwa na juhudi zilochukuliwa ku-s*olve* hili tatizo ni ndogo sana, ni sawa sawa na unachukua sukari unaenda kutia kwenye bahari.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo niipongeze Wizara kwa kuwawezesha vijana waliojiunga katika vikundi mbali mbali vya SACCOS na vyengine vilivyojikusanya pamoja. Mhe. Mwenyekiti, lengo la Wizara mwaka huu 2013/14 ni kuendeleza na kuimarisha miundombinu ya uzalishaji wa mazao ya kilimo cha *rosella* na mboga mboga kwa vijana Unguja na Pemba. Naipongeza Wizara sana kwa hili, lakini nilikuwa nataka nimuulize Mhe. Waziri, wamehakikishaje lile soko la *rosella* kwa hawa vijana yaani wanawatafutiaje soko ili hawa vijana waweze kuuza hizi mboga mboga na *rosella*, *fine* kulima wamelima lakini soko wanapata wapi.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema nimeona pia Wizara imechukua juhudi ya kuondokana na kile kilimo wanaita cha asili, sasa hivi wanaenda kwenye kilimo kile cha *green house* niipongeze sana Wizara kwa hatua iliyochukua na nawaomba wawashajiishe vijana ambao bado hawajafanya hizi kazi kwa pamoja tushajiishe vijana wajikusanye ili wafaidike na kilimo hichi kwa sababu hakitumii nguvu na faida yake ni kubwa kuliko kilimo cha kawaida.

Kwa hiyo niwaombe vijana wajitokeze ili wafaidike na fursa ya kilimo hichi. lakini vile vile niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi wa Majimbo na wao pia waone wawe na ile hamu ya kusaidia vijana wasiiwachie Wizara pake yake kwa sababu tatizo ni kubwa, huyu mtaalamu wa *green house*, mimi namjua kwa anayetaka anifuate nitawapeleka wakapewe taaluma wao halafu wakusanye vijana wao wapeleke hii miradi katika majimbo yao, ili kuona kwamba vijana na wao wanafaidika *rather than* kuwaachilia Wizara ya Wanawake na Watoto peke yake.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimeona kwamba Wizara ilishiriki kongamano la vijana la Dunia lililofanyika Indonesia na kati ya kazi ambayo waliifanya walijadili umuhimu wa upatikanaji wa afya na elimu ikiwa ni pamoja na elimu ya amali na upatikanaji wa ajira zenye kutambulika na zenye staha kwa vijana. Sasa niwaombe Wizara tu wale waliojifunza kule basi wakusanye vijana hasa katika haya mambo ya elimu ya amali, wakusanye vijana wawape taaluma, wawashajiishe, wawezeshwe ili yale waliyojifunza kule kama Idara hii tuone kwamba vijana wetu wanafaidika na haya mambo ambayo wameenda kujifunza.

Mhe. Mwenyekiti, nikimaliza na ajira za vijana, nilikuwa nataka kuzungumzia mporomoko kwa maadili kwa vijana. Mhe. Mwenyekiti, jukumu la Idara ya Maendeleo ya Vijana ni kujenga mazingira endelevu ya kuwawezesha vijana kujiimarisha kiuchumi, kiutamaduni na kijamii. Pamoja na kwamba tunajua utandawazi umechukua nafasi kubwa sana katika kusababisha hali ya mporomoko wa maadili kwa vijana, lakini pia Wizara kama Wizara kwenye jukumu lake la kuwawezesha vijana kujiimarisha hasa pale tunapozungumzia kiutamaduni hatujaona bado. Tumeshaona kweli wamewezeshwa vijana kiuchumi na kijamii lakini pale kiutamaduni hatujaona bado. Na nilikuwa nataka nimuulize Mhe. Waziri, jee wamefanya nini wao kama Wizara kuwawezesha kiutamaduni, kwa sababu tunajua kwamba kwenye kuimarisha kijamii na kiuchumi tumeona lakini kiutamaduni bado hatujaona *may be* hilo lingesaidia katika kuwaweka vijana katika maadili mazuri, kwa sababu na hasa tukizingatia silka za Mzanzibari zinalindwa na utamaduni wao. Hivyo nilikuwa namuomba Mhe. Waziri, aje atueleze kiuchumi na kijamii tumeona amefanya kazi nzuri sana lakini hapa kiutamaduni Wizara kama Wizara imefanya nini?

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo naingia Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Niipongeze Wizara kwa kazi nzuri sana ambayo inaifanya ya kuwawezesha wanawake na niwapongeze kinamama wameshajiishika vizuri kuliko vijana, na waendelee tu wale kinamama walioamka waendelee kuwaamsha wenzao ili tusione tunaachwa nyuma. Mhe. Mwenyekiti, katika shabaha alizopanga kutekeleza mwaka 2012/13 hii Idara ya Maendeleo, Wanawake na Watoto moja ni kuhamasisha uanzishaji wa Benki ya Wanawake na nimeona kwamba Wizara imechakarika imefanya utafiti hapa na pale kuona kwamba hii Benki inaanzishwa.

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba upatikanaji wa fedha kama Waziri alivyoripoti ni wa kusuasua, sasa nataka kusema kama fedha ni tatizo basi *at least* Waziri afanye namna ya kuona kwamba wale waliofungua Benki kama hii kule Tanzania Bara wanafungua *at least* Tawi, tunaweza tukaanza na lile tawi baadae tukaja na Benki yetu wenyewe, lakini kwa sasa anaweza kufanya wale waliofungua kule wakaja kufungua huku ili wanawake na wao wakafaidika na huduma zile za kibenki ambazo zinatolewa na Benki ile. Mhe. Mwenyekiti, kwa wanawake sina mengi ya kusema nitaawachia wanawake wenzangu najua watagusia mambo mengi sana lakini naingia kwa watoto sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kushirikiana na Wadau wa maendeleo *Save the Children* sambamba na Wizara ya Katiba na Sheria hatimae kuona kwamba Mahakama ya Watoto ama *juvenile court* imeanzishwa ni hatua nzuri na ya kupongezwa. Lakini vile vile niipongeze

Wizara kwa jitihada waliyoichukua ya kuandika mradi wa kurekebisha mfumo wa sheria za watoto Zanzibar ili kupitia mfumo wa sheria za watoto na kuyafanyia kazi mapungufu yaliyopo katika sheria za watoto. Mhe. Mwenyekiti, hilo ndio tatizo kubwa kuna mapungufu katika sheria za watoto na ndio maana watoto wanashindwa kupata haki zao. Mhe. Mwenyekiti, kwa hatua hiyo waliyoichukua kweli nimeamini panapo wanawake hakiharibiki kitu.

Mhe. Mwenyekiti, katika uanzishwaji wa Mahakama ya Watoto wameanzisha ule utaratibu wa kuendesha kesi bila ya kuonana na yule mhalifu na mtoto kwa sababu walituambia katika Kamati kwamba kuna siku mtoto alimuona mtu ambaye alimfanyia kitendo cha udhalilisha akazimia hapo hapo. Kwa hiyo, wameanzisha ule utaratibu kwamba huyu mhalifu anakuweko kwenye chumba chengine na mtoto anakuwa kwenye chumba chengine wanahojiana kwa njia kama ya *video conference.*

Lakini Mhe. Mwenyekiti, hapa kulikuwa kuna tatizo, tatizo ni kwamba kifaa cha sauti hakijapatikana na wafadhili kidogo wanasuasua. Tuliulizia kwenye kamati tukaambiwa ndio wanafuatilia. Lakini Mhe. Mwenyekiti, niseme wizara hii nayo ihangaikie suala hili kwa sababu kifaa hiki ni muhimu kitasaidia sana mtoto kutoa ushahidi bila kuogopa.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ambalo naona ni muhimu kiambatanisho nambari 3 ukurasa wa 58 kimeonesha hapa, taarifa za Kituo cha Mkono kwa Mkono, *one stop centre* kuanzia mwezi wa Julai 2012 hadi Aprili. Huu ni mwezi wa Julai 2012 tu hadi Aprili 2013 kubakwa 480, mimba 186, kulawitiwa 53. Mhe. Mwenyekiti, tatizo ni kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, nilisikitishwa sana na Wizara ya Afya juzi wakati inajibu swali la Mhe. Saleh Nassor Juma nafikiri, walisema kwamba ile *DNA machine* umuhimu wake ni katika ku-*prove maternal right,* ile kuhakikisha kwamba baba ndiye mzazi halali wa mtoto. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nimesikitishwa na kauli ile ya Wizara ya Afya na nasema kwamba kile kifaa ni muhimu sana ku-*prove* hizi kesi za kulawitiwa na ubakwaji.

Mhe. Mwenyekiti, *DPP* haamini ushahidi wa kuona hata ukimpeleka mtoto anachuruzikwa na umchukue yule mbakaji umpeleke wao hawaamini ushahidi wa kuona. Wao wanaamini kwamba hakuna hatia bila ushahidi, ushahidi wao wanaoamini ni ule wa kitaalamu na kifaa hiki hatuna. Mkurugenzi wa Mashtaka anafika sehemu anasema kwamba yeye anashindwa kutokana na bajeti yake ndogo kulipa wale wataalamu wanaotoka Tanzania Bara kuja huku kufuatilia zile kesi, kwa hiyo wanakatisha kati kati kesi zinaishia juu juu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sishangai kwamba pia huu ubakaji na kulawitiwa kwa watoto unaendelea. Kwa sababu wale wanaofanya hicho kitendo wameshajua kwamba Zanzibar ku-*prove* hizo kesi ni ngumu, utakwenda utarudi, utakwenda utarudi na ndio maana ubakaji na kulawitiwa kwa watoto unaendelea siku hadi siku. Sasa Mhe. Mwenyekiti, niishauri wizara kwa kuwa hiki kifaa kimeshakuwa mtambuka, Wizara ya Afya wanahitaji, *DPP* anahitaji na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto pengine itasaidia. Kwa hivyo, wakae waone, Mhe. Naibu Waziri wa Afya alisema ni shilingi 600 milioni, pesa hizo ni kidogo sana kwa serikali.

Kwa hivyo, wizara hizi tatu au taasisi hizi tatu za serikali zikae zione kwamba hiki kifaa kinapatikana ni muhimu, ni muhimu sana. Watu wanajifanyia mambo tu kwa sababu wanajua ku-*prove* hizi kesi ni ngumu sana. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na naheshimu muda wako, baada ya kusema hayo machache naunga mkono hoja.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa na mimi fursa hii nikachangia machache katika hotuba hii ya Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kutupa uhai wake tukaweza kufikia tena Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani tukiwa tumo ndani ya hali ya uzima na afya njema. *Inshaallah* tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie, atutakabalie Ramadhani zetu na atusamehe makosa tuliyomkosa.

Baada ya shukurani zangu hizo Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa ujumla kwa kutuletea bajeti yao hii ili kuweza kutoa mawazo yetu na sisi Wajumbe kwa kuweza kusaidia ufanisi zaidi katika shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nikianza mchango wangu nianze katika Idara ya Mipango, Sera na Utafiti katika kifungu cha 15, ingawa watu wengi wameshaielezea lakini na mimi kidogo nataka niigusie.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili la ombaomba hasa kwa asilimia hii iliyotolewa hapa ambayo asilimia 65 ni wanawake, basi kwa kweli kwa upande wangu mimi sikujisikia vizuri, sikujisikia kwa sababu si kitendo kizuri na wala sio mila na desturi yetu katika kisiwa hiki cha Zanzibar. Kwanza linanisikitisha hili jambo, na kwa sababu nilikuwa sijalisikia mara ya kwanza kuona katika kitabu hiki suala hili ukizingatia wilaya yangu mimi ni Wilaya ya Micheweni ndio wilaya ambayo pengine inasemekana ndio watu wanaoishi katika mazingira magumu. Kitendo hiki bado sijakifanyia utafiti, lakini naona wanawake wa wilaya ile ni watu wanaojithamini sana na ni watu ambao wana

shughuli zao nyingi za kufanya hasa wanawake. Ukienda kwenye kilimo ni wanawake, ukienda kwenye uzalishaji wa masuala madogo madogo wanawake wanajishughulisha na kupitia hasa hata hao viongozi wao tuseme Waheshimiwa basi si aghalabu kuwakuta wanawake ndio saa 24 saidia hili, nipe hili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mimi lilinisikitisha suala hili, lakini sishangai Zanzibar ni kubwa. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri kama wanavyotupa tathmini za matokeo mengine mfano masuala ya UKIMWI kuwa pengine wilaya fulani kuna asilimia fulani, kuna watu wangapi, basi na hili angetupa tathmini yake kwa kiwilaya ni wilaya gani hasa ambayo inajishughulisha na mambo haya na hasa katika umri huu uliotajwa ambao ni wanawake waliokuwa bado wanaweza kufanya kazi na kujipatia riziki zao za uhalali. Kwa hivyo, naiomba Wizara ifanye uchunguzi wa kina ili na sisi Wawakilishi ambao tunawawakilisha wananchi wetu hapa basi na hili tuwe Wajumbe wa kulifanyia kazi huko tunakotoka.

Mhe. Mwenyekiti, jengine katika maendeleo haya ya Sera na Utafiti kifungu cha 17 Mhe. Waziri amesema kwamba wizara imesimamia uundwaji wa kamati 11 za kupambana na udhalilishaji wa kijinsia, kataja katika Shehia ya Mkoani. Kwanza Mhe. Mwenyekiti, mimi nampongeza sana kwa hili, lakini ingawa hili wanalianza kwa wilaya hii ya Mkoani na wilaya nyengine nadhani litafuatia, lakini huku nyuma tunakotokea kuliundwa kila shehia kuna Jumuiya za Kinamama ambazo zilikuwa zikifanya shughuli hizi. Tulitegemea sana kuwa jumuiya zile nazo ziwemo. Sasa mimi nataka anifahamishe Mhe. Waziri, kamati hizi zinazoundwa wajumbe wake ni nani na nani ili kushughulikia suala hili. Kwa sababu kama kunaundwa kamati hizi, kama kuna mchanganyiko pengine baina ya wanawake na wanaume basi mimi ningependelea sana kamati hizi masheha wawemo na polisi jamii ili kufanikisha, na wanawake pia waingizwe katika kamati hizi.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nataka aje anieleze Mhe. Waziri hizi kamati zilizokwishaundwa ni watu wa aina gani. Pia katika shehia hiyo pengine au katika kamati hizo zitakazoundwa kama kuna wafanyakazi wa vituo kama Polisi basi waingizwe nao katika kamati ile ili kila mmoja awe na mawazo yake tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kifungu cha 12 matokeo ya awali ya utafiti yalionesha kwamba, vitendo vya udhalilishaji vinaonekana kote Unguja na Pemba na kesi nyingi za udhalilishaji hazihukumiwi. Mimi nikubaliane naye hili, lakini katika huku kuhukumiwa kuna hila mbili; kuna kutohukumiwa pengine kwa kukosa ushahidi hili pia linachangia kupitia jamii na ningewaomba wanawake wenzangu kusimamia suala hili na kupeana elimu ili

tuondokane na hili la kuwa ushakuwa na mtu kafanya kosa lakini hatimaye ushahidi unashindikana kutolewa hilo litakuwa ni tatizo.

Lakini na suala jengine kwa upande wa serikali ni kweli kuwa masuala haya hayafikii muafaka mzuri, lakini pia hata kuwa zitafikia hayo maamuzi kutolewa basi hukumu zinazotolewa ni ndogo kulinganisha na udhalilishaji wa watoto unaoendelea.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niwashukuru sana watu wa Mawio, kila siku watu wa Mawio utasikia ndani ya taarifa za mawio matokeo kadhaa wa kadhaa. Juzi tu kuchelewa jana nilisikia kuwa kuna mtoto ambaye amelawitiwa wa miaka kumi. Basi kesi ile ikaendeshwa na ushahidi wa watu ukapatikana, lakini hatimaye mtu huyo alitolewa hukumu ya kufungwa miezi minane. Hee! Miezi minane ni hukumu ya kufungwa mtu katili namna hii anayekwenda kumlawiti mtoto wa kiume wa miaka kumi, maana yake kakusudia nini? Kakusudia nini mtoto wa miaka kumi bado ni mtoto mdogo kwenda kumfanya kitendo kama kile, ati anahukumiwa miezi minane, huyu ni mtu wa kufungwa angalau miaka mitano kwa uchache.

Sasa kwa kweli hili suala lina matatizo na litaendelea kuwa na matatizo kwa hukumu hizo tunazozitoa na pengine hiyo miezi minane anayofungwa ana watu wake siku nyengine unakuja kumuona keshatolewa huyo. Sasa hili Mhe. Mwenyekiti, litaendelea kuwepo na tutaendelea kuwepo watoto kwa kufanyiwa vitendo kama hivi.

Juzi moja kwenye Mawio hivyo hivyo nilisikia kuna mtoto wa miaka mitatu huyo hakuwahi kumfanya chochote, lakini tayari alikwishaanza kumvua suruali hatimaye wazazi wake wakatokea. Lakini kapelekwa kwenye vyombo vya sheria hata bakora kupigwa angalau akaoneshwa kuwa hiki kitendo anachokifanya ni kibaya hafanyiwi, ni kwenda pale kwa sababu hakuwahi kumfanya hivyo na yeye akaondolewa. Sasa hivi vitendo Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wizara yake isimamie sana suala hili lakini ni tatizo kusema kweli.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 39 Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto na Utekelezaji shabaha zilizotolewa katika kufanya maendeleo ya wizara. Suala la nne hili kuhamasishwa uanzishwaji wa Benki ya Wanawake.

Mhe. Mwenyekiti, hili angalau tungetegemea leo kuona kuwa imefikia wapi, lakini mwaka jana tuliambiwa kuna masuala haya ya kuwahamasisha watu kuanzishwa benki hii ya wanawake. Lakini kitabu leo kimekuja tena kina suala hili hili la kuhamasishwa na kuanzishwa benki hii. Hapa Mhe. Waziri angetwambia tatizo ni nini? Kwa sababu ukiangalia vikundi vingi viko kwa

SACCOS zinazoanzishwa. Sasa hili nalo pia angetueleza tatizo ni kitu gani au kakwama wapi tukaishauri serikali ikasaidia kuhusu hili ili Zanzibar nayo likapatikana suala hili la kuanzishwa hii benki ya wanawake.

Mhe. Mwenyekiti, jenginge kuhusu hii Mahkama ya Watoto. Mimi ningemuomba Mhe. Waziri kama hii mahkama ishaanza kufanya kazi kesi zozote zitazokuwa ni za watoto basi zipelekwe kwenye mahkama hiyo. Hatutaki tena kupeleka kesi za watoto kwenye mahkama nyengine ili tuone hii mahkama ya watoto nayo itaendeshwa vipi. Hilo ni ombi langu jengine, lakini ningemuomba pia atuelezee kuhusu ujenzi wa jengo la wizara tumefikia hatua gani ili tupate kujua.

Lakini la mwisho Waheshimiwa kuna vikundi vingi huku ambavyo vimetembelewa, vimefadhiliwa, vimesaidiwa, chungunzima. Sasa angetueleza Mhe. Waziri vikundi hivi vinavyofanyiwa haya katika utembeleaji wenu tathmini inaonesha vipi? Kwa sababu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika juzi alipokuwa akijibu maswali alisema kwamba hata mikopo iliyotolewa ya AK na JK haikuwa na mafanikio. Sasa kama kuna vikundi tu lakini havina mafanikio inakuwa si jambo zuri, kwa sababu pesa ni nyingi zinazotumika, misaada inatolewa lakini hatujui masuala haya yanaendelea vipi.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mwanzo kabla ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeweza kuniwezesha kusimama hapa na kuweza kupumua kwa pumzi zake. Nitakuwa si mwingi wa fadhila Mhe. Mwenyekiti, kama sikukushukuru wewe kunipa fursa hii kwa kuniruhusu kuchangia. Vile vile nataka nimshukuru Mhe. Waziri kwa mashirikiano yako, utu wake, uungwana wake aliouonesha katika kamati iliyomaliza muda wake ya Baraza la Wawakilishi. Ningeomba Mawaziri wengine au Manaibu Mawaziri wengine wakaonesha mashirikiano aliyoonesha. Mheshimiwa huyu alionesha mashirikiano ya hali ya juu ya kamati iliyomaliza muda wake.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, nianze katika utangulizi kuhusu Mwezi Mtukufu wa Ramadhani tulionao ambao tumeanza leo wengine pengine wameanza jana, lakini safari Mhe. Mwenyekiti, mnayokwenda kwa miguu usitegemee kuwa nyote mtafika kwa wakati mmoja, wengine watakuweko mbele wengine watakuweko nyuma muhimu tufike salama.

Mhe. Mwenyekiti, wito wangu wafanyabiashara kama alivyozungumza Mhe. Rais wetu wa Zanzibar wasije wakatumia mwezi huu Mtukufu kama ndio machumo watoe huduma tu, na wale wanaokula watafute sehemu ya kujistiri kama mila zetu na desturi za Zanzibar zilivyo.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, nianze Idara ya Ustawi wa Jamii ukurasa wa 58. Kuhusu matokeo ya unyanyasaji wanawake na watoto Mheshimiwa hali ni mbaya kwa mujibu wa takwimu inaonekana tatizo limekuwa sugu, mfano wa matokeo ya ubakaji 480 yameripotiwa kuanzia Julai, 2012 – Aprili 2013; kesi za mimba 176, kesi za kukashifiwa 273 na kesi za kutorosha 22. Jumla ya watu waliokumbwa na mikasa ya unyanyasaji wa wanawake na watoto ni 105 ikiwemo matukio 53 ya kulawitiwa watoto.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, ningependa Mhe. Waziri atueleze wamefanya utafiti gani kujua chanzo cha kuibuka kasi ya matukio ya ubakaji na unyanyasaji. Vile vile Mhe. Waziri akija anieleze maeneo gani hasa yaliyoathirika na kadhia hii kwa vitendo vya ubakaji na unyanyasaji kwa wanawake na watoto. Vile vile kumekuwa na tatizo kubwa la usimamiaji kesi. Suala hili tulikuwa tunalipigia kelele sana, kuna kesi zilizofunguliwa 127, kesi 66 zilizosikilizwa kati ya kesi hizo washtakiwa watatu tu, ndio waliopatikana na hatia na mmoja tu ndiye aliyefungwa jela. Tumekuwa tukilipigia kelele sana Mhe. Mwenyekiti, suala hili pamoja na jitihada alizozichukua Mhe. Rais wetu za kuanzisha Kitengo cha Rushwa labda hiki kitasaidia.

La pili Mhe. Mwenyekiti, jamii lazima ibadilike, iache tabia ya kuona matukio ya ubakaji ni kama matukio ya aibu na badala yake kuyaona kifamilia wanaohusika kuozeshwa. Kitendo hiki kinasababisha vijana hasa suala la ubakaji wanasikitisha sana. Na tabia nyengine unapompeleka mhalifu au mtuhumiwa kituoni askari kuna taarifa hugeuka ndio mashehe wanaoozesha baada ya kusimamia makosa ya jinai.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 26 watoto wanaoishi katika mazingira magumu kutokana na matatizo ya umasikini, vizuri serikali ikaweka mipango madhubuti itakayosaidia kuondoa tatizo hilo. Kwa mujibu wa hotuba ya Mhe. Waziri watoto 7,368 wanaoishi katika mazingira magumu walitambuliwa na wizara yake. Lakini Mhe. Waziri hao bado wanaendelea kuteseka na serikali lazima itafute njia ya kuwasaidia.

Sasa nije katika Wilaya ya Micheweni ambayo wengi wamechangia. Watoto wamegeuzwa kuwa mitambo ya kuvunjia kokoto kule kwa kusaidia familia zao, wanakosa masomo na wengine hata kutofika maskuli na kuchangia mahudhurio madogo sana Mhe. Mwenyekiti. Hii inasababishwa na waume

zao kuhamia dago kwa muda mrefu na kuacha watoto, mama zao wakawatuma ili kwenda kutafuta chejio.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nafikiri serikali ingeangalia njia muafaka ya kuweza kuwasaidia wale kuwapelekea boti za kisasa watu wa Micheweni na kuondoa tatizo la kuvunja kokoto. Mhe. Mwenyekiti, hawa wanatembea hata shati hawana wanatembea vifua wazi watoto hao wa Micheweni.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye maadili. Vile vile watoto chini ya umri wa miaka 18 wasiruhusiwe kuingia katika makundi ya disko na kusababisha watoto wadogo leo hii kuwa bingwa wa kucheza muziki kuliko watu wazima. Mheshimiwa ombi langu siku moja tulitembelea ukumbi wa disko *Full Moon* huko Nungwi kisha tupate jibu ndivyo Zanzibar ilivyokuwa na mila na desturi zake ambapo Zanzibar ilikuwa ni kituo kikuu cha dini? Kuna tatizo jengine Mhe. Mwenyekiti, watoto hivi sasa wanatembeza *CD* za ngono mitaani. Hili nalo liangaliwe. Vile vile wengine hukaa kwenye barabara hasa ya Mzee Ali Hassan Mwinyi na wengine hata Bwawani.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, sitounga hoja mkono mpaka nitakapopata maelezo kamili.

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema mchana huu. Pili napenda kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kupanga bajeti yao na kutuletea hapa, vile vile napenda kuipongeza wizara yake kwa kuchukua bidii katika kutekeleza malengo ya MKUZA II katika kuongeza kipato na kupunguza umasikini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nina masikitiko makubwa kwa vikundi ambavyo vimepata misaada na kupewa mikopo. Wilaya takriban zote zimepata mikopo na vikundi vyengine vimepata kusaidiwa. Cha kusikitisha ni kwamba, Wilaya ya Kusini Unguja ni kubwa ambayo imesaidiwa vikundi vitatu tu, navyo ni Kizimkazi, Muyuni ‘B’ na Paje. Kuna vikundi vingi kama Makunduchi sijakiona, Bwejuu na Jambiani, sijui Mhe. Waziri kuna vigezo gani ambavyo vinapelekea kutokana na vikundi hivi ambavyo havikupata chochote, havikupata msaada wala pesa.

Mhe. Mwenyekiti, vikundi hivi vyote ambavyo nimeviona katika orodha hii sijui ni vingapi ambavyo vina watu wenye ulemavu au ni wenye ulemavu wangapi ambao wamo katika vikundi hivyo.

Mhe. M wenyekiti, nije katika suala la ubakaji. Kwa kweli suala la ubakaji bado serikali haijawa tayari, kutokana na kwamba juzi nilisikia kwenye Chombo cha Habari, kwamba kuna kijana mmoja ambaye kijana huyo ni mwanamme mwenye umri wa miaka 20 kambaka mtoto wa miaka kumi na hatimaye kupelekwa kwenye vyombo vya sheria na kufunguliwa mashtaka na kafungwa kifungo cha miezi kumi, sio mwaka ni miezi kumi. Je, kweli serikali iko tayari kwa suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, Kituo cha Kulelea Wazee wasiojiweza Welezo. Kituo hicho ni kituo ambacho wafanyakazi wake ni watu ambao wana bidii, ni watu hodari, wana jitihada kubwa, ningeiomba serikali iwaongezee posho wafanyakazi wale kutokana na juhudi wanayoichukua pamoja na wafanyakazi wao.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije kwenye jengo la Wazee Wete, jengo ambalo halina uzio. Sasa ningeiomba wizara kuiuliza kwamba ni lini watajenga uzio kwenye jengo hilo? Katika bajeti yake kasema katoa vespa nne, vespa nne hizi ningemuuliza Mhe. Waziri, Unguja ni ngapi na Pemba ni ngapi? Kwa kuwa Pemba tulikwenda tukaona mfanyakazi wa kituo cha kulelea wazee alikuwa hana usafiri je, mfanyakazi yule keshapata usafiri.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi asubuhi hii ya leo kunipa nafasi kuweza kuchangia hotuba ya mama yangu hapo. Kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa ujasiri wake wa kutusikiliza viongozi wenzake katika kusaidia harakati za maendeleo. Hilo nampongeza pamoja na Katibu wake, Naibu wake, Wakurugenzi wake namalizia jumla na watendaji wake wote. Hiyo ni moja katika sifa ya kiongozi kuwa mtiifu kwa kuwasikiliza viongozi wenzake wa *backbencher*.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze na suala ambalo nataka nisilisahau ningemuomba sana Mheshimiwa wangu; wapi, ukurasa atatafuta yeye, nimeomba kwa kuwa haki sawa kwa wote na hasa katika suala la utembezaji wa mwenge ningemuomba Mhe. Waziri ajaribu mara hii tuwe sawasawa ikiwa kule watatu na huku watatu. Hilo naomba sana Mhe. Waziri ajaribu kulipigia debe kuwa tuwe haki sawa kwa wote kule watatu na huku watatu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimefurahi sana na kitabu hiki, kitabu cha aina yake na hasa ukitaka kumjua mtu ambaye hana nia ya ubadhirifu wa kutaka kula mali za umma basi ni mmoja mama yangu, leo kaonesha jinsi ambavyo fedha anavyozitaka kuzitumia hizo atazopewa katika bajeti yake. Amepangilia kitabu chake kizuri ametuonesha jinsi gani programu ambazo wanataka

kuzitekeleza katika kipindi hiki cha bajeti. Mama, Mheshimiwa Waziri hongera sana na hii leo aina ya peke yake sijapata kuona kitabu kama hiki.

Mhe. Mwenyekiti, nimpe pole Mhe. Waziri katika utendaji wa kazi. Kwa sababu Mhe. Waziri hana mafungu ya fedha ya kuwasaidia vijana, kuwasaidia kinamama na kuwasaidia watoto. Mhe. Mwenyekiti, sisemi Mhe. Rais amekosea, Mhe. Rais amefanya vizuri, lakini na sisi tunaweza kumsaidia, na mimi namsaidia ushauri wangu. Ingewezekana ile Wizara ya Uwezeshaji basi angepewa mama yangu huyu, kwa sababu asilimia kubwa ndio wamo wa kuwezeshwa wenyewe mle, lakini kwa bahati mbaya imekwenda kupelekwa sehemu nyengine pale mama angu ndio angepata kuweza kuwatajirisha vijana na kuweza kuwatajirisha kina mama na kuondoa kudhalilika kwa watoto kwa kutumwa kazi ambazo zilizokuwa sio umri wao. Lakini ndio limekuwa na limeshakuwa.

Lakini mimi zaidi ningesema Mhe. Mwenyekiti, kwa nini hili fungu la Zakka na Sadaka asipewe yeye kwa sababu anahudumia mama mpaka wajane, na wajane ni moja katika fungu kubwa mkamsaidia katika kumuendeshea maendeleo. Sasa sadaka hizo lile fungu angepewa yeye mama na Mhe. Waziri akaweza kusaidia wajane akaweza kuwasaidia vijana ambao hawana ajira mafakiri, masikini ya Mungu ambao hawana mbele wala nyuma. Lakini sasa limekwenda kupelekwa kwengine. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, na yeye fungu hili apatiwe huyu mama ili aweze kufanya kazi zake kwa vizuri. Vyengine tutakuja kumpigia buti hapa tushachoka nae.

Mhe. Mwenyekiti, bado hatujawa *serious* kuwasaidia vijana. Kwa mfano niseme Jimbo la Kitope kuna vijana wengi sana hawana kazi na ukanda wote ule una mahoteli tumehangaika vya kutosha hatujafika pahali lile lengo tukihangaika huku Waziri huyu anatwambia jambo jengine wa Uwezeshaji. Lakini nataka kumwambia mama angu sasa tuondoke mezani tukimaliza bajeti twende hoteli hadi hoteli ukaangalie mwenyewe jinsi vijana wako wa kizanzibari wamekosa kazi na wakati hoteli zimewazunguka katika kisiwa hichi cha Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, tunapiga kelele kila siku ajira lakini tatizo hamjaliona na mkiliona nikikwambieni mnafumba macho hamtaki kuona sasa hilo ndio tatizo lenyewe. Leo Wahindi wanaletwa kibao wamo kwenye mahoteli, hawana hata vyeti wanaitana tu unafikiri wewe Mzanzibari utapata wapi kazi. Mhe. Mwenyekiti, isitoshe Wakenya kibao ndani ya mahoteli unafikiria vipi Mzanzibari atapata kazi hizo. Mhe. Mwenyekiti, linasikitisha na tulisema katika mgao kati ya *Mainland* na hapa tutafanya ubia uwe pamoja asilimia kidogo izidi huku kwetu, lakini hadi leo hatukuyafanya hadi leo hii tunapiga kelele tu kila siku. Mhe. Mwenyekiti, na sisi tunachoka kupiga debe sasa. Na

kusema tuandamane haiwezekani kwa sababu nchi yetu haipendi mambo ya fujo fujo. Lakini iko siku na wao wananchi wetu watasema wamechoka.

Mhe. Mwenyekiti, hii ardhi ni yao uchumi wao, Sera ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeleta sera ya kuwainua vijana kwa kupata kazi, ajira na kusema kuwa watu wajenge mahoteli ili tunufaike na ajira hizo, lakini hamna kitu Mhe. Mwenyekiti, hatunufaiki hatujawa *serious* hili ukweli tuseme.
Hili nitakuja kulisemea zaidi kunako mbele ya safari kunako wizara husika. Lakini naanzia hapa kwa sababu hapa napo ajira imo vijana wamo. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hali ni ngumu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano nina swahiba wangu sasa hivi anataka kuleta viwanda vya kuwasaidia wananchi au vijana kuleta ajira, mimi naomba sana hata hiyo Serikali iweze kutafuta eneo la kuweza kumsaidia ili ajira ziweze kupatikana kwa wananchi kwa wingi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, usiwashe taa namalizia kama dakika mbili. Nimshukuru sana Mhe. Waziri na watendaji wake tulipeleka ombi la kutaka...

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe hapa juu leo na muda huu mnaowaona na kuwashuhudia ni wageni wetu kutoka Bunge la Korea ambao wamefika hapa wakiongozana na Mhe. Naibu Spika, wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Lakini pia wapo na Spika wetu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar wamekuja kututembelea na kuona namna gani tunaendesha shughuli zetu katika Baraza letu la Wawakilishi la Zanzibar. Naomba mtambue uwepo wao na jumla yao ni Wajumbe 25. Wageni wetu karibuni sana. Anayeongoza msafara huo ni:- (*Makofi*).

1)	Hon. Kang Chang Hee	- Speaker of the National Assembly
2)	Hon. Lee Jae Sook	- Spouse of the Speaker
3)	Hon. Lee Ju Young	- Member of the National Assembly
4)	Hon. Kang Dong Won	- Member of the National Assembly
5)	Hon. Kwom Eun Hee	- Member of the National Assembly
6)	Hon. Seo Young Kyo	- Member of the National Assembly
7)	Hon. Lee Jae Young	- Member of the National Assembly
8)	Hon. Kim Yeon Kwang	- Chief of Staff to the Speaker
9)	Mr. Bae Sung Rye	- Spokesman of the National Assembly
10)	Mr. Song Dae Ho	- Director General
11)	Mr. Cho Yun Soo	- Principal Secretary to the Speaker (Foreign Affairs)
12)	Mr. Hwang Yong Ho	- Secretary to the Speaker
13)	Mr. Kim Kyoung Ho	- Director

14)	Mr. Choi Ki Do	-Secretary to the Speaker
15)	Mr. Je Min	-Deputy Director
16)	Mr. Im So Young	- Protocol Officer & Interpreter
17)	Mr. Kim Kyung Pil	- Secretary to the Speaker
18)	Mr. Park Moon Sook	- Secretary to the Speaker
19)	Mr. Cho Sung Hoon	- Program Coordinator
20)	Mr. Lee Chul Kyu	- Program Coordinator
21)	Mr. Lee Jun Seo	- Journalist (Reporter)
22)	Mr. Kim Bo Hyun	- Journalist (Camera Crew)
23)	Mr. Kim Hyun Kyung	- Journalist (Reporter)
24)	Mr. Lim Jin Wan	- Journalist (Photographer)
25)	Mr. Moon Sung Hwan	- Director of Africa Division

Waheshimiwa hawa ndio wageni wetu na majina yao ndio hayo kama mlivyoyasikia. "*Welcome* Zanzibar".

Mhe. Makame Mshimba malizia dakika moja iliyobakia.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: (anaendelea) Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka kuwapongeza wageni wetu, lakini siwapongezi tena kwa dakika uliyonipa.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru na wewe kwa kuyajua majina ya wageni wetu kwa ufasaha vizuri *inshaallah* Mwenyezi Mungu akujalie uendelee na lugha hiyo uende ukasome upate kuijua zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, ugomvi wangu mimi kuhusu suala la ajira kwa vijana. Mhe. Mwenyekiti, ajira zipo lakini tuseme kuwa Serikali haijajipanga katika kuwatafutia vijana ajira hizo. Mhe. Mwenyekiti, ukanda wetu umezungukwa na mahoteli kama ninavyosema Serikali imeleta sera hii kwa nia nzuri ili kuondoa ukali wa ajira kwa vijana. Lakini hatujawa *serious* katika kuwatekelezea wajibu wao.

Mhe. Mwenyekiti, wanafukuzwa vijana wetu vibaya sana kwenye mahoteli. Mhe. Mwenyekiti, wanafukuzwa vijana kwa sababu ndogo tu lakini watetezi wao wakuwa wadogo sana. Lakini nishukuru kitengo cha nasaha ya sheria cha Idara ya Kazi wanasaidia kwa ukali wao akiwemo yule msimamizi wao ambaye anajua sheria na yeye anasaidia vizuri kwa kuwaokoa vijana na kuwarejesha kwenye kazi au kulipwa haki zao.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri kwa mfano Jimbo langu la Kitope kina mama wameitikia sana katika kuwekeza vikundi hasa ile Vikundi

vya Kufuli naomba sana Mhe. Waziri ufanye siku maalum uje kuona kina mama walivyoshamiri kutafuta fedha za kujikimu wao wenyewe.

Kwa kumalizia Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana nilipiga kelele sana suala la benki ya kina mama. Kina mama ilikuwa mnipe hongera benki hii niliipigia debe sana ili kina mama waondokane na ukali wa umasikini. Mhe. Mwenyekiti nimeona tayari taa ya kijani inaanza kuwaka kuwa Benki hiyo kwa kina mama itakuwepo kwa wakati wowote.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir amechangia na mimi naongeza nyama. Mhe. Mwenyekiti, tumeambiwa fedha zimelipwa kidogo lakini tunaomba Serikali kwa makusudi ifanye hicho kitu kwa makusudi kuwaokoa kina mama wasihangaike hangaike hatari hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la Skauti suala hili nimpongeze sana Mhe. Waziri ametoa kibali wale waliokuwa na moyo wa kuifuatilia Skauti na kuifufua ametoa barua. Lakini la kunisikitisha barua tumepeleka Idara ya Elimu mpaka leo hii hatujapata majibu, tena wametufanyia dharau kubwa sana. Maana hata lile jibu la kutwambia "nyoko!" wameshindwa kusema. Hili ni moja ambalo wametudharau tena nasema kabisa sitoiunga mkono Wizara ya Elimu kwa tabia hiyo waliyotufanyia. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono asilimia mia kwa mia bajeti hii. (*Makofi*).

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na nimshukuru pia Mhe. Waziri kwa jinsi alivyowasilisha hotuba yake jana jioni, hotuba ambayo imejaa takwimu ambazo zimechambuliwa na bila shaka ni sahihi kwa maslahi na maendeleo ya Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuchangia hotuba hii nimuombe kidogo anielimishe tumezowea kuona kwamba kabla ya hotuba yake Mhe. Waziri alikuwa na utaratibu wa kutuwasilishia ripoti ya mwaka mara hii hatujaiona ripoti ya mtoto ya mwaka. Sasa naomba Mhe. Waziri atwambie kwa nini mara hii ameshindwa kutuwasilishia Barazani ripoti ya Mtoto ya Mwaka ili kuona halisi mtoto wa Zanzibar alivyo.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwenye ukurasa wa 122 kwenye Bajeti ya wizara ya mwaka jana na Makadirio ya mwaka huu. Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka mwaka jana nilisema kwamba fedha ilizotegewa kwa Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto ni milioni 20 kama shughuli za maendeleo ni fedha ambazo zisingeleta maslahi na ufanisi kwa Idara hii. Nilisema hayo mwaka jana lakini bahati mbaya Waziri wa Fedha akajibu kwamba fungu hili limewekwa kama ni msaidizi lakini ziko fedha Wizara ya fedha zitasaidia.

Sasa ushahidi wa hili ni huu hapa kwamba mwaka jana Idara ya Wanawake na Watoto ilitengewa fedha za Serikali milioni 20 hadi mwezi Machi Mhe. Waziri anatwambia zimeingizwa milioni tano ni sawa sawa na asilimia 25 ya fedha za mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, huu ni ushahidi kwamba Serikali haiko makini katika kuwatetea wanawake na watoto. Fedha zilizotengwa mwaka jana ni milioni 20 lakini zilizoingizwa hadi Machi ni milioni 5. Hii ni ushahidi wazi kwamba Serikali haina ukweli, haina nia hasa ya kuwatetea na kuwalinda wanawake na watoto kama ilivyo katika maandiko mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nililihoji mwaka jana ni Idara ya Maendeleo ya Vijana. Serikali ilitenga milioni 50 lakini hadi Machi mwaka huu zimeingizwa milioni 16. Sasa najiuliza ni jinsi gani maendeleo ya vijana yatafikiwa ikiwa fedha zilizotengwa ni milioni 50 lakini zilizopatikana ni milioni 16.

Mhe. Mwenyekiti, nimeanzia hilo kuna kumdharau kumlinda mtoto au kumlinda mwanamke maana yake unawaambia wahisani wakulelee watoto wako. Unapotoa mwanya wahisani kuchangia fedha nyingi maana yake unawaambia wahisani sasa waweke masharti mazuri kwa maslahi yao jinsi ya kumlinda, kumtetea na kumlea mtoto wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kuna msemo unaosema kwamba "*aliyekufadhili ndio bwana wako*". Ikiwa fedha hizi tumewaachia wahisani ndio wachangie maendeleo ya watoto, wachangie maendeleo ya wanawake, tumewaachia wahisani wachangie kwenye maendeleo ya vijana maana yake pia tunakubali kwamba wahisani watoe masharti juu ya malezi na makuzi ya vijana wetu.
Mhe. Mwenyekiti, kwa mtizamo wangu mimi hapa ndio inaanzia athari ya malezi ya watoto wetu, kwa nini mzungu alete pesa zake asitwambie mtoto huyu avae nguo kiasi hichi, mtoto huyu usimpige na usimuadhibu, atasema hivyo kwa sababu ndiye aliyechangia maendeleo ya mtoto huyu, ndiye aliyechangia maendeleo ya vijana na ndiye aliyechangia maendeleo ya wanawake.

Mhe. Mwenyekiti, niiombe Serikali sana kwamba kama wana nia ya kuweka malengo mazuri kwa Wazanzibari basi wakubali vile vile kuweka fedha za kutosha kwa ajili ya Maendeleo ya Watoto na Maendeleo ya Wanawake na maendeleo ya Vijana. Mhe. Mwenyekiti, muda mchache suala la Maadili na Ustaarabu wa Wazanzibari utaondoka kwa sababu anayekufadhili ndiye anayeweka masharti ya fedha zake.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya pili ambayo nataka nichangie ni hoja ya ajira mpya na kustaafu. Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kitabu hichi Mhe. Waziri ametuonesha kwamba wameajiri na kuhamisha ajira mpya 12. Lakini waliofariki na kuacha kazi na kustaafu ni watu 16 maana yake nini. Maana yake tumeajiri 12 lakini tumewatoa 16 maana yake wizara imepoteza watu 4, kwa tafsiri ya haraka haraka hakuna ajira iliyofanywa kwa sababu hawa 12 wamechukua nafasi za watu 16, wizara ina mapungufu ya watu 4.

Mhe. Mwenyekiti, wizara isonekane kwamba imeajiri lakini na ijulikane kama wizara imepoteza watu 4 baada ya 12 waliokuwa nao. Mhe. Mwenyekiti, hili naomba Mhe. Waziri alione kwamba hakuongeza ajira badala yake amepoteza ajira katika Wizara yake kwa sababu ameajiri 12 ametoa watu 16. Mimi ningefikiria Mhe. Waziri angeajiri zaidi ili akachukua nafasi 16 ambazo amezitoa katika wizara yake.

Mhe. Mwenyekiti, zimeelezwa hapa kesi za udhalilishaji zimeongezeka kwa kasi mno Unguja na Pemba na dalili za kupungua Mhe. Mwenyekiti hakuna, kwa sababu Serikali haijawa makini kudhibiti kesi hizi za udhalilishaji. Wenzetu wa Wizara ya Ustawi wanaendelea kuratibu, wanaendelea kushajihisha lakini bila ya fedha na vitendea kazi wataendelea kushajihisha lakini hakuna punguzo la kesi hizi za watoto.

Mhe. Mwenyekiti, niliwahi kushauri mwaka jana kwamba baada kufungua mahakama za watoto isingetosha kama hatuweka mawakili maalum na sheria maalum kwa ajili ya kesi za watoto.

Mhe. Mwenyekiti, naendelea kushauri kwamba Serikali imefungua mahakama za watoto, lakini Serikali ikubali kuwaajiri wanasheria maalum kwa ajili ya kesi za watoto. Ili wanasheria hawa waweze kufanya kazi masaa 24 kwa ajili ya maslahi ya watoto. Vyenginevyo mahakama zetu basi kesi hizi zitaendelea kuongezeka na wala hakuna kesi ambayo itapungua. Nashauri kwa nia safi kabisa kwamba Serikali ikubali kuajiri wanasheria maalum kwa ajili ya Mahakama za Watoto ili waweze kuwa ni mawakili wa wizara hii kwa maslahi ya watoto.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hili kwa sababu hatuoni kama kuna nia thabiti na Serikali ya kupunguza kesi hizo. Kwa hivyo, mimi naamini kwamba tukiajiri wakili maalum kwa wizara hii kwa ajili ya watoto basi wao watakuwa na kazi maalum ya kusimamia maslahi ya watoto baada ya kumwachia Mwanasheria Mkuu au Ofisi ya *DPP* kushughulikia kesi ile. Mhe. Mwenyekiti, naliomba hili kwa nia safi ili tuweze kupunguza suala hilo.

Mhe Mwenyekiti, Idara ya Mipango Sera na Utafiti imeleezwa hapa kama inafanya majukumu yake na imetengewa fedha na imetekeleza. Lakini mimi napata mashaka Mhe. Mwenyekiti, kwamba kama tunataka maendeleo ya kasi hatuwezi kuwa na mpango na utendaji wake miaka 5. Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri asimamie sheria ile ya kuanzisha hifadhi ya wazee. Wazee wanaendelea kudhalilika, kuendelea kuwa omba omba lakini tatizo ni sheria hakuna.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana mimi Mhe. Waziri alinipeleka *Mauritius* na kwa sababu nchi ile ilikuwa na tatizo la wazee wengi, Waziri Mkuu wa nchi ile alitoa agizo la kuthamini sheria ya hifadhi ya wazee ndani ya wiki mbili, kwamba Serikali ilimuagiza Waziri kwamba ikamilishe sheria ndani ya wiki mbili, Zanzibar tunazungumza suala hili miaka 5. Ningemuomba Mhe. Waziri akajenga hoja kwenye Baraza la Mapinduzi kwamba sheria hii ya hifadhi ya wazee ikamilishwe haraka.

Baada ya kuwa hadithi ya miaka mitatu, minne na mitano. Wenzetu wenye nia safi wamefanya ndani ya wiki mbili na inawezekana wataalamu wapo, wanasheria wapo, jambo hili ndani ya wiki mbili. Baada ya kuwalaumu kwamba wanaomba wataomba, nani ambaye hana maslahi, hana nguo asiombe ataomba. Kwa hiyo, baada ya kuwa hadithi na kuwalaumu wazee kwamba wanaomba Mhe. Waziri ningekushauri usimamie suala hili ndani ya wiki mbili likamilike na linawezekana.

Zanzibar tuna tatizo la urasimu kama jambo dogo lakini linakwenda miaka mitatu, minne. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri najua kama ana nia safi lakini ajenge hoja Serikalini kwamba jambo hili limalizike haraka iwezekanavyo isiwe hadithi ya miaka mitatu au minne, wenzetu wanafanya jambo hili ndani ya wiki mbili, limekamilika na sasa watu wanaendelea kuishi vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri tuliwahi kuambiwa hapa kwamba wameanzisha Dawati la Jinsia Mawizarani. Je, nini hatima ya madawati yale bado yapo wanashirikishwa au wametupwa, na kama yapo nani anasimamia maslahi ya Dawati zile kwa maana ya fedha na rasilimali watu.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hayo kwa sababu nina wasi wasi kama Madawati pengine yapo lakini hana nyenzo au wizara husika haziwashughulikii. Kwa hiyo, Mhe. Waziri labda unielimishe haya Madawati ya Jinsia katika Mawizara mbali mbali yanafanya kazi na nani anayasimamia kiutendaji katika wizara mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, jengine mimi nimpongeze tu Mhe. Waziri Ofisi yake Afisa Habari anafanya kazi nzuri sana. Wizara nyingi za Zanzibar hazina Maafisa habari, wana Maafisa Habari jina tu lakini hawawatumii. Lakini Wizara hii ya Wanawake na Watoto ina Ofisa Habari ambaye anatumika na anafanya ufanisi mzuri. Mhe. Mwenyekiti, niombe Wizara mbali mbali waige kwa Mhe. Waziri wetu huyu kwamba wamemtumia Ofisa Habari Wizara ndiye Ofisa atakayetoa taarifa za wizara ambazo ni sahihi na za uhakika kwa ajili ya maendeleo ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, binafsi nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwa kumuandaa na kuandaa kitengo hiki cha Ofisa Habari ambacho kinafanya kazi vizuri na kwa ufanisi wa hali ya juu.

Jambo jengine nilisema mwaka juzi na naomba niseme tena kwamba wizara hii inasimamia vituo vya kulelea watoto mbali mbali. Nikawashauri kwamba lazima waweke *Data Base* maalum kwa ajili ya watoto wale ili Mzanzibari popote alipo ajue kwamba Zanzibar ina watoto wangapi wanaolelewa chini ya wizara hii. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aandae haraka sana *Data Base* ya watoto wanaolelewa na wizara hii ambao watakuwa wanajulikana popote.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ametuonesha malalamiko ya wanawake. Amesema kwamba kuna wanawake 26 wamedhalilishwa Unguja na 63 Pemba kwa maana ya Talaka kupigwa na mambo mengine. Mhe. Mwenyekiti, mimi niiombe wizara ifanye utafiti na wanaume wangapi wanaodhalilishwa. Mhe. Mwenyekiti, tumegundua sisi kwamba wanawake wengi wanatumia fedha kudai talaka. Kwa hivyo na wizara hii ifanye utafiti na wanaume wangapi wanaachishwa na wake zao bila ya taarifa. Mhe. Mwenyekiti, wanaume wengine ni wanyonge mwanamke mwenye uwezo kidogo basi yuko tayari kutoa fedha ili apate talaka na hayo yapo tumeyashuhudia.

Mhe. Waziri nikuombe hii Wizara ya jinsia na wanaume muwafanyie haki uwalinde kwa kuwafanyia utafiti wangapi wanakataliwa bila ya sababu ili tuweze kujua kwamba jinsi gani wanawake wanadhalilisha wanaume. Lakini hili ilivyo kama kwamba wanaume ni makatili wanawaonea wanawake tu, lakini na wanawake wanawaonea wanaume wanapigwa na wengine wanabakwa hivyo hivyo na wengine wanakataliwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikuombe sana sisi kama Wawakilishi tumegundua kuna wanawake wanatoa fedha kudai talaka bila ya msingi, kwa hivyo nikuombe ufanye utafiti ili tujue wanaume wangapi wanadhalilishwa na pengine hao wanaobaka wamekataliwa, kwa hivyo wanaamua sasa kuingia kundini.

Mhe. Mwenyekiti, mimi baada ya hayo niunge mkono hotuba hii na niwaombe wenzangu wasipige buti. Hii ni wizara ambayo naifahamu ina nia nzuri, ni wizara ambayo bila ya kuficha ukweli kwamba ukilinganisha na wizara zinazoongozwa na wanaume basi ni tofauti sana na hii inayoongozwa na mwanamke na huo ni ukweli. Na mimi ningekuwa ni kiongozi wa nchi hii ningeshawishika zaidi kwamba wanawake wanaweza wa Zanzibar kuliko wanaume. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe pamoja na kwamba tulisema kwamba saa sita mwisho wa kuchangia lakini idadi ya wachangiaji bado iko kubwa. Kwa hiyo, kutokana na umuhimu wa Wizara hii tunaendelea kumkaribisha Mhe. Abdi Mossi Kombo na baadae ni Mhe. Salma Mussa Bilali. (*Makofi*).

Mhe. Abdi Mossi Kombo: *Bismillahi Rahmani Rahiim*. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniruhusu na mimi kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii Wanawake na Watoto ikiwa ni Wizara yangu katika kamati yangu.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijachangia ningeomba nitoe taarifa moja kwa ndugu zangu wale wanaume wanaotudhalilisha sisi wanaume tunapowakuta kule njiani wamesuka nywele. Sasa wale mimi nasema ile ni kazi ya wanawake sio ya wanaume, waachie wanawake kazi ile. Kwa hivyo, mimi naiomba serikali iunde tume maalum ya kuangalia vijana wa kiume wanaojidhalilisha kwa kujifanya wanawake, wanatutia aibu. Zanzibar sio tabia yetu na sio utamaduni wetu wanaume kujifanya wanawake.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naanza kuchangia nikianza na ukurasa wa 39 ibara ya 85 kuhusu maendeleo ya wanawake na watoto. Mhe. Mwenyekiti, akina mama wetu hawa ndio wanaotuhudumia sisi wanaume, sisi wanaume na watoto bila ya akina mama hawa basi hata tusingepata ukubwa wala maendeleo mazuri. Lakini akina mama baada ya kutuzaa sisi wanatukogesha na kutufanyia kila huduma, hata chakula mama anaweza akasamehe lakini akampa mtoto wake. Kwa hivyo, naiomba wizara ya ustawi wa jamii ikiongozwa na mama Zainab ni mwanamke shujaa, ni lazima awafikirie akina mama kwanza kuwapa elimu tena kuwakusanya pamoja ili kuwawezesha kwa makusudi kuwapatia miradi mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto hivi sasa ina jukumu kubwa sana, la kuwakusanya kina mama, kuwapa miradi na kuwakopesha kina mama fedha ili wajiendeleze. Sasa hivi kina mama wamekuwa wengi sana na wengi wamekuwa wajane, na wanapoachwa wanaachwa na watoto watano, sita au saba, akina baba

wanawakimbia watoto wale wanabakia kina mama kuwachukua watoto. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri afanye juu chini awakusanye kina mama na awawezeshe na hii benki ya wanawake, nakumbuka mwaka jana tuliambiwa kunataka kufunguliwa benki za kina mama. Kwa hivyo, benki hizi zifanye kazi na wakopeshwe kina mama fedha.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 32 kuhusu maendeleo ya vijana. Mhe. Mwenyekiti, tuna vijana wetu wengi sana hivi sasa wamesoma, hawana kazi na wanazururа ovyo. Kwa upande wa majimbo yetu kama kule Matemwe kuna mahoteli mengi sana, kama alivyosema hapa Dk. Mshimba hapa kwamba tuna mahoteli mengi sana, lakini sasa hivi mahoteli yale yamevamiwa na wageni. Vijana wetu wazaliwa wa Kimatemwe wanapokwenda katika mahoteli wanaambiwa hawakusoma, sasa hatujui ni elimu gani ambayo inatakiwa ya kufanya kazi za mahoteli.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naiomba wizara hii wakati akimaliza bajeti hii, mimi nitamuomba Mhe. Waziri nimchukuwe Matemwe nikamtembeze katika mahoteli ili tuwaangalie vijana wa Matemwe mmoja baada ya mmoja. Kwa sababu vijana ni wengi hivi sasa na wameshatuzidi. Sera yetu ya mahoteli ni kweli mahoteli yapo, lakini vijana wetu wa Kizanzibari hawapati kazi za mahoteli wanaambiwa hawakusoma, kwa hivyo hii inachangia hata hii omba omba inakuwa nyingi.

Mhe. Mwenyekiti, ukienda kule shamba vijana wote wanajua sasa hivi kama hatukupata kazi za mahoteli tuelemee mjini, wakija mjini nako kuna vijana zaidi ya mara 20 sijui waende wapi. Kwa hivyo, hili tatizo kubwa la ajira linatupata kutokana na kazi zetu ambazo zinazidiwa na wenzetu wageni, vijana wetu wanazikosa hasa katika mahoteli. Kwa hivyo, na sisi kule mashamba hakuna viwanda vya kuingia katika makaazi isipokuwa mahotelini.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri ningekuomba baada ya bajeti afanye ziara rasmi aje Matemwe niko tayari kumtembeza, ili tukahakikishe kwamba ndani ya mahoteli yetu vijana wa Kimatemwe wanapata ajira.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa 8 kuhusu omba omba. Mhe. Mwenyekiti, nikirudi nyuma katika *Hansard* yetu, katika mwaka 1964 Mhe. Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Mapinduzi ya Zanzibar, kitu cha kwanza alichokiona ili kupunguza matatizo ya nchi hii ni kujenga viwanda vidogo vidogo.

Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka Kaskazini 'A' kulikuwa na Kiwanda cha Sukari, watu wa Kaskazini wote walikuwa wakifanya kazi pale, hawaji mjini. Tukija katika wilaya ya mjini kulikuwa na viwanda; cha viatu, cha sigara na

viwanda vidogo vidogo pale amani vinafika 25. Viwanda vile vilikuwa vikichukua kina mama na vijana wengi sana, lakini ilipofika miaka ya 1980 huko basi viwanda vile vyote vimekufa. Sasa idadi yote ile kubwa iliyokuwa ikifanya kazi kwenye viwanda vile na hivi sasa imeshazaana haina pa kwenda, kwenda kwake sasa hivi akina mama wale wadogo wadogo wenye wari ndio sasa wakubane, akikujua Mheshimiwa basi anakwambia mimi tokea jana sijala au tokea juzi sijala, haya utamfanya vipi, hana pa kwenda kwa sababu hakuna kiwanda hakuna chochote.

Kwa hivyo, naiomba Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto hivi sasa ifanye sensa kwa makusudi hasa ili waandikwe vijana wote ambao hawana kazi ya kufanya, muhakikishe mnawapatia ajira, wapatiwe nyanja za kufanyia kazi, kama si hivyo itakuwa omba omba hapa haiishi. Mhe. Mwenyekiti, vijana wale wakiamka asubuhi waende wapi? Wakati viwanda vilipokuwepo hapa ikifika asubuhi saa 12:00 magari yanawachukua na kuwapeleka viwandani. Sasa hivi badala ya magari kuwachukua na kuwapeleka viwandani wanakwenda kurundikana Darajani, mwisho wake wanavuta unga kwa sababu hawana kazi ya kufanya, kutwa wanakaa. Lakini kijana ikiwa yuko kiwandani saa 24 atavuta unga, hawezi akavuta unga kwa sababu kazi anayo ya kufanya, vijana wanavuta unga kwa sababu hawana kazi ya kufanya.

Kwa hivyo, naiomba serikali irejeshe sera ya viwanda Zanzibar ndio tutapunguka na omba omba. Siku zote Mhe. Mwenyekiti, nasema katika Baraza hili kwamba Zanzibar kama haijaleta sera ya viwanda, hatuwezi kuendelea na Mwenyezi Mungu anatujaalia tunakwenda katika nchi mbali mbali, tusome katika nchi za wenzetu wanafanya utaratibu gani. Lakini bado sisi hatujaweza kuleta sera ya kuwaokoa vijana wetu katika nchi hii. Nchi bila ya viwanda haiendi.

Kwa hivyo, naiomba serikali na wizara hii ihakikishe wanawake wanapatiwa mikopo ili kujiendeleza na maisha yao. Mhe. Mwenyekiti kwa kuheshimu wakati wako, mimi naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia, pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Matemwe wananisikia. Ninahakikisha Mhe. Waziri akija Matemwe tutampeleka katika mahoteli ili ahakikishe vijana wa Matemwe hawamo kwenye mahoteli, ili wapatiwe kazi katika mahoteli. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi).*

Mhe. Salma Mussa Bilali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako hili tukufu na kuchangia hotuba hii angalau kwa dakika tatu.

Mhe. Mwenyekiti, na nimpongeze kwa dhati kabisa mama Zainab, Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto, kwa uwasilishaji wake wa hotuba hii, hotuba ambayo aliiwasilisha vizuri, ilikuwa na mvuto na hata kama ulikuwa unasinzia basi utaamka ili kumsikiliza mama jinsi alivyokuwa akiwasilisha. Mama Zainab nakushukuru sana.

Pia niwashukuru na niwapongeze watendaji wako kwa kuitayarisha hotuba hii na baadae wewe kutuwasilishia. Mhe. Mwenyekiti, nianze katika kuchangia bajeti hii kwenye suala la udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia katika kiambatanisho nambari 3, wenzangu wameshachangia lakini na mimi natilia mkazo, kuna jumla ya udhalilishaji uliofanywa ni 1,005 na namba hii sio kwamba ni hawa tu, wako wengi. Hawa ndio waliofuatiliwa na kuripotiwa, lakini wako wengi ambao hawakuripotiwa katika kitabu hiki. Mhe. Mwenyekiti, hali hii ni ngumu na ni mbaya sana na kila siku tukija hapa kuchangia tunalisemea kila mwaka, lakini suala hili badala ya kupungua kila kukicha linazidi. Nadhani suala hili linazidi kutokana na kutokuwa na adhabu za kuwakomesha hawa ambao wanafanya masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, inauma sana na hasa sisi wanawake inatuuma sana kwa sababu ndio wazazi, sisi ndio tuna uchungu hasa wa hawa watoto na hawa wanaotufanyia haya ni wanaume, ni wazazi lakini wao hawana uchungu wa haya na wanafanya hivi kwa sababu hakuna adhabu ya kuwakomesha kufanya suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani labda kuwe na mkakati maalum, sheria ichukue mkondo wake. Kwa sababu linapotokezea tatizo kama hili, kubwa inasemekana hakuna ushahidi. Tuseme mtoto amefanyiwa udhalilishaji, atakusanyiwa mijanadume pale ataambiwa haya mtambue yupi aliyekufanyia, atamtambua huyu. Ataletewa siku nyengine atasema ni huyu huyu, lakini bado kesi itaambiwa haina ushahidi na baadae mwanamme yule anaachiwa huru. Kipindi kinachofuata atafanya tena na tena na hili suala badala ya kukoma litakuwa kila kukicha linaongezeka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani Mhe. Waziri kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kuwekwe utaratibu wa kutiliwa mkazo wa kupatikana hii mashine ya *DNA*, labda inaweza kusaidia katika kutoa ushahidi kamili wa suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba wizara hii ikishirikiana na Wizara ya Afya, iandae semina maalum ikiwashirikisha madaktari wa kitengo cha *One Stop Centre*, askari wa upelelezi wa kesi za ubakaji, ustawi wa jamii, ZAFELA, waandishi wa habari na mahakama. Wapewe semina maalum kwa pamoja ili

kuweza kuzungumziwa suala hili kwa vizuri, ili zinapokwenda kesi baina ya mahakama na askari ziweze kushughulikiwa ipasavyo na ziweze kuchukuliwa hatua ipasavyo.

Hatua zinazochukuliwa isiwe tu mwanamme ameshabainika kuwa amembaka mtoto, kama walivyosema wenzangu kuwa anafungwa miezi tisa. Mhe. Mwenyekiti, miezi 9 sio adhabu. Mimi nadhani hii sheria tuifanyie marekebisho, yeyote atakayethibitika kwamba amemdhalilisha au amembaka au amempa mimba mtoto halafu baadae anakataa, basi kuwe na adhabu kali ya miaka labda kuanzia 30. Uongo miaka 30 pengine ataishia kufia jela au hata akitoka basi hatofanya tena na wale wengine wataogopa sasa, wataona hapa nikifanya hivi nikigundulikana kuanzia miaka 30 jela nitafia jela, nitakoma. Mhe. Waziri naomba uchukue juhudi ya makusudi ili kurekebisha sheria na kuwekwa sheria kali, ili hawa wanaofanya udhalilishaji waweze kukomeshwa.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ninalotaka kuchangia, huku nikijali muda wako ni suala la vijana. Mhe. Mwenyekiti, vijana ni taifa la kesho, tukiwawezesha vijana tutajenga vyema taifa linalokuja. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, pamoja na juhudi zako kubwa ambazo unachukua kuwasaidia vijana, basi naomba uendelee na juhudi hizo kuwasaidia vijana ili wasikose muelekeo.

Mhe. Mwenyekiti, vijana wako wengi na vikundi viko vingi. Katika kitabu chako kuna baadhi ya maeneo yamepata misaada na mikopo zaidi, lakini kuna baadhi ya maeneo hayajaonekana kabisa. Sasa sijui ni kigezo gani Mhe. Waziri ambacho kimetumiwa kuwafanyia utafiti hawa vijana na kuvifuatilia hivi vikundi na sehemu nyengine kukawa na idadi kubwa ya misaada na sehemu nyengine kukawa na idadi ndogo, na sehemu nyengine hakuna misaada kabisa wala mikopo iliyotolewa kwa vijana. Mhe. Mwenyekiti, ningeomba kuwe na uwiano wa kutoa misaada na mikopo, kufanya utaratibu wa makusudi kupitia ma-*star* wetu wa vijana, wanawake na watu wa wilaya kwa kupitia wao, kufanya utafiti wa makusudi ili kuwe na uwiano katika utoaji wa mikopo na misaada kwenye vikundi vya vijana pamoja na vikundi vya kina mama.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kuhusu wazee. Mhe. Waziri nikupongeze sana kwa juhudi zako ambazo unachukua kuwasaidia wazee wa Sebleni, Welezo na wale wa maeneo ya vituo vile vya Pemba. Lakini Mhe. Mwenyekiti, wazee ambao wanasaidiwa ni wale ambao wako mjini, lakini vijijini kuna wazee wengi Mhe. Mwenyekiti, hawajiwezi, wana matatizo, hawana watoto wa kuwasaidia, wanasaidiwa na majirani tu.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Mwenyekiti, kufanywe utafiti wa makusudi wa kuwafuatilia na wazee wa vijijini. Nashukuru kwamba ule msaada wanapewa umetoka kwenye shilingi 500 umekwenda kwenye shilingi 5000, lakini sasa hiyo haitoshi kwa maisha ya leo. Mhe. Waziri naomba ufanye utafiti wa makusudi ili wazee wa vijijini nao wana haki ya kuhudumiwa na kusaidiwa. Ikiwezekana kama yalivyojengwa maeneo ya Sebleni, Welezo na sehemu nyengine, basi na kule vijijini watafutiwe maeneo wajengewe na wale kule vijijini wawekewe majumba wasaidiwe kama wanavyosaidiwa wazee wa mjini.

Mhe. Mwenyekiti, najali sana muda wako, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.*(Makofi).*

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi ya kuweza kuchangia machache katika wizara hii. Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia leo hii kukutana hapa na kujadili mambo yetu katika Wizara hii ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, naanza na ukurasa wa 8 ambao unazungumzia wizara kusimamia uundwaji wa kamati 11 za kupambana na udhalilishaji wa kijinsia. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kamati hizi zimeundwa, lakini kila siku tunashuhudia masuala haya yanaendelea, sijui kwa nini kamati hizi ziundwe halafu tusione matunda yake yanayoshughulikia masuala haya ili kuhakikisha yanapungua na yasiendelee.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri nimuombe kamati hizi alizoziunda zifanye kazi kikamilifu, ili tujue namna gani watu hawa wanapungua kufanya mambo haya ya udhalilishaji wa watoto. Mhe. Mwenyekiti, nakwenda katika suala la watoto wenye mazingira magumu. Suala hili katika nchi yetu lipo kubwa hasa katika Wilaya ya Micheweni na kwa Unguja kwenye Wilaya ya Kaskazini 'A'. Lakini Mhe. Mwenyekiti, watoto ambao mmewasaidia ni shilingi 100, 500, 1000, ambapo utazitumia kwa siku moja tu, siku ya pili haipo.

Kwa hivyo, nitoe ushauri kwamba kwa kuwa sasa hivi serikali imeandaa mfuko wa Zaka, basi ungeelekezwa zaidi katika watu hawa wenye mazingira magumu. Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu unakwenda kijumla jumla tu.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee hapo hapo kuhusu watoto, kwa sababu wizara hii inahusika na watoto hasa vijijini kuna baadhi ya watoto wanajihusisha na ajira. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri alifuatilie hili ili ajue ni namna gani ya kulitatua ili watoto hawa waondokane na kufanya kazi hizi za ajira au biashara ndogo ndogo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu nije kwenye sehemu ya wazee. Kwa kuwa serikali imeamua kuwasaidia wazee, basi natoa ushauri kwamba wazee hasa wa vijijini wanapatiwa shilingi 5,000 kwa mwezi, pesa hizi ni kidogo sana. Sasa nimuombe Mhe. Waziri angalau wapewe shilingi 30, 000 kwa mwezi ili na wao wajihisi serikali yao inawajali wazee hao.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nataka kuchangia kwenye benki ya wanawake, japokuwa tunaambiwa tukichangia tusirejee rejee, lakini kila tukirejea tukiwa wengi ndio tutafanikiwa. Mhe. Mwenyekiti, benki ya wanawake kila siku tunaambiwa iko katika mipango, bado inapangwa, sasa sijui lini benki hii itaanzishwa.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kwa kuwa duniani mote wanawake ni wengi na hata motoni tumeambiwa tutakuwa wengi, afanye jitihada zake zozote ili benki hii ianzishwe haraka iwezekanavyo ili tuondokane na umaskini tuliokuwa nao, hasa kwa kuwa wanaume wanatuachia mizigo ya watoto wanapotuacha.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na mchango wangu sehemu ya mikopo kwa vijana. Wizara yako imewapa vijana mikopo, lakini pia umewawekea mikakati ya kwamba kama watashindwa kulipa basi watoe fidia. Kwa maana hiyo kwanza kabla ya kuwalipisha, mimi natoa ushauri wangu, muwaite muzungumze nao, mkimuona mtu ni mgumu kulipa basi mtamuwekea ile mikakati migumu ya kutolipa.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 21 ambao unazungumzia kuhamasisha hali za kiuchumi, kiutamaduni na maendeleo kwa wanawake, vijana, watoto na wazee. Afisi ya Mhe. Waziri imesaidia kuboresha mfuko wa watu wenye ulemavu. Mhe. Waziri hapa nikupongeze sana kwa jitihada hii uliochukua ya kuwasaidia watu wenye ulemavu wanawake na baadhi ya SACCOS. Niwaombe Waheshimiwa Mawaziri wengine wachukue mfano kama huu kwa kumfuata Mhe. Waziri. Baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza naanza kwa kumshukuru Allah kwa kutujaalia kuwa wazima kwa siku hii ya leo. Vile vile namuomba Mwenyezi Mungu atuwezeshe kufungu Ramadhani yetu kwa kuifunga hasa, sio kushinda na njaa. Vile vile atupokelee ibada zetu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii. Pia napenda nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake kwa jinsi alivyoiwasilisha hotuba yake na watendaji wake wanavyotekeleza majukumu yao katika wizara.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitokuwa na mchango mkubwa, kwa sababu wenzangu wengi wameshachangia. Lakini naomba nitie baraka katika wizara hii. Mhe. Mwenyekiti, nina kumbukumbu katika bajeti ya wizara hii ya mwaka 2012/2013, kikao hiki kiliongozwa na Mwenyekiti, mwenzako ambaye ni Mhe. Mgeni Hassan Juma Mwenyekiti wa UWAWAZA. Vile vile aliyewasilisha ripoti ya kamati alikuwa ni Mhe. Amina Iddi Mabrouk. Pia makatibu wetu katika kumbukumbu zangu nakumbuka palikuwepo na wanawake mbele hapa na wale askari wetu alikuwemo mwanamke nafikiria ni mmoja au wawili. Nilitegemea Mhe. Mwenyekiti, utaratibu ule ungeendelea kwa wizara hii. Lakini nasikitika sana Mhe. Mwenyekiti, leo hii kuona Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto wanaowaongoza wote ni wanaume. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa kumueleza Mhe. Waziri kama elimu inahitajika kwa wanawake kujua haki zao. Kwa kweli nasema haya kwa kujua kwamba kuna baadhi ya maeneo ambayo yanaona wanawake hawana uwezo wala haki ya kuamua, kuchagua na hata kujipangia mahitaji yao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, haya ninayasema kwa ushahidi na ninamuomba Mhe. Waziri kwa kupitia wizara yake waandae vipindi katika *television* na redio kuwaelimisha wanawake wajue haki zao. Hali hii inaweza kusaidia sana kwa wanawake kujua haki zao na pia kukataa kuonewa, kwa sababu kumnyima mtu haki yake ni kumuonea.

Suala jengine ambalo nataka nilizungumzie ni kuhusu kunyimwa elimu kwa watoto wa kike. Mhe. Mwenyekiti, nachangia hili nikiwa na ushahidi, kwamba kuna baadhi ya wazazi kwa itikadi zao za kidini wanawazuia watoto wa kike kuwapeleka skuli. Kwa kweli hili ni tatizo, kwani itapelekea kuwa na wanawake wengi wasiojielewa katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kutokana na hali hii namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja kufanya majumuisho anieleze kwamba atawasaidia vipi watoto hawa kupata haki yao ya elimu.

Mhe. Mwenyekiti, ingawa umetuambia tusirudie, lakini suala la udhalilishaji wa watoto, basi kila mzazi ni lazima alitilie nguvu. Vile vile hapa Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri aangalie sana katika skuli zetu pamoja na madrasa zetu, kwani kunajisiwa kwa watoto kumeshamiri na imekuwa ni jambo la kawaida. Kwa kweli kama tusipoangalia, basi tutakuja kujikuta kwa muda mfupi tu nchi yetu ina watoto wa kiume wengi ambao ni wanaume jina tu. *(Makofi)*

Jambo la kusikitisha Mhe. Mwenyekiti ni kwamba vitendo hivi vimeshamiri na wala husikii wahusika wa vitendo hivi kukamatwa na hata wakikamatwa adhabu inachelewa kutolewa na wakati mwengine utasikia kama wazee wamepitisha suluhu. Mhe. Mwenyekiti, suala hili si la kupitisha suluhu na jambo hili si suala la wazee tu, isipokuwa ni suala la serikali kwa sababu aibu inapotokea si ya mzee tu hata serikali yenyewe.

Kwa hivyo, ushauri wangu Mhe. Mwenyekiti, hapa ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati zinapotokea kesi hizi wazisimamie wao pamoja na kwamba wazazi wapo, lakini wao wawe ni wahusika, kwa sababu hii wizara yake inashughulikia maendeleo ya vijana, wanawake na watoto.

Sasa katika kushughulikia sehemu moja iwe ni hapa kusimamia kesi zao, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, tumeshazoea kuona wazazi wana tabia ya kuoneana muhali. Kwa maana hiyo, namumba Mhe. Waziri kesi hizi wazisimamie wao.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie viambatanisho kwenye ukurasa wa 54 kiambatanisho Nam. 1. Mhe. Mwenyekiti, kiambatanisho hichi kinahusu ajira mpya, uhamisho, waliofariki, walioacha kazi kwa Unguja na Pemba. Kwa hivyo, kuhusu ajira mpya ni 7, ajira kwa njia za uhamisho ni 5, waliohamishiwa taasisi nyengine ni watatu, waliofariki ni watatu, waliostaafu ni 9 na walioacha kazi ni 1.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu hapa ni kuwa ajira mpya ni 12 ukiacha 7 za ajira mpya na wale watano waliopewa uhamisho kutoka wizara nyengine, lakini waliohama katika wizara kwa kufa au waliohamishiwa taasisi nyengine, walioacha kazi na waliostaafu ni 16.

Kwa hivyo, swali langu hapa ni kwamba wizara imeondokewa na wafanyakazi 16, lakini imeajiri wafanyakazi 12. Je, wizara hii baada ya muda mdogo itakuwa kweli ina wafanyakazi wa kutosha katika wizara, kwa sababu nilitegemea watatoka wizarani ni 16, lakini watakaoajiri ni 16 au na zaidi na walioajiriwa ni 12 na hivyo hapa sijui Mhe. Waziri atanieleza nini.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 55 kiambatanisho 1(b) kinazungumzia kuhusu wafanyakazi waliopatiwa likizo ya kawaida kwa mwaka 2012/2013. Wafanyakazi waliopatiwa likizo inaonesha ni wafanyakazi 138 na waliolipwa posho la likizo ya kawaida ni wafanyakazi 56. Sasa hapa namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, anifahamishe wale ambao wenye haki ya kulipwa hili posho la likizo walikuwa ni 56 tu na kama kuna ziada kwa nini hawa wengine hawakupatiwa posho hilo.

Vile vile kwenye ukurasa huo wa 56 kiambatanisho 1(c) kinazungumzia kuhusu mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Mhe. Mwenyekiti, mafunzo ya muda mrefu ni wafanyakazi 12 na mafunzo ya muda mfupi ni wafanyakazi 7. Lakini hapa swali langu katika mafunzo ya muda mfupi ni kwamba Pemba hakuoneshi kuwa na mfanyakazi hata mmoja. Kwa hiyo, sijui hawa wafanyakazi wa Pemba hawakutaka kupata haya mafunzo au wizara ilikuwa na sababu gani ya kuwa kule Pemba asitoke hata mfanyakazi 1 katika mafunzo haya.

Mhe. Mwenyekiti, hapa pia nilitegemea wakati hii wizara ni inayohusika hasa na mambo ya wanawake, basi nilitegemea katika wafanyakazi ambao watakuwa wamepewa elimu wengi itakuwa ni wanawake. Lakini inavyoonesha hapa kwa mafunzo ya muda mrefu wanawake ni 7 na wanaume 7 na ya muda mfupi wanawake ni 2 na wanaume ni 5. Katika hali kama hii sijui Mhe. Waziri atatueleza nini sisi wanawake, kwa sababu yeye ni Waziri wetu na tunamtegemea kutusaidia katika mambo yetu.

Kiambatanisho chengine ni 2(b) nacho kiko kwenye ukurasa wa 57 kinazungumzia kuhusu misaada iliyotolewa na ofisi ya Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa misaada uliyoitoa. Lakini tumeona hapa 4 kuna vikundi vya *SACCOS* Pemba na fedha ambazo umetoa msaada na wala hatujui ni vikundi vingapi.

Sasa hofu yetu ni kwamba hivi vikundi vinalingana na hii gharama ya fedha ulizotoa na ikaja ikawa yale maendeleo yaliyokusudiwa hayakupatikana, kwa sababu mtu au kikundi kukipa msaada wa shilingi 10,000/= au 1,000/= haisaidii kitu. Kwa hivyo, ni vyema ilikuwa Mhe. Waziri atuoneshe angalau ni vikundi vingapi vilivyopata huu msaada, ili tuweze kujua kila kikundi kimepata asilimia ngapi.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa kuwajali wazee, lakini naomba aelewe kwamba wazee sio wale ambao wako Sebleni, isipokuwa tuna wazee wengi mitaani ambao wanahitaji misaada. Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wa kuweka utaratibu wa kuona na hawa wazee wengine, ambao ni wazee kama walioko kule, basi wanayo haki ya kupata misaada hii.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa jinsi anavyoiongoza wizara yake. Baada ya maelezo hayo nakushukuru na ninaunga mkono bajeti hii kwa niaba ya wanawake wa Wilaya ya Chake Chake kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Sasa kabla sijamkaribisha Mhe. Amina Iddi Mabrouk, ningependa nimsaidie Mhe. Mjumbe hata na sisi ndani tulipokaa tungekuwa na fahari tungemuona Mhe. Mgeni Hassan Juma amekaa kwenye kiti hichi leo.

Lakini kwa bahati mbaya amekwenda Dar-es-Salaam kwenye semina na baadhi ya Mawaziri pamoja na baadhi ya Waheshimiwa Wawakilishi kwa ajili ya kuhudhuria semina ndio maana sisi tumemshikia nafasi yake kwa leo. Kwa hivyo, *Inshaallah* mambo yatakuwa mazuri pengine kesho kama atawahi kurudi basi atamalizia na majumuisho. *(Makofi)*

Mhe. Amina Iddi Mabrouk na Mhe. Abdalla Juma Abdalla akae tayari.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii, ili niweze kuwa mmoja wa wachangiaji wa Hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, ambayo ni muhimu sana kwa taifa letu.

Vile vile nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika kuhakikisha kwamba vijana wetu, wanawake wenzangu wanakwamuka na matatizo mbali mbali yaliomo kwenye jamii yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu kwenye ukurasa wa 32 kuhusu uundwaji wa Mabaraza ya Vijana. Kwa kweli kama tunakumbuka sote Mhe. Mwenyekiti, kwamba kitabu hichi au maneno haya ambayo yanazungumza kwamba kuratibu uanzishwa wa Baraza la Vijana, sentensi hii ipo tokea kipindi cha mwaka jana. Matokeo yake Mabaraza haya mpaka leo bado hayajaanzishwa. *(Makofi)*

Hata hivyo, Mhe. Rais wakati alipokuwa akifungua Baraza letu la Wawakilishi alisema azma yake ya kuanzishwa Mabaraza haya ya Vijana. Lakini mpaka hii leo Mabaraza haya ya Vijana bado hayajaanzishwa na kuhusu hii uratibu kama tunakumbuka sote sisi na tukilinganisha na Tanzania Bara, basi sisi Zanzibar ndio tulioanza uratibu huu wa Mabaraza ya Vijana na baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wamezungumza. Kwa hivyo, inaonekana wenzetu hivi sasa wameshatuacha nyuma na kwamba wenzetu wanapiga hatua na sisi tupo pale pale. *(Makofi)*

Kutokana na hali hii, Mhe. Mwenyekiti namuomba Mhe. Waziri ambaye ni mama yangu wakati atakapokuja kufanya majumuisho, basi atueleze kwa ukamilifu tena kwa yakini kwamba Mabaraza haya ya Vijana yataanzishwa

lini. Mhe. Mwenyekiti, kusuasua kwa Mabaraza haya ya Vijana kunakwamisha maendeleo makubwa kwa vijana.

Sasa kama mabaraza haya yangekuwa tayari pengine vijana wetu wangepiga maendeleo makubwa katika nchi hii, lakini tumebaki tunalalamika sana kwamba vijana wana matatizo haya na yale. Lakini chombo ambacho watahakikisha kwamba vijana hawa wanakaa na kuzungumza matatizo bado hakijaungwa mpaka leo.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja basi atueleze vizuri na tusije kumpiga mabuti, kwa sababu inaonekana kwamba leo wanawake ndio wametawala kwenye chombo hichi. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la ubakaji wa watoto. Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wamezungumza sana suala hili na pengine inawezekana mkatuona tunarejea rejea, lakini naamini kwamba kurejea ndio kufanikiwa tatizo hili kuondoka. *(Makofi)*

Kwa mfano, tukiwa tunasikiliza vyombo vya habari ubakaji wa watoto kila siku na tatizo halijulikani kwa nini ubakaji wa watoto unaendelea. Kwa kweli sisi kama wazazi Mhe. Mwenyekiti tunaumia, tukiona kwamba watoto wetu kila siku wanabakwa, lakini kesi inapokwenda mahakamani ufumbuzi hauonekani, Mhe. Waziri kulikoni.

Vile vile huwa tunaambiwa ushahidi haupo na hichi chombo cha *DNA* mpaka leo hakijanunuliwa tatizo liko wapi, kwa sababu chombo kipo cha *DNA* ambacho kimefungwa Hospitali ya Mnazi Mmoja na chombo kile kiko robo bado hakijakamilika. Pia chombo kile hakioneshi uchunguzi hasa wa watoto wetu. Mhe. Waziri mtoto anapobakwa *specimen* inapelekwa Bara na inaweza ikakaa kwa muda wa wiki moja mpaka mbili na ushahidi hauonekani. *(Makofi)*

Kwa hali hiyo, naiomba serikali kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia kesi ya meli wakati ilipokuwa ikizungumzwa, basi serikali ilijipiga na hivi sasa meli iko njiani inatengenezwa na meli ile imegharimu mabilioni ya fedha na chombo hichi kwa mujibu wa habari kitagharimu shilingi milioni 600/=. Mhe. Mwenyekiti, meli yetu ni muhimu kwa wananchi kwa ajili ya kuwahudumia, lakini na watoto nao pia ni muhimu, kwa sababu kama ikiwa hatuna watoto bora meli ile ataipanda nani? *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tatizo la kifaa hichi ni kwamba serikali ikifuatilie, kwa sababu wananchi wanalalamika, watoto wanaendelea kubakwa na wala ufumbuzi haupatikani.

Jambo jengine labda nije kwa upande wa familia. Kwa kweli hivi sasa kuna tatizo sugu kwenye familia, yaani kesi za familia, uchunguzi unaonekana kwamba mtoto amebakwa, lakini hatimaye kesi zinachunguzwa na ushahidi unapatikana na baadaye unaambiwa familia zimekaa na imeonekana kwamba huyo mtu aliyembaka tuko kwenye familia moja na hivyo tunaoneana muhali. Mhe. Mwenyekiti, nadhani ni vyema wananchi tuipe ushirikiano wa kutosha serikali yetu. *(Makofi)*

Hata hivyo, utakuta familia wanasema hadharani kwamba maana yake mfanyaji ameshalipa fidia na amemlipa mtoto wetu shilingi 500,000/=, hivi kweli shilingi 500,000/= zinalingana na afya ya mtoto na hivi fedha hizi mzazi atatumia siku ngapi, wakati mtoto ameshaharibiwa maisha yake, yaani ameshafisidiwa mtoto kwa lugha nyengine. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri jamii, familia pamoja na wazee tushirikiane kuhakikisha kwamba hizi suluhu za mitaani tusizikubali. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni nimesikia kwenye vyombo vya habari kwamba baba amembaka mtoto wake na habari zikaenda mpaka katika vyombo vya sheria. Sasa baadaye unaambiwa wazee wamekaa, kwa hiyo baba amemlipa fidia mtoto shilingi 500,000/=. Kwa hivyo, mama na baba wanaomba kesi ifutwe, mama anaona kwamba mumewe atafungwa atamkosa mume ana hiari bora ampoteze mtoto, hivi kweli ni halali hali hii au ni haki ya binadamu? Kwa sababu mtoto naye anazo haki zake. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, naiomba serikali pamoja na wananchi kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, tuhakikishe kwamba tusilaghaiwe tu kwa mambo madogo madogo, lakini tunapoteza watoto wetu, kwa sababu watoto ndio taifa la hivi sasa na kesho. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie suala la omba omba. Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wengi wamelizungumzia suala hili na hivi sasa limekuwa ni hatari kwa jamii yetu na hasa kwa kuwatumia watoto. Kwa kweli hivi sasa imekuja *design* mpya, yaani wazee wanaomba kupitia watoto wetu. Kwa mfano, hivi sasa tutatoka kwenda Darajani pale Mhe. Mwenyekiti, basi unamkuta mama mtoto amemshika mtoto wake wa miaka 7 anapita naye kuomba na hivi mtoto tunamjenga vipi.

Mhe. Mwenyekiti, hatuioni *impact* yake kwa hivi sasa, lakini baadaye inawezekana ikaonekana baadaye. Lakini mtoto yule unapokwenda naye kuomba omba unamjenga ki-*psychology* kuwa omba omba ndio maisha ya kila siku au maisha yangu. *(Makofi)*

Vile vile mtoto yule baada ya kumjenga kuwa umuhimu wa kusoma na kujipatia elimu ndio muhimu kwake yeye, lakini badala yake tunamjenga mtoto yule kuwa omba omba ndio maisha yangu ya kuniendesha baadaye. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wakati wa bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria nilitaka nichangie kwenye Ofisi ya Mufti lakini sikupata nafasi. Kwa kweli siku hizi kuna mtindo mwengine mpya umejitokeza kwa Vyuo vyetu vya Madrasa, wakati tunapokuwa na mahitaji ya kuchangiwa katika vyuo kama vile kujengewa chuo au mashindano.

Kwa hivyo, tunawapa watoto au wanafunzi barua kuzirandisha kwenda kukusanya michango, utawaona watoto wale wanarandisha barua madukani na hata majumbani. Sasa baada ya mtoto yule kumjenga kuwa anakwenda madrasa kusoma, lakini mtoto yule tunamjenga kuwa kuomba ndio muhimu katika maisha. *(Makofi)*

Naomba niseme tena Mhe. Mwenyekiti, kwamba *impact* yake haionekana kwa hivi sasa, lakini baadaye inaweza kuonekana, yaani wakati pale mtoto anapokuwa ni omba omba. Kutokana na hali hiyo, basi niombe kwamba suala la michango ni la walimu wenyewe na wala sio suala la mtoto, isipokuwa mtoto mpe barua apeleke nyumbani kwao kwa mzee, kwamba mtoto akampe barua mama au baba yake barua hii kwa ajili ya kuchangia, hivyo mwanafunzi yule usimpe barua kwenda kusambaza mji mzima.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri kwamba suala hili ni hatari, basi ni vyema Mhe. Waziri akalisimamia kwa ukamilifu kulikemea kwa ukamilifu, kwa sababu suala hili ni hatari sana kwa jamii yetu, kwani tunawaharibu watoto, lakini tunawajenga kuomba.

Pia akinamama tunawabeba watoto wetu tunapita majumbani na halafu mtoto anaambiwa nenda nyumba ile pale kagonge na mama yule anakuwa amejificha, na halafu akishafika pale kwenye nyumba anagonga na kusema nimekuja kuomba kiasi fulani. Sasa kama mdadisi ndio unamuuliza umekuja na nani au umefikaje hapa nyumbani kwangu, yule mtoto anakuwa hasemi kwa sababu mzazi anakuwa tayari ameshamwambia kwamba usiseme kama umekuja na mimi.

Kwa hiyo, unapomdadisi yule mtoto au ukamwambia sikupi mpaka uniambie umefika vipi hapa na pengine yule ni mtoto wa miaka 7 au 6, basi mwisho hatimaye yule mtoto anakwambia nimekuja na mzee wangu yuko kule.

Mhe. Mwenyekiti, natoa wito kwa jamii kwamba tusiwatumie watoto wadogo katika suala zima la kuomba omba. Kwanza si utamaduni wetu wa kuomba na hivi sasa imekuwa tunaharibu silka na utamaduni wa Kizanzibari na pengine *Wallahi* ninaapa Mhe. Mwenyekiti, pengine kuna watu ambao hali zao ni mbaya sana majumbani, lakini hawatoki kuomba na wanakuwa wamekaa majumbani wametulia. *(Makofi)*

Hata hivyo, inawezekana wale wanaomba kila majumba huwezi kuamini jioni anaweza kuwa na shilingi 200,000/= mpaka 300,000/=, lakini asubuhi kukicha unamkuta tena mama yule anaomba, pengine unaweza ukajiuliza fedha zile alizozipata jana amezipeleka wapi? Kwa hivyo, huyu Mhe. Mwenyekiti, ameshajijengea utamaduni kwamba mtu maisha yake ni kuomba. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kupitia Baraza hili, kwamba akinamama tunajidhalilisha kupita kiasi. Kwa kweli kama una shida basi omba leo kesho usiombe na upumzike baada ya siku tatu, lakini unamkuta mama yule kila siku anaomba. Sasa pale anapoomba anakwambia kuna mwanangu nyumbani amejifungua anataka umpe na *share* ya yule mwanawe na huu sio utaratibu mzuri.

Namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba awaelimishe akinamama kwa sababu sote tuliopo kwenye ukumbi wazazi pamoja na akinamama. Hivyo, pale tunapoona akinamama wenzetu kwa kweli wanafanya matendo ambayo siyo, basi sisi tunaumia na tunajisikia vibaya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri kwa vile wewe ni Waziri mwanamke, Katibu Mkuu wako ni mwanamke na wengi Wakurugenzi wako katika wizara yako ni wanawake. Kwa hivyo, kupitia kwako naomba tufanye kazi hii na wala tusione tabu na tusiridhike kukaa ofisini tu, na siku moja tutie gari mafuta na tukatembee tuone na hasa kipindi hichi cha Ramadhani ndio utawafaidi na wala huwakuti wanaume wengi, isipokuwa wengi wao ni wanawake ndio wanaoomba omba. *(Makofi)*

Jengine kuhusu watoto tunawatumia katika kupara samaki.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, zingatia muda.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Mwenyekiti, nitajitahidi, lakini wizara hii leo tumeguswa wanawake zaidi kuliko wanaume.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, uliomba dakika 5 kwa ajili ya kuchangia.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Mwenyekiti, watoto tunawatumia sana katika kupara. Kwa mfano, kama utakwenda kwenye masoko utawakuta watoto Malindi, Soko la Darajani, Matemwe, Mwanakwerekwe utawakuta watoto wengi wanatumiwa katika kupara samaki, yaani baada ya ule muda mtoto yule anatumiwa katika kupara samaki awe yuko skuli anasoma, basi unamkuta mtoto yule yuko marikiti anapara samaki. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri kwamba alikemee jambo hili ili lisiendelee, kwa sababu tatizo hili linaendelea siku hadi siku. *(Makofi)*

Sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la Uanzishwa wa Benki ya Wanawake. Mhe. Mwenyekiti, naomba univumilie na hii itakuwa ndio *agenda* yangu ya mwisho. Kwa hivyo, naomba nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kumpongeza Mhe. Waziri kwa jitihada ambazo anachukua kuhakikisha kwamba benki inaanzishwa. *(Makofi)*

Kitabu cha Mhe. Waziri amezungumzia kwamba yumo katika harakati za kutafuta fedha na akipata fedha kama milioni 500,000,000/= au 600,000,000/=, basi inaweza kuanzishwa benki hii. Lakini mimi naamini kwamba Mhe. Waziri peke yake hawezi kuanzisha benki hii, hivyo ni lazima Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na serikali kuu kwa jumla isaidie, ili kuhakikisha kwamba Benki hii ya Wanawake inaanzishwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ningefurahi sana leo kama Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo angekuwepo akatusikia wanawake jinsi tunavyolalamika au tunavyotamani na sisi Zanzibar ianzishwe Benki hii ya Wanawake.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwa kweli tunajisikia vibaya kuona kwamba wenzetu wa Bara, yaani wanawake wa Tanzania Bara tayari wameshaanzisha Benki hii ya Wanawake na sisi Zanzibar ambapo wanawake tupo kidogo, basi mpaka leo Benki hii ya Wanawake haijaanzishwa.

Kutokana na hali hiyo, naomba Mhe. Mwenyekiti na ninaamini kwamba Mawaziri wapo na watampa salamu Mhe. Waziri wa Fedha, kwamba mumwambie Mhe. Waziri wa Fedha kuwa wanawake wote wamechangia suala zima la kuanzishwa Benki hii ya Wanawake. Kwa hivyo, tukijaaliwa mwakani Mhe. Waziri atakapokuja na bajeti yake basi *Inshaallah* iwe mambo

yameshakuwa mazuri na isiwe kila siku tunaona maandishi ya mchakato wa kuanzishwa Benki ya Wanawake, au tunao mpango ama tukipata fedha kiasi fulani benki itaanzishwa na hali hii inasikitisha sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile umenihimiza zamani, isipokuwa umenistahamilia kwa busara zako, na kwa vile na wewe unao wanawake wamekuzunguka, basi naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Sasa ni zamu ya Mhe. Abdalla Juma Abdalla na baadaye Mhe. Mohammed Mbwana Hamad na Mhe. Viwe Khamis Abdalla ajitayarishe.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi ingawa ni mwanamme kunipatia nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani umefanya busara, kwa sababu Mwenyezi Mungu anasema *"Arrijaalu Qawwaamuuna Alaa Nnisai"*, wanaume ndio wanaowasimamia wanawake. Kwa hivyo, si vibaya kuzungumza mambo ya wanawake na kwa busara hizo Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana kunipa nafasi hii na mimi niseme mawili matatu katika wizara hii ya mama yangu Mhe. Zainab Omar Mohammed. *(Makofi)*

Nikianza mchango wangu kwanza nataka nimpongeze kwenye ukurasa 15 *paragraph* ya 31 na leo nataka nipongeze tu. Mhe. Mwenyekiti, kwenye *paragraph* hii Mhe. Waziri anasema amewahamasisha wanawake 70 wenye sifa kushiriki katika mchakato wa kugombea nafasi za uongozi katika nyanja za siasa pamoja na utendaji. *(Makofi)*

Kwa kweli amefanya kazi kubwa, kwa sababu miongoni mwa watu ambao katika jamii yetu wanabakia nyuma nyuma sana ni hawa akina mama. Sasa juhudi yake hii ya kuwapata angalau 70 akawajengea uwezo wa kuweza kugombea nafasi hizi kwa kweli ni jambo jema sana na anastahiki pongezi nyingi.

Ila katika hili nilikuwa naomba aangalie sana kwa sababu kilichotajwa hapa zaidi ni nafasi za kisiasa, nafasi katika vyombo vya maamuzi ambayo ni Baraza la Wawakilishi. Wanayoongea humu ni wanasiasa na kwa bahati nzuri zaidi kwamba sasa tuna vyama vingi vya siasa si chama kimoja tena. Nilikuwa naomba sana katika hili Mheshimiwa aangalie vyama vyote, aangalie wanawake wa kumjengea uwezo wa vyama vyote kama Chadema wawemo, CCM wawemo, CUF wawemo, kisionekane kimeangaliwa chama kimoja tu, itakuwa haileti sura nzuri hata kidogo.

Kwa sababu hiyo nilikuwa nataka ufafanuzi katika hawa wanawake 70 basi atwambie katika hawa kuna CCM wangapi na Chadema wangapi, TLP wangapi, CUF wangapi ili tupate kujiridhisha kwamba haki sawa kwa wote na ndio *transparency*. Hizi nafasi ni vizuri zingekuwa zikitangazwa kila mmoja akaweza kuomba kupatiwa mafunzo ya namna hiyo ili na yeye aweze kushiriki vizuri katika mambo haya ya mabaraza ya maamuzi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye ukurasa wa 20, nigusie kwenye paragrafu ya 43 ambapo katika hili Mhe. Waziri ameeleza juhudi alizofanya kubwa sana, na nataka nimpongeze sana kwa kufanya marekebisho juu ya ukarabati wa nyumba zile za wazee pale Sebleni. Wazee ni rasilimali ya jamii, wazee ni rasilimali ya taifa, hatuwezi kwenda bila ya wazee. Wazee ni *reference* zetu, watafiti mbali mbali wakifanya mambo ya utafiti wa mambo ya kale jambo la kwanza huwafika wazee ambao wanakumbuka zamani zaidi wakawahoji mambo kadhaa. Watu hawa wanahitaji matunzo ya hali ya juu na ndio maana nikasema nataka nimpongeze sana Waziri kwa kurekebisha zile nyumba ili wapate pahali pazuri pa kukaa. Zile nyumba zilikuwa mbovu, zimechakaa sana na wazee tayari walikwishaanza kuwa na roho mbaya na serikali yao kwamba wanawekwa pahali pachafu. Wazee ni watu wa kutunzwa kwa sababu hali zao ni dhaifu.

Namshukuru sana Waziri kwa kufanya kazi hii, ila naomba aongeze juhudi katika kumalizia ule uzio. Kwa sababu kuna watoto vibaka wanakwenda wakiwaibia wale wazee kule, mtu anaweka kiredio chake cha kupata habari akitahamaki watoto wamekichukua. Uzio ule utengenezwe patiwe geti pale iwe si rahisi watoto wa mitaani kwenda kuwafanyia fujo.

Halafukuna Sera inaandaliwa, hii sera ni muhimu sana, mpaka sasa hivi tunawatunza wazee lakini tunaowatunza ni wachache sana. Kwa kadiri tunavyoona katika jamii yetu wazee wako wengi, lakini kwa sababu sera haijakuwepo haijawatafsiri ni akina nani. Kwa hivyo hii sera mimi nilikuwa naomba sana Wizara ifanye haraka ipatikane tuwe na tafsiri nzuri zaidi ya wazee ili tupate kuwashughulikia wazee wengi zaidi. Unapomshughulikia mzee hata Mwenyezi Mungu yuko karibu na wewe, kwa hivyo tujitahidi sana kuwatunza wazee hawa.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti niende ukurasa wa 22, hapa kama nilivyosema mimi leo kazi yangu ni kumpongeza tu mama angu. Ukisoma paragrafu ya 48, kwa kweli Mheshimiwa katoa mfano mzuri sana na mfano huu nilitaka niwaombe Waheshimiwa Mawaziri na wao wauige si vibaya. Kasema kwamba Ofisi ya Mhe. Waziri imesaidia kuboresha mfuko wa watu wenye ulemavu, kuwanunulia vitabu wanafunzi wa skuli ya Chwaka na kumsaidia mtu mmoja aliyekuwa mlemavu Pemba. Lakini ukiangalia

kiambatanisho Nam. 2 kimeeleza mambo mengi sana ambayo Ofisi ya Mhe. Waziri imefanya kama haya yafuatayo.

Mfuko wa watu wenye Ulemavu	Shs 500,000/-
Ununuzi wa vitabu	Shs 200,000/-
Kumsaidia mtu mwenye ulemavu	Shs 500,000/-
Vikundi vya SACCOS Pemba	Shs 1,000,000/-
Tuvumiliane SACCOS - Fuoni	Shs 300,000/-
Bahari Haikauki - Fujoni	Shs 100,000/-
Utayarishaji wa Soko la Wanawake Pemba	Shs 500,000/-

Huu ni mfano mzuri sana ambao Mhe. Waziri mwenyewe kaamua Ofisi yake ijitolee katika kuinua hali za watu kwa sababu ni mlezi. Kwa kweli Waziri kapewa ulezi, maana kapewa watoto wadogo, kapewa watu wenye umri mrefu ni watu wenye kuhitaji kulelewa ni wanyonge, wanawake ni wanyonge, kwa hivyo ni lazima awe na huruma juu ya mambo kama haya. Nitumie fursa hii kumpongeza sana kwa kazi yake hiyo.

Nikiondoka hapo niende ukurasa wa 27 kuna paragrafu hii ya 59 inazungumza watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Unajua hili neno kulitamka unaliona ni jepesi lakini watoto wenye mazingira magumu ni wengi mno na kwa kweli ni tatizo kubwa sana katika jamii yetu. Katueleza Mhe. Waziri kuna taasisi moja anashirikiana nayo ya Kimarekani inaitwa *Major Evaluation* na kazi yao kubwa ni kujaribu kuangalia ule mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya watoto wenye mazingira magumu. Mimi naomba huu utafiti wanaoufanya wauharakishe ili mfumo huu uweze kupatikana. Nadhani ndani ya mfumo huo kutakuwa na vitendo vya kuwatambua hawa watoto wanaoishi katika mazingira magumu ili tuwapate kwa ukamilifu tuweze kuwashughulikia.

Mhe. Mwenyekiti, jamii yetu ina watoto wengi sana wenye mazingira magumu, kuna watoto wametelekezwa, kuna watoto wanazaliwa kwa kweli sio wa kisheria, wanaishi katika mazingira hawana familia ya kuwasaidia. Lakini katika nchi yetu hii tulikabiliwa na majanga hivi karibuni tumeachiwa mayatima wengi mno nao pia ni watu wenye mazingira magumu sana hao. Nilikuwa naomba huu utaratibu uharakishe ili hatimaye vigezo vipatikane na utaratibu uandaliwe wa kuweza kuwapata hao watoto na kuwafanyia matunzo. Ni jambo moja ambalo litatusaidia sana katika jamii.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti ambalo nataka lizungumze na watu wengi wameligusia lakini kwa umuhimu wake naona na mimi niliseme tena, nilishawahi kulisema huko nyuma lakini na leo nataka nilizungumze tena ni suala la udhalilishaji wa watoto.

Mhe. Mwenyekiti udhalilishaji wa watoto umekithiri na mimi nataka niilaumu kidogo serikali kwamba haijakuwa makini katika hili. Tunapata taarifa watoto wanadhalilishwa leo utahadithiwa mambo mpaka utaona kichwa kinakuuma. Ukija ukiangalia upande wa pili ni hatua gani zilizochukuliwa hakuna hatua za msingi zinazochukuliwa, changamoto nyingi tu sijui hakuna DNA, sijui hakuna jambo gani. Kuna mambo mengine hayahitaji hata hiyo DNA wale watoto wenyewe wanahojiwa wakipata mwanasaikolojia mzuri anawahoji wanatoa ushahidi wa kutosha hapahitajiki kupimwa. Kwa nini mpaka leo hatujaona watu walioadhibiwa kwa masuala haya?

Tukizungumza watoto wanaodhalilishwa tusifikirie kwamba kudhalilishwa ni kule kufanyiwa vitendo viovu vya kunajisiwa na vyengine. Udhalilishaji mwengine unatokana na talaka za ovyo ovyo. Tumo wanaume humu mtu ukimtizama tu mkewe keshamuacha. Akishamuacha akitaka asitake watoto aliozaa nao watadhalilika kwa sababu uzoefu unatuonesha kwamba hakuna mtu anayeweza kumtunza mtoto wa kambo vizuri si mwanamke si mwanamme. Watoto wanaweza kulelewa vizuri na baba yao aliyewazaa na mama yao aliyewazaa. Ukimuacha mwanamke ukimuachia watoto yule mwanamke ataolewa, baba atayemuoa yule mwanamke hatowatunza wale watoto. Ukiwachukua wewe mwanamme utalazimika kuoa mke mwengine, yule mke utakayemuoa hatowatunza kama ambavyo angewatunza mama yao mzazi.

Mimi nilikuwa nadhani Mhe. Waziri atoe nasaha sana na ikiwezekana si vibaya kufanya semina na mashekhe, watawanyike mitaani watoe mawaidha kuachana si vizuri, maana yake kuacha hata Mwenyezi Mungu kaweka kuwa ni dharura tu labda wasipoachana watadhuriana lakini kama kuna *alternative* nyengine basi ni afadhali waishi na matatizo yao lakini wasiachane lengo ni kulea watoto vizuri. Nasema watoto wanadhalilika kwa talaka.

Lakini pia kuna akina baba wengine tuna tabia mbaya ukishamuona mwanamke mwengine unayempenda zaidi unakwenda kumuoa yule, huyu mkeo huku unamkimbia. Tena unamkimbia hasa, maana unamuachia watoto humpelekei chochote cha huduma. Matokeo yake yule mama anahangaika, ukiuliza vipi, unaambiwa mume wake anaye lakini kamtelekeza. Mhe. Waziri mambo haya ilikuwa uyachukulie hatua kali sana, ukimkuta mtu kamtelekeza mke wake ni afadhali tumpeleke Mahakamani kwa sababu sio kwamba anamdhalilisha yule mwanamke tu lakini anawadhalilisha na wale watoto na hatimaye ndiyo hii omba omba inaongezeka mitaani.

Idhilali nyengine inafanyika zaidi katika taasisi za taaluma tumetaja sana vyuo vya Qur-an. Mimi naumia sana kusema walimu wa vyuo vya Qur-an wana tabia hii. Tulipokuwa tukisoma sisi katika watu waliokuwa

wakiheshimika sana mitaani ni walimu wa Madrasa. Ni watu ambao kwa kweli walikuwa ni rufaa ya baadhi ya mambo yetu mengine, ni watu wanaheshimika, watu wanajiheshimu, watu wametimia. Lakini karne hizi tulizonazo mambo yanabadilika kweli kweli. Mimi nadhani wengine wanajitia tu kuwa ni walimu wa chuoni lakini si walimu wa chuoni ni watu wana malengo yao mengine. Ukiangalia *speed* ya kuharibu watoto inayotokea humu katika vyuo vya madrasa ni kubwa.

Nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria basi kufanyike utafiti maalum na uratibu wa karibu sana ikiwezekana kuna mpango wa Ofisi ya Mufti inaanza kusajili vyuo vya Qur-an basi lazima kwanza katika kusajili basi tuangalie sifa za wale walimu wanaosomesha je, wanaelekea kuwa ni walimu wanaweza kuwalea watoto wetu vizuri. Mtu unamkuta mwalimu wa chuoni lakini mambo yake yanakuwa ya ajabu ajabu na wala sio siri. Maana katika Zanzibar bahati nzuri hakuna siri, lolote linalofanyika linaenea katika jamii haraka sana. Tukinusanusa tu kwamba mwalimu wa madrasa fulani ana tabia hii mimi nadhani apigwe marufuku mara moja kukusanya watoto wetu akawaharibu.

Mhe. Mwenyekiti, tusije tukajikuta siku moja kwa sababu watoto hawa ndio nguvu kazi ya keshokutwa, lakini kwa utaratibu huu na *speed* hii tunayokwenda tusije tukajikuta siku moja hatuna nguvu kazi. Mheshimiwa mmoja kasema hapa unaweza ukawakuta watu si mwanamke wala si mwanamme huwezi kujua ni mtu wa aina gani. Mimi nilikuwa nalisisitiza hili kwa msisitizo mkubwa sana lifanyiwe kazi na ikiwezekana vitendo hivi tuweze kuvikomesha mara moja katika jamii yetu.

Baada ya kusema hayo machache Mhe. Mwenyekiti mimi naunga mkono hoja hii ila namuomba sana Waziri afuate ushauri huu tunaoutoa kwa ajili ya kurekebisha mambo yetu haya. Ahsante.

Mhe. Mohamed Mbwana Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu (SW) kutujaalia mchana huu kuwepo hapa kuendeleza majukumu yetu ya msingi. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuwa leo ni siku ya mwanzo wa Mwezi wa Ramadhani. Mwenyezi Mungu atujaalie *taufiq* tuifunge Ramadhani yetu kwa salama na tuyapate hasa yale matunda ya Mwezi wa Ramadhani.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Vijana, Wanawake na Watoto, Mhe. Zainab kwa kuwasilisha hotuba ya wizara yake kwa ufasaha na kwa umakini sana. Lakini pia nachukua nafasi kuwapongeza watendaji wake wote kwa mashirikiano yao makubwa mpaka leo tokea tulipoanza kuzipitia bajeti mbali mbali ni Wizara ya kwanza hii kuwasikia

Wajumbe wengi kusema kwamba tunaunga mkono kwa asilimia mia moja. Mhe. Zainab Omar hongera sana na watendaji wako.

Mimi mchango wangu utakuwa si mkubwa sana kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati hii. Lakini pia nimepata faraja kubwa kuona kwamba Wajumbe Waheshimiwa wengi wa Baraza lako katika bajeti hii tayari wameshaiunga mkono, kwa hivyo ni dhahiri kwamba hii bajeti Mhe. Zainab Omar itapita kama umeme.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niende kwenye kitabu hichi ukurasa wa 41 paragrafu ya 90, amewasilisha maneno haya naomba kunukuu.

"Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na kazi yake ya kuyashughulikia na kuyapatia ufumbuzi malalamiko yanayohusu wanawake ambapo kwa mwaka huu uliopita jumla ya malalamiko 26 Unguja na 63 Pemba ya wanawake yalipokelewa na kupatiwa ushauri na maelekezo yanayofaa ... (**Angalia kiambatanisho Na. 9a na 9b).**"

Twende kwenye kiambatanisho Nam 9 (a) Kinaeleza malalamiko ya wanawake Unguja Kiwilaya kuna aina ya lalamiko kupigwa,

Wilaya ya Mjini	-
Wilaya ya Magharibi	2
Wilaya ya Kaskazini 'A'	3
Kaskazini 'B'	2
Kati	-
Kusini	-
Jumla ya malalamiko hayo	**7**

Kijumla napata faraja kiasi fulani kwamba malalamiko mengi katika Wilaya za Unguja yanaonekana ni machache. Nataka niende katika kiambatanisho Nam. 9(b) malalamiko ya wanawake Pemba Kiwilaya aina ya lalamiko halafu kuna Wilaya hapa, kuna migogoro ya ndoa kama hivi,

Wilaya ya Chakechake, kuna malalamiko	33
Mkoani	3
Wete	3 na
Micheweni	1

Tukienda katika lalamiko la pili kuhusiana na masuala ya kupigwa ni kama ifuatavyo,

Wilaya ya Chake chake ina malalamiko	2
Mkoani	-

Wete	1
Micheweni	-

Kesi za madai ya mali hapa kuna malalamiko kama haya:-

Wete	1
Micheweni	1

Kesi za kutelekezwa:-

Wilaya ya Chakechake	3

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kuna shambulio ya aibu, Chakechake malalamiko mawili, madai ya mahari, Chakechake malalamiko manne. Ujauzito Chakechake kuna malalamiko mawili. Kuna jumla ya malalamiko 46 katika Wilaya ya Chakechake, ambapo Mkoani kuna malalamiko manne, Wete manane, Micheweni matano.

Kwa hivyo nimuulize Mhe. Waziri hii Wilaya ya ChakeChake ina nini hata ikawa malalamiko ni mengi kuliko Wilaya zote za hapa Zanzibar. Malalamiko mengi yanaonekana kwamba ni migogoro ya ndoa. Hivyo wanawake wa Chakechake hawatakiwi au hawataki. Kwa hivyo nakuomba Mheshimiwa hili ulifanyie kazi kwa kina tujue kwamba kwa nini Wilaya ya ChakeChake inazidi malalamiko kuliko Wilaya nyengine za Zanzibar.

Nikiondoka hapo niende katika Ofisi Kuu pale Pemba. Nasikitika sana kuona Ofisi Kuu haina jengo lake mahsusi jengo liliopo ni la kukodi na Wizara inatumia Shilingi milioni 18 kila mwaka kukodi eneo la kufanya shughuli zake. Naomba hapa utupe maelezo ya kina ni lini basi Ofisi yako au Wizara yako ya hapa Pemba itajenga jengo la kuweza kujitegemea bila ya kutegemea jengo la kukodi.

Mhe. Mwenyekiti, niende kidogo katika kitengo cha jinsia kule Pemba. Tulipokwenda Pemba na Kamati hii tuliona kwamba mpaka kamati inapita Ofisa wa Kitengo cha jinsia hajaajiriwa pale hayupo, je ni lini Ofisi yako Mhe. Waziri itamuajiri Afisa huyu ili aweze kufanya kazi vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Idara ya Ustawi wa Jamii. Hapa nitazungumzia kuhusiana na wazee. Turudi nyuma kidogo kwa kweli wazee ni rasilimali kubwa, pamoja na kusema kwamba vijana ni rasilimali ni kweli lakini vijana hawawezi kuwepo kama si wazee. Mhe. Mwenyekiti, wazee wa Kizanzibari kwa kweli tumewaweka nyuma sana, tunapotaja wazee katika Baraza tunahusisha wazee waliokuwepo Sebleni, waliokuwepo Welezo na

Limbani. Hawa ni wachache, Zanzibar ina wazee wengi kwa nini serikali haiweki Sera maalum kwa ajili ya kuwashughulikia wazee wa Kizanzibari.

Mimi naamini uchumi uliopo Zanzibar umechangiwa kwa asilimia kubwa sana na wazee hawa. Wazee wa Kizanzibari ni wakulima, lakini uti wa mgongo wa uchumi wa Zanzibar unatokana na kilimo cha mikarafuu waliyopanda mikarafuu ile ni nani kama sio wazee. Je, haujafika wakati wa wazee wa Kizanzibari ambao wamefikia umri wa miaka 60 na zaidi kuwapa posho. Jamani Zanzibar ina umasikini wa kiasi gani kutowathamini. Leo vijukuu na vitukuu vinafaidika wazee wanakufa wakiwa na unga wa meno.

Mhe. Waziri naiomba wizara yako kwa nguvu zote iwaangalie wazee wa Kizanzibari ili na wao wajisikie wapate matunda ya nchi yao waliyotangulia wameshatangulia lakini waliokuwepo wafaidike. Zanzibar inaongozwa kwa uchumi wa mikarafuu na minazi. Unguja minazi imepandwa na nani? Si Wazanzibari wenyewe. Hili Mheshimiwa nakuomba uliunge mkono katika kipindi kijacho basi Wazee wa Kizanzibari japo kwa asilimia ndogo wajisikie kwamba wapo katika nchi yao na inawathamini kama wao walivyotumia nguvu zao kuweka uchumi imara katika nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende katika SACCOS ya Mkono kwa Mkono pale Wete kimefikia hatua gani.

Baada ya hapo niende katika tatizo ambalo Wajumbe wengi wamelizungumza, hili ni tatizo la omba omba Zanzibar. Kwa kweli Mzanzibari yoyote ambaye anayeyaangalia maadili yetu ya Zanzibar basi tatizo la omba omba linamuuguza sana. Hili ni tatizo na lipo na miongoni mwa omba omba ni vijana wenye nguvu. Waliposema hapa baadhi ya wachangiaji na hata kitabu kinaeleza kwamba asilimia kubwa ni wanawake. Ni kweli kuna wanawake wamezoea omba omba na wana tabia miongoni mwao hii ifuatayo.

Mwanamke anaondoka kwake nafikiri ana gunia maalum amelitia matambara analivaa kama mjamzito, unamkutia kitumbo kipo juu, anakuomba, unampa, anakwenda zake na safari yake siku ukipita nyumbani kwake jioni kitumbo kimenywea, mimba hamna. Unajiuliza huyu mama keshajifungua. Asubuhi unamkutia tayari kitumbo kipo juu tena. Hali hii kwa kweli inawadhalilisha akina mama na inaidhalilisha Zanzibar. Nawaomba Wazanzibari, turudieni katika utamaduni wetu wa kuridhika na kile tunachopata. Miongozi mwa wanaoomba si kweli tu kwamba mia kwa mia walikuwa hawana uwezo. Yupo Mheshimiwa mmoja hapa kachangia akasema kwamba unamkutia omba omba jioni ikifika ana karibu shilingi laki mbili, ikipita gari anasimamisha

anaomba, aliyevaa vizuri anamsimamisha anamuomba, mpandaji wa baskeli anamsimamisha, naomba hichi, naomba nauli naomba kitu gani.

Mheshimiwa Wizara yako inapaswa kufanya utafiti wa kina juu ya hili na kulikemea kwa nguvu zote ili Zanzibar iendelee kuwa na heshima. Aibu Zanzibar yetu inaingia wageni, wanakuja. Mtoto kijana anamnyooshewa mkono mgeni, naomba nauli. Yule mgeni, pengine hata lugha unayoizungumza wewe haitambui.

Mhe. Mwenyekitik ili kuiweka Zanzibar katika hadhi na heshima yake nakuomba suala hili kwa nguvu zote tushirikiane Wazanzibari kulipiga vita na ikiwezekana kwa vile tunawatumia Masheha kila aina ya shughuli zetu. Tufanyeni sensa kwa Masheha zile omba omba zote tuzijue kwamba omba omba hawa wanatoka eneo gani, omba omba hawa wanatoka wapi ili tuwape taaluma ya kutosha ili kuepukana na hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache niseme kwamba na mimi naunga na Waheshimiwa waliounga mkono hoja hii kwa niaba ya Wananchi wangu wa Jimbo la Chambani naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kusema machache katika Wizara yetu hii. Kwanza kabisa naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya.

Lakini pia nichukue fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza wanaume wote ambao wamechangia bajeti hii ya akina mama. Lakini pia na wale waliokuwa hawakuchangia naamini wanatuunga mkono sana akina mama kwa sababu Mwenyezi Mungu amewaambia Arijalu Qawwamuna Alan-nisai, kwa hivyo hilo hawawezi kulipinga isipokuwa wataendelea kuwa wasimamizi wa mambo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka nianze mchango wangu katika ukurasa wa 38 kwenye Nam . 7 ambapo imeeleza kama hivi,

"Kuendeleza na Kuimarisha miundombinu ya uzalishaji wa mazao ya kilimo cha *Rosela* na mboga mboga kwa vijana Unguja na Pemba."

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kuwapongeza sana kwa uanzishwaji wa jambo hili lakini nataka na mimi niungane nao na niwaombe sana katika hiyo elimu, mimi naihitaji sana katika Mkoa wangu wa Kaskazini.

Nataka nimwambie Mhe. Waziri nataka niende hasa katika Wizara yake ili nikajue utaratibu gani unatumika wa kuweza kupata elimu hii ili vikundi viweze kufaidika na maendeleo haya.

Pia nikienda ukurasa wa 39 kwenye Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto, wenzangu wameeleza kwa kina na mimi naomba nitilie mkazo kwenye Nam. 4 ambapo panaeleza uhamasishaji. Uanzishwaji wa Benki ya Wanawake na mimi naunga mkono na wale wote ambao wameliunga mkono jambo hili ili itakapoanzishwa benki hiyo basi wanawake tunaweza tukapata maendeleo ya kutosha. Pia Nam. 6 inasema kwamba, kuratibu na kusimamia uanzishwaji wa Mabaraza ya Watoto katika ngazi zote hili pia wenzangu wamelieleza na mimi nalitilia mkazo.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa 44 kwenye paragrafu hii ya 97 ambapo Mhe. Waziri ameielezea siku ya wanawake duniani kwamba huwa inaadhimishwa kila ifikapo mwezi wa Machi ambapo kauli mbiu yake itakuwa ni ‘Ahadi ni **deni, wakati umefika kumaliza vitendo vya udhalilisha dhidi ya wanawake.'** Mheshimiwa napenda niungane na kauli hii na niseme kwa kweli udhalilisha juu kama hatutochukua juhudi kubwa sisi wanawake wenyewe ambao yanatukumba matatizo haya basi tuelewe tutaendelea kudhalilishwa siku hadi siku. Naiomba sana Wizara juu ya jambo hili. Tukiwemo sisi Wawakilishi wanawake ambao tunawawakilisha wanawake wenzetu kulichukua jambo hili kama ni changamoto kubwa kwetu, na tukaweza kukaa kwa pamoja kati ya Wizara na sisi Wawakilishi na wale maafisa wetu wa wanawake na watoto katika Wilaya zetu na kuweza kupanga mikakati ya pamoja ambayo inaweza kwa nguvu ya pamoja tunaweza tukalifikisha jambo hili mahala pazuri.

Nakuomba sana Mhe. Waziri uweze kukaa nasi na tutapokaa na watendaji wako ambao wana elimu mbali mbali za kuweza kutupatia sisi, basi kwa umoja wetu tunaweza kulifanya jambo hili na tunaweza tukafanikiwa kwa kiasi kikubwa kuondosha udhalilishaji huu.

Mhe. Mwenyekiti niende katika *paragraph* ya 98 ambapo pia Wizara huwa inaadhimisha siku 16 za kupinga ukatili dhidi ya wanawake na ujumbe wa mwaka 2012 ulikuwa ni *amani ya duniani huanza nyumbani tupigane na vitendo vya utumiaji wa nguvu dhidi ya wanawake na watoto*. Mheshimiwa naungana na ujumbe huu na nichukue fursa hii kuwataka wale kinababa wote ambao wanatumiliki wanawake kuona ni kweli wanaondosha ukatili dhidi ya wanawake, wale wanaopiga basi waache kutupiga, waache kutunyanyasa kwa mambo mengine na Mhe. Mwenyekiti naomba ninukuu kuna msanii ambaye alisema, *'mwanamke hapigwi kwa fimbo wala mateke, hupigiwa kwa mapambo hilo ndilo pigo lake, na ukiyaharibu mambo utajuta mwisho wake'.*

Mhe. Mwenyekiti kwa kauli hii niwaombe sana kinababa, kinamama, ndio ambao tumewazaa na ndio ambao tunaendelea kuwazalia watoto na kuwalea. Kwa maana waendelee kututunza ili tubaki katika hali yetu ya kawaida na sio kutusababishia vilema ambavyo havistahiki.

Mhe. Mwenyekiti, pia nilitaka nichangie, wenzangu walisema sana kuhusu omba omba na ni kweli hili jambo si zuri lakini mimi nataka niende kwa wale wanawake ambao wanajidhalilisha wao, lakini hatimae wanatudhalilisha na sisi. Niende kwa wanawake hawa ambao wanakuwa wanakuja hasa hapa kwetu kwa lengo la kujiuza miili yao. Mhe. Mwenyekiti jambo hili si zuri linawadhalilisha wao na linatudhalilisha sisi na kutuondoshea heshima, na wale ambao wanavaa nguo ambazo hazistahiki kusema kweli.

Pia mimi niiombe sana Wizara ishirikiane na Wizara hii ya habari ambayo ina kazi kubwa ya kulinda mila na utamaduni wetu kuhakikisha wanazipitia upya sheria zile, ama kama hazipo ziweze kutungwa ili kuhakikisha mila na utamaduni wa nchi hii unaendelea kudumishwa kwa mavazi na hata silka zetu na utamaduni wetu.

Mhe. Mwenyekiti mimi niendelee na mchango wangu katika suala zima la udhalilishaji na nataka nilizungumzie sana, wenzangu wamesema sana kuhusu udhalilishaji lakini huu udhalilishaji uko wa aina nyingi na mimi nataka niukemee sana huu ambao umejitokeza kwa kasi kubwa hivi sasa ambao watoto wa kiume wanadhalilishwa sana ambalo linaitwa kulawiti.

Jambo hili kwa sasa linaonekana katika nchi yetu ni kubwa tuliwahi kupata semina hapa na tukaambiwa jambo hili watu wamefanyia utafiti linaonekana lipo kwa ukubwa mno hapa kwetu. Mhe. Mwenyekiti jambo hili si zuri na jambo hili kama tunavyoelewa nchi yetu visiwa vyetu hivi asilimia kubwa ni waislamu na tunaelewa Mwenyezi Mungu alivyolikemea jambo hili katika *qur-an*. Kwa hivyo mimi nawaomba au niwasihi sana wenzangu waliomo katika Baraza hili kwamba tuelewe wanaodhalilishwa ni watoto wetu ambao tumewazaa, na uzazi usisikie unauma, huwezi ukaona mwanao ambaye umemtegemea kwamba umemzaa ni mwanamme halafu ukaja wewe ukasikia maneno mengine unaumia zaidi.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti nimuombe sana Mhe. Waziri na wanawake wenzangu wote waliomo katika Baraza hili, suala hili kwa kweli sasa wanawake ambao sisi ndio tunaodhalilishwa, maana yake kudhalilishwa kwetu tunadhalilishwa sisi lakini tunadhalilishiwa na vile ambavyo tumevizaa. Kwa hivyo nikuombeni sana hili tulikamie na tuungane kwa pamoja tuweze kufanya kazi pamoja na Wizara na tusiiwachie Wizara peke yake, tuungane nayo sasa katika kuona hii ni changamoto kubwa imetukabili

na tujipange vizuri na kuweka mikakati ili tuweze kukabiliana na jambo hili. Hata kufanya utafiti pamoja na kuwa unafanywa, sasa wanawake nasi tupate nafasi ya kufanya utafiti huo ili tuweze kuona jambo hili liko kwa ukubwa gani au kwa kiasi gani.

Lakini pia tuweze kuhakikisha sheria kali zinachukuliwa dhidi ya wale ambao watabainika na udhalilishaji huo. Ukiacha mwenzangu aliwahi kusema hapa kwenye mawio imetolewa kama mtoto amemlawiti mwenzake lakini hukumu iliyotolewa haikuwa ya kuridhisha kusema kweli Mhe. Mwenyekiti wakati jambo hili kweli tunaamua kulikomesha hukumu ile haituridhishi, na naomba hata Wizara iweze kufuatilia kwamba hukumu zikiwa ndogo kama hizi basi suala hili tujue kama litaendelea kudumu.

Mhe. Mwenyekiti, wakati akichangia Mhe. Hija hapa aliwahi kusema pia kuwaambia Wizara kama na wanaume na wao wanadhalilishwa ufanywe utafiti huo. Mimi naungana nae kwa hili kwa sababu pia wapo wanawake wenzetu ambao watukutu wanawadhalilisha wanaume. Na wanawadhalilisha kwa kuzikataa ndoa zao wakihakikisha kwamba wana watoto na watoto wale wataendelea kuyumba, pengine hakuna sababu za msingi.

Hivyo Wizara ikifanya mikakati ya kufanya utafiti huu inaweza pia ikajipunguzia mzigo ule wa kuona talaka kwanza zinatolewa kiholela holela lakini pia inaweza ikadhibiti kuziweka vizuri zile ndoa kwa sababu tunaweza pale tukawanasihi. Na hata Mhe. Jussa alipokuwa akichangia pia alisema Wizara hii iweze kufanya na Ofisi ya Mufti ambapo kule pia inaonekana mashekhe talaka zinatolewa bila ya kuzingatia saa nyengine. Lakini tunapofanya nao kazi pamoja maana yake tatizo tutaweza kulijua kwa pamoja tatizo liko wapi na tutaweza kulidhibiti pengine talaka zile zinazotolewa kiholela na kusababisha watoto hawa wa mitaani kuwa wengi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi baada ya kusema hayo naomba sana sana kuiunga mkono hotuba hii, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa Kaskazini kwa asilimia mia moja, lakini msisitizo wangu bado suala la udhalilishaji hasa watoto wanaume linaniuma sana na hili naomba wanawake tujifunge mikanda ili tuweze kulifuatilia kwa undani na tuweze kuchukua hatua zinazohusika.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi kunipa fursa hii niweze kuchangia mchango wangu kama mwanamke kwanza halafu tena niweze kuona jinsi gani Serikali tumejitahidi kwa hili. Kwanza niunge mkono hoja hii asilimia mia kwa mia halafu nimpe pongezi Waziri wetu jana kila unayemsikia huko nje anasema leo mama kaamua. alisoma hotuba yake vizuri kwa muda mfupi kikakamavu, kwa hivyo kwa kweli wanawake nje wametusifu sana.

Pia napenda niipongeze Wizara yake pamoja na wafanyakazi wake wote kwa msaada mkubwa wanaokupa kufanya nao kazi maana bila ya wao ukweli usingekuwa na ushujaa huu. Kwa hivyo nawapa nao pongezi kwa kazi nzuri wanayoifanya. Baada pongezi ilikuwa nianze sasa nizungumze na mimi kwanza kama mwanamke na shida tunazozipata. Kwa hivyo tuache ya serikali kwanza tuzungumze ujanajike.

Mhe. Mwenyekiti, suala la matatizo ya wanawake sio suala jepesi sio kwa watoto sio kwa watu wazima, ile kuwa mwanamke peke yake ni mtihani. Tunapata mitihani wanawake inaweza kuwa mimi sijapata lakini wapo wanaopata. Sasa nataka niseme mimi kwa sababu wanaopata ni wanawake, kuna maisha tunaelewa tunazaa huo ndio mfumo uliopo. Tunapoolewa tunakubali, tunaulizwa tunasema ndio kwa hivyo tunaolewa.

Bahati nzuri huo ndio utamaduni wa kiislam, mwanamke anaolewa, mwanamme anaoa. Wenzetu wakristo wanaoana bibi anatoa ruhusa na bwana anatoa ruhusa wanaoana sisi tunaolewa na tumekubali hilo kwa sababu ni waislamu, tumekubali dini yetu sina tatizo nalo. Lakini kabla hujaolewa mume anakuja kukuposa unamkubali kwa kutegemea kwamba ukienda kule maisha yatakuwa mazuri na ndio maana ukiulizwa umekubali unasema nimekubali, kwa hivyo unaolewa unakwenda zako kwa mume unakwenda kuanza maisha.

Sasa bahati mbaya au nzuri wenzetu wana fursa nyingi za kuoa mke zaidi ya mmoja, wewe utaolewa utakuwa wa mwanzo, mwanamme pale unamkuta hana chochote mnakula dhuli mnahangaika, unakusanya, unabania na yeye anakwambia na mimi naanza maisha, mimi najenga, mimi ninafanya hivi nafanya hivi, maisha yakimwendea vizuri keshajenga, keshamaliza wewe tena unakuwa huna thamani, anatafutwa mwengine kichinchiri anaolewa anatiwa ndani ya nyumba umehangaika weee hakuonei huruma, wanawake wanavumilia sana, wanaume hawavumilii tatizo dogo tu anaweza akakutwanga talaka ya kwanza, hujakaa vizuri takala ya pili, hujakaa vizuri talaka ya tatu, mumeo unamtaka unaona dhiki vya kufanya huna vitoto vimekuzunguka. Akikupa talaka ya kwanza ukirudi unarudi shingo upande unajua matatizo yapo lakini utafanyaje vitoto vimekuzunguka. Wengi wao hawana kazi cha kuwalisha hawana anarudi kwa sababu ya watoto.

Na mara nyingi wanawake wanarudi kwenye ndoa kwa sababu ya watoto. Anakwenda kule kwa sababu ya watoto wake. Unajua kanga alisema vipi kwamba *mtoto hamlishi chui*, kanga analala juu ya mti watoto anawaacha, lakini binaadam hatufanyi hivyo wanawake wanasononeka sana kwa ajili ya watoto wao. Kama kampa talaka mwengine anamwachia na watoto na ilhali anajua hana uwezo anahangaika nao weee hao wanaopita wakiomba na

watoto wao wengi wao wameachwa, cha kuwalisha watoto hawana na si kama waume zao wanakuwa hawana pesa hawana uwezo wanakuwa nao, lakini labda kwa kuwakomoa au kwa dhamira yoyote waliyonayo wanawaachia na watoto. Wanahangaika na watoto wao wanapita wakiomba, hawezi akamwacha mwanae akafa njaa.

Kwa hivyo kweli kuna kesi ambazo mtu anaomba kwa sababu kaamua lakini wengine wanaomba kwa kweli wanakuwa wana dhiki. Sasa ninafikiri tutafautishe, mimi ninafikiri labda sasa sisi tunaokuwa tuna uwezo tujitahidi kwa wale ambao tunawahisi wana matatizo basi tuwasaidie, yule unayemuhisi kwamba aaa huyu anafanya tu tufanye tuone jinsi gani tutavyoweza kuwaepuka.

Tupo Baraza la Wawakilishi hapa huu mwezi wa Ramadhan, kuna sikukuu inakuja tunaambiwa tutoe zaka, hebu basi na tufanye mfuko hapa ambao tunachanga zaka Wawakilishi tuwape watoto na mama zao wenye matatizo, ikifika angalau siku ya sikukuu mzazi aweze kumnunulia chochote mwanawe. Hakuna mtoto anayeona raha kuwa sikukuu asipate cha kuvaa. Mzazi utastahmili lakini watoto hiyo haiwezekani. Na si watoto, wazee pia wale waliokwisha kukusanywa kule labda wapo Sebleni, wako Welezo na kwengineko waliko na watoto wale ambao hawana wazazi mayatima tujitahidi kuwasaidia, tuelekeze na sisi sadaka zetu huko ili na wao waweze kupata kile ambacho wengine wanakipata.

Lakini hapa nimesikia wanawake wenzake wengi wanazungumza na ndio wengi leo waliozungumza lakini tujue kitu kimoja kwamba wanawake bila wanaume hatusimami, familia ni wanaume na wanawake. Kwa hivyo tushirikiane na wanaume kwa pamoja ili familia zetu ziwe nzuri. Kwanza sisi wanawake ngoma yetu haikeshi, tukikaa peke yetu saa moja tu tushatiana vidole vya macho. Kwa hivyo tuwape nafasi na wanaume washiriki katika hili, watoe ushiriki wa kutosha ziwe familia madhubuti, tutunze watoto wetu tufanye yote yale yanayostahiki. Bahati mbaya ulimwengu hauendi hivi.

Tulikwenda kwenye mkutano wa WHO mwaka huu; moja katika mada ambazo zinatiliwa mkazo ni suala la ndoa za jinsia moja na utoaji mimba, na wanapita wanafanya kampeni kikundi kwa kikundi wanataka hayo yakubalike na wengine wanadiriki mpaka kusema kwamba nchi tutainyima misaada kama hili hamkulikubali. Hili janga ni janga kabisa. Kwa hivyo sasa kama huko juu wenye pesa zao wanafanya hivyo seuze ulimwengu tulionao na watoto tulionao. Kwa hivyo sasa hivi tunao watoto wa kike na wanawake wenzao wanaume, wanaume wenzao haya sasa yamekuwa ndio *fashion* ya ulimwengu. Ninafikiri hapa kwetu tujitahidini wazazi na hasa kama familia zitakaa pamoja kuwalinda watoto wetu wasitumbukie katika majanga haya.

Lakini nilizungumzie suala sasa linalozunguzwa sana hapa la ubakaji. Kuna NGO nyingi zinajitahidi pamoja na mashirika, NGO za kitaifa na za kimataifa kuhakikisha kwamba inawatoa watoto katika kufanya kazi wakiwa watoto wadogo. Kile ni kimoja ya chanzo ambacho kinawafanya watoto wadhalilishwe wa kiume na wanawake. Ziko NGO nyingi tu zinafanya hivyo, zinawanunulia watoto *uniform*, zinawarudisha watoto maskulini, wanaume na wanawake, kuna za wanawake watupu ambazo zinataka wanawake wainuke. Lakini juhudi hiyo inafanywa pamoja na serikali ndio maana kumeanzishwa *one stop centre*. Mnazi Mmoja ipo *one stop centre*, mimi nilikwenda makusudi kutafuta kwani kinachoendelea huku ni nini? Kwa nini tunalalamikiwa kila siku na *one stop centre* iko hapa na kesi kila siku zinakuja, kwa nini kesi hazifiki mwisho? Sababu ndio tutasema zile zile, Polisi hawafanyi uchunguzi, ukienda Polisi wanakwambia jamani sisi tunafanya mpaka tunakamilisha.

Majaji wanasema aa wazazi hawaji, mimi ninajiuliza kwani kuna Polisi kuna daktari hawa hawatoshi kutoa ushahidi. Wako pale *one stop centre* Polisi yupo, ningependa kama kungekuwa na uwezekano kwa sababu hawa wazazi kama kweli wanahangaishwa, anakwenda mara ya kwanza, mara ya pili anachoka, hana nauli, hana uwezo anajua kwamba hapati hana pesa ya kutoa rushwa. Sasa kama hizo ndizo sababu basi mimi ningependekeza kwa serikali yetu nipende Mwalim Abuu tuwasaidie wazee kwa sababu hizi kesi na malalamiko yameshakuwa mengi. Daktari na yule polisi aliyeko pale akishapeleka yule mtoto pale aliyedhalilishwa na ushahidi upo kamili, basi wale wachukuliwe kama mashahidi ili kupunguza hili tatizo ambalo la wimbi la wazazi kutohudhuria kwa sababu hiyo kwenye Mahkama ili iwasaidie.

Kwa sababu kuna kesi nyengine ziko wazi, kwa hivyo tuwasaidie ili waweze nao watoto wapate haki. Mimi ninafikiri kama serikali wenzangu tushauriane kwa hili ili likubalike kama kutakuwa na uwezekano maana mimi si mwanasheria sijui lakini mimi naona tuwasaidie ili hilo liweze kukaa vizuri. Vyenginevyo labda Mhe. Abuu atusaidie atwambie atatusaidiaje kama serikali, najua mipango ipo lakini yeye kaja Waziri wa Katiba na Sheria. Lakini na mimi pendekezo langu moja hilo ningeomba nalo uliangalie.

Sasa unakuja watoto wameachwa mama kahangaika nao weee ukienda baba unamwambia nisaidie akusomeshee, lakini wewe mama ndio ulimkubali baba mtoto hana kosa umehangaika nae kasoma sasa baba ata haya haoni mtoto anakwenda kumuomba sasa, lakini mama kamhangaikia unakwenda kuomba wewe, huwezi kumwambia mwanao usimpe lakini aa wanaume nalo tulifikirie, tukihangaika na watoto wetu na nyie mjue kwamba mna jukumu msiwaachie kinamama peke yao wakahangaika nao halafu tena watoto

wakakua mkaona kwamba sasa nyinyi kwa kuwa mababa mna haki hizo. Haki mnayo kwa sababu ni baba lakini muwahurumie na wenzenu.

Mimi ningependa kuwashauri wenzetu serikalini nikiwemo pamoja na mimi kungekuwa na kitu maalum, ukimuacha mke na watoto kuwe na sheria Bi Zainab omba sheria. Mtoto akiachwa ahakikishe mume anawalisha watoto wake na kuwavisha kama jukumu linavyomwambia. Tukiwa na sheria kali ya aina hiyo hawatotoka kwa sababu itakuwa sasa ni sheria. Sasa hivi wengi wanapigwa chenga kwa sababu kwa kwenda lalamika hakuna, na sheria inayowalinda wanawake labda haiko nzito kiasi hicho. Kwa hivyo kuwe na sheria inayowabana wanaume wanaowaacha wanawake na watoto wawahudumie watoto wale, kwa sababu hilo ni jukumu lao. Lakini wanaume wakishapata kitu baba hawatusikilizi.

Mfano mzuri kampeni tu mtu utahangaika naye akishapata basi tena umekuwa sie anatafuta mwanamke mzuri mwengine anaoa. Kaeni na wale mliohangaika nao maisha yote, wasaidieni nao wana haki, mnahangika nao leo mkipata msitafute wengine halafu wale mkawadhalilisha wengi wanalalamika kwa hilo. Nasema kama mwanamke sasa maana naona wenzangu nao wanapata shida. Sikusema wasiolewe waolewe lakini tena utaoaje halafu tena yule uliyehangaika nae ulipokuwa huna kitu, leo kwa kuwa umekuwa Mwakilishi tena ndio umuache mkeo ukatafute mwengine halafu yeye usimpe haki yake. Oeni wanne kama mnavyotaka lakini na yule wa mwanzo kama sheria inavyokuruhusuni, mnawadharau ndio maana nasema (*Makofi*).

Tunazungumza kuhusu suala la DNA mimi narudia kusema kesi nyingi hazihitaji DNA. DNA *machine* itanunuliwa tutafanya hayo tunayoyataka na tuko mbioni kama tunavyosema kwa sababu mapesa si kidogo lakini iko siku tutafika mfundani. Lakini kesi nyingi za udhalilishaji hazihitaji DNA lakini zina vielelezo viwazi, mimi kila siku nikisoma kwenye magazeti Bunda, Shinyanga wapi mtu kahukumiwa miaka30, miaka 60 kule DNA imetoka wapi? Hakuna DNA kule wanatizama vielelezo watu wanahukumiwa. Kwa hivyo mimi ninafikiri ifikie wakati wahukumiwe. Wakati wa Karume kulikuwa hakuna DNA na watu wakifungwa miaka mitano mitano hapa, ukitia mimba miaka mitano, DNA ilikuwepo lakini kesi zilikuwa hazikawii. Wakati wa Kitangi watu wamefungwa waliokuwa siku kidogo DNA mashine haikuwepo. Leo hii mpaka DNA kwa msingi gani mnawaachia kwa sababu hawahukumiwi, watu wanafanya wanavyotaka na wataendelea midhali hawafungwi. Mimi ninafikiri DNA isiwe kisingizio anayefanya matatizo afungwe kwa mujibu wa tatizo alilolifanya.

Baada ya kusema hayo ninashukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe muda tulionao ni mdogo mno hautoshi kwa Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba kuweza kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya mambo. Naomba kuchukua fursa hii basi kuja kuimalizia kazi hii hapo kesho kwa kuanzia na Mhe, Waziri wa Katiba na Sheria ili atoe majumuisho kwa baadhi ya mambo baadae Mhe. Waziri anayehusika na Wizara hii atakuja kufanya majumuisho.

Baada ya maelezo hayo naomba kuchukua fursa hii kuliakhirisha Baraza hili hadi kesho siku ya Alkhamis tarehe 11/07/2013 saa 3.00 barabara za asubuhi.

(Saa 8.00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 11/07/2013 saa 3.00 asubuhi)